Nipashe
Jumatano Desemba 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581159
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13




**Mnyukano** kisheria waibuka mawakili rufani ya Sabaya

UKURASA 4



# Mama, watoto mbaroni tuhuma mauaji baba yao

• **Wadaiwa** kukodi watu kwa 800,000/- kutekeleza unyama, ni baada ya... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### TANZANIA MWENYEJI MKUTANO KIMATAIFA CHAKULA



RAIS Samia Suluhu Hassan, ameridhia Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Jukwaa la Mtandao wa Chakula Afrika...

UKURASA WA 4

### MAMLAKA YATOA MSIMAMO KURUHUSU MATUMIZI BANGI

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema haiwezi na haina mamlaka ya kuruhusu matumizi...

UKURASA WA 5

### ROYAL TOUR YAZIDI KUVUTIA WATALII

KATIKA kipindi cha Januari hadi Oktoba, mwaka huu, Tanzania imepokea watalii 1,175,697 kulinganisha na watalii 716,741...






Wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, wakiuza bidhaa zao huku Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikiwataka kujisajili na kutoa risiti za kielektroniki (EFD). **PICHA: MAKTABA**

## Machinga watoa msimamo kauli TRA kulipa kodi, matumizi ya EFD

UKURASA 3

## Vurugu tupu usafiri kwenda mikoani stendi ya Magufuli

UKURASA 2



**MICHEZO** SIMBA NA REKODI KWA MKAPA CAF, YANGA... UK.32 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali kuhusu kilimo katika Mkutano wa AGRA uliofanyika Ofisi za Taasisi ya Bill na Melinda Gates, jijini Washington Marekani jana. **PICHA: IKULU**

# Vurugu tupu usafiri kituo cha Magufuli

**Na Jenifer Gilla**

NI vurugu tupu. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na pilikapilika za usafiri katika kituo kikuu cha mabasi ya kwenda mikoani na nchi jirani cha Magufuli, Mbezi Mwisho mkoani Dar es Salaam.

Huu ni wakati wa watu hasa wa mikoa ya kaskazini kusafiri kwenda nyumbani kwa ajili ya kuungana na ndugu zao kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kusherehekea Krismasi kama ilivyo desturi yao miaka nenda miaka rudi.

Wakati hayo yakiendelea, wako watu ambao wanachukulia usafiri huo kama fursa kwa ajili ya kupandisha nauli na wakati huo huo, wale wanaosafiri kwao ikiwa ni maumivu. Kwa wale wanaokatisha tiketi, baadhi yao kwao ni kipindi cha mavuno.

Kwa sasa, abiria hawezi kukata tiketi siku mbili kabla kwa kuwa wenye magari wanaona watashindwa kuamua nauli wanayopaswa kutoza huku ulanguzi wa tiketi unafanywa na wapiga debe ambao wanaona ni namna ya kujipatia kipato.

"Kaka nahitaji kusafiri siku ya Ijumaa kwenda Arusha nahitaji tiketi," alisema dada mmoja aliyekuwa akitafuta nafasi katika moja ya mabasi kwa ajili ywa kusafiri.

"Dada hatukatishi tiketi siku mbili kabla. Njoo kesho au keshokutwa tutakukatia. Magari yetu yanajaa sana kwa sasa, tunahofia tusije tukakosa gari la kuwasafirisha," alisema kijana aliyekuwa kwenye moja ya ofisi za mabasi katika kituo hicho.

Hali hiyo inaonyesha kuwa wenye magari wanapata abiria wa kutosha na hata nauli walizopanga kwa siku hiyo zinatozwa hivyo hivyo, tofauti na nyakati zingine wanalazimika kushusha hata bei elekezi kwa aina ya basi.

Ni maumivu kwa wasafiri kwa kuwa ulanguzi wa nauli unafanyika huku ukatishaji tiketi za kawaida ukiendelea kama kawaida licha ya serikali kuanzisha utaratibu wa tiketi mtandaoni.

Jana, Nipashe iliweka kambi katika kituo hicho na kushuhudia baadhi ya wasafiri wakilazimika kusafiri kwa gharama mara mbili ya bei elekezi kwa sababu ya kukosa usafiri.

Aidha, mwandishi alikuta mamia ya abiria wakikata tiketi na wengine wakilipia nauli mlangoni kwenye mabasi hali iliyotoa mwanya kwa makondakta kuwalipisha bei kubwa.

Mmoja wa abiria aliyekuwa akienda Morogoro, Hellen Kigosi, alisema alilazimika kulipia nauli ya Sh. 15,000 kwa kuwa alilipia nauli mlangoni wakati abiria ni wengi na huku mabasi yakiwa machache.

"Ndio hivyo dada madereva wanaringa hasa kwa sababu mabasi makubwa yote yamejaza. Sasa haya ambayo siku zote watu hawayapandi sasa hivi ndiyo yamepandisha bei. Hawakuongeleshi mara mbili, unataka lipa nauli hutaki mwenzio analipa anasafiri," alisema.

Abiria mwingine, Nancy Leonard, alisema amelipa nauli ya Sh. 33,000 kwa mabasi yanayokwenda Arusha badala ya Sh. 25,000 ya bei elekezi iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

**TIKETI MTANDAONI ZAKWAMA**

Baadhi ya mawalaka walisema utaratibu wa tiketi mtandaoni unakwaza kwa sababu inachukua muda mrefu mmiliki wa gari kupata fedha.

Mmoja wa mawakala wa tiketi kwenda Moshi, Michael Mtemvu, alisema inachukua hadi wiki mbili kuingiziwa pesa zilizolipwa na abiria kupitia tiketi mtandao hali inayozorotesha utoaji huduma.

"Abiria anakata tiketi leo, anaondoka kesho, hela yake ndiyo tunaitegemea kujaza mafuta gari, kuifanyia marekebisho na kulipa ushuru. LATRA wanaingiza zile fedha baada ya wiki mbili, hela za kujiandaa tunapata wapi? Huo mfumo hatuoni kama una manufaa zaidi ya kutuumiza tu," alisema.

Wakala mwingine, Godfrey Vincent, alisema licha ya huduma hiyo kuchelewesha mapato yao, pia bado mfumo wake haujatengemaa na kuwa kuna wakati mashine zinagoma kutoa risiti, hivyo kulazimika kurudi katika mfumo wa kawaida wa kutoa tiketi a mkono.

"Kuna wakati unatoa risiti kumi mashine inagoma kabisa kutoa tiketi, au inakwama kabisa mpaka uizime na kuiwasha, sasa inabidi turudi kwenye mfumo wa zamani, kwa kweli unakuwa ni usumbufu hasa kipindi hiki ambacho wasafiri ni wengi," alisema.

Meneja wa mabasi ya Tashrif, Hamisi Shemweta, alisema changamoto nyingine ni kuwa abiria anauwezo wa kukata tiketi kwa siku za mbali jambo ambalo linaleta shida ikiwa gari alilokatiwa tiketi likapata hitilafu, tofauti na kama mteja angekata tiketi siku moja au mbili kabla ya kusafiri.

Aidha, aliwasihi abiria kuingia ndani na kukata tiketi kwenye ofisi zao moja kwa moja ili kuepuka madeiwaka wanaowawahi wakiwa barabarani na kuwaongezea kiwango cha nauli kwa manufaa yao binafsi huku lawama ikienda kwa mawakala hao.

**LATRA YAFUNGUKA**

Meneja Usalama na Mazingira wa LATRA, Geoffrey Silanda, alisema wameshatoa leseni za muda kwa magari 22 kutoka Dar es Saalam kwenda mikoani na magari 42 nchi nzima na kufanya jumla ya leseni za muda 64.

Alisema mchakato huo ulianza Desemba 8, mwaka huu, kwa kuzingatia mabasi yaliyotimiza masharti, ikiwamo kuwa na uwezo wa kubeba abiria wasiopungua 40, kuunganishwa kwenye mfumo wa tiketi mtandao na kuwa na leseni ya LATRA.

Aidha, alisema wameshafanyia kazi changamoto nyingi zinazoleta usumbufu kwa abiria ikiwamo huduma ya tiketi mtandao ambayo sasa wamiliki wanatapata zao moja kwa moja mara baada ya malipo hayo yanapifanyika kupitia benki husika.

Pia alisema vilevile wanashirikiana na Mamlaka ya Reli Tanzania (TRL) ambayo imekubali kuongeza behewa ambayo yatapachikwa kwenye treni za kwenda mikoani, ili kuongeza nguvu na kupunguza adha ya usafiri wanayopitia abiria kipindi hicho.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Abdallah Mohamed, alisema walifanya kikao na madereva wa mabasi na kuwasisitiza wafuate sheria za usalama barabarani na kanuni za LATRA ili kuwaepushia abiria usumbufu hasa msimu huu wa sikukuu.

"Tumewaambia mwaka huu hatutaki kusikia kabisa abiria wakilalamikia changamoto zilizosababishwa na wamiliki au mawakala, kila dereva ahakikishe anazingatia sheria, kabla magari hayajaondoka wahakikishe yapo salama, na pia abiria wote wakae kwenye siti, hakuna kusimamisha abiria," alisema.

# Mama, watoto wadaiwa kumuua baba yao

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia mama na watoto wawili kwa madai ya kumuua baba yao baada ya kuwakodi watu kwa ujira ili kutekeleza mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilibroad Mutafungwa, alisema tukio hilo la mauaji lilipangwa na familia ya Mange Mwasha kwa kutekelezwa usiku wa manane nyumbani kwake, Kwimba mkoani Mwanza.

Alisema katika tukio hilo, mke wa marehemu, watoto wake wawili na watu wengine, waliokodiwa kwa Sh. 800,000 walitekeleza mauaji hayo.

Mutafungwa alisema siku ya tukio, watu wasiojulikana wakati huo, walivamia nyumbani kwa marehemu Mwasha kwa kuvunja mlango kisha kuingia ndani na kumkata shingo, hivyo kusababisha kifo chake.

Baada ya mauaji hayo yaliyotokea Desemba 1, mwaka huu, alisema polisi walianza msako na Desemba 5, walifanikiwa kukamatwa watuhumiwa hao.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni kutokana na ugomvi wa kifamilia kati ya baba na mtoto wake wa kiume ambaye alikuwa akituhumiwa kujihusisha na wizi.

Baba mzazi wa kijana huyo, ilidaiwa baada ya kubaini mtoto wake alikuwa mwizi, alimfukuza nyumbani kwake, kitendo ambacho hakikumfurahisha mama mzazi, hivyo kuamua kuwashawishi watoto wake kumuua baba yao.

Katika hatua nyingine, Mutafungwa alisema polisi mkoani Mwanza wanashikilia watu mbalimbali kwa tuhuma mbalimbali kutokana na operesheni inayoendelea mkoani hapo ijulikanayo 'Tokomeza Uhalifu'.

Mutafungwa (pichani) alisema watu hao walikamatwa kwa tuhuma mbalimbali zikiwamo wizi, uvuvi haramu, uuzaji wa dawa za kulevya, pombe haramu aina ya gongo, utoaji mimba, bangi na mirungi.

Kamanda Mutafungwa alisema katika operesheni hiyo ya mwezi mmoja, pia wamefanikiwa kunasa vitu mbalimbali vilivyoibwa mkoani Mwanza.

Alitaja vitu hivyo kuwa ni pamoja na televisheni, redio, pikipiki ambavyo kwa sasa viko katika vituo mbalimbali vya polisi kwa ajili ya utambuzi, hivyo akawataka wananchi mkoani hapa kufika vituo vya polisi wakiwa na vielelezo kwa ajili ya kutambua mali zao ambazo waliibiwa.



Pia alisema polisi wanamshikilia Mary Seni kwa tuhuma ya kutoa mimba ya miezi saba na kisha kutupa mtoto eneo la Kitangiri mkoani Mwanza.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, akimkabidhi baiskeli ya kutembelea Ayubu Makaburi kwa ajili ya mtoto wake mwenye ulemavu Yusuph Ayubu baada ya kuhutubia mkutano wa hadhara katika Kata ya Mtera Jimbo la Kibakwe Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machinga watoa msimamo wao kuhusu kauli ya TRA kulipa kodi matumizi EFD

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKISHO la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA), limesema ni muhimu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kutoza kodi machinga wote nchini badala ya Kariakoo pekee.

Hata hivyo, wamesema hawakushirikishwa katika mchakato wa kupewa mashine za kielektroniki (EFD), ambazo watatakiwa kulipia Sh. 580,000 kila moja.

Makamu Mwenyekiti wa SHIUMA Taifa, Steven Lusinde, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alisema mazingira ya kundi hilo kuhifadhi mashine hizo ni magumu na maisha yao ni ya kuhamahama.

"Tumeshasajiliwa zaidi ya machinga 5,000 wa eneo la Kariakoo, mwakani tutapewa mashine za EFD kwa ajili ya kuanza kulipa kodi," alisema.

Vile vile alisema hawana tatizo katika kulipa kodi, lakini kuwe na utaratibu shirikishi ambao utawalipisha kodi wote badala ya wachache wao.

Lusinde ambaye ni Mwenyekiti wa Machinga Kariakoo, aliiomba TRA kuondoa utaratibu wa kuwataka wafanyabiashara hao wadogo kuwa na mashine za EFD kwa kuwa ni gharama na hauendani na mitaji yao na utunzaji wake ni mgumu kutokana na mazingira wanaofanyia shughuli zao.

"Mashine ya EFD ni gharama, hatuna elimu namna ya kuitumia na hata mazingira ya kuitunza ni magumu kwa sababu shughuli zetu ni za kwenye jua na mvua, kwa hiyo ikiharibika inaongeza gharama nyingine ya kuitengeneza," alisema Lusinde.

Alipoulizwa wanahifadhi vipi simu zao alisema "Simu utaweka kwenye nailoni, mfukoni au kumuomba mtu akuhifadhie, lakini hii mashine huwezi kufanya hivyo."

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, wako tayari kulipa kodi, lakini wanaomba watengenezewe utaratibu mzuri ambao hautawaumiza.

"Sisi tuko tayari kulipa kodi na kuchangia kwenye taifa letu, lakini tunachokiomba TRA watengeneze sheria ambayo itaweka utaratibu wa kila Machinga kulipa kodi kwa uwiano sawa badala ya kuwabana wa Kariakoo pekee," alisema.

"Ni bora waseme kwamba kila mfanyabiashara mdogo alipe Sh.150,000 au Sh. 200,000 kwa mwaka kuliko kumkadiria kila mtu kivyake hiyo italeta shida."

"Machinga anayefanya biashara Kariakoo ana utofauti gani na yule anayefanya Mbagala, Mwenge, Tabata na maeneo mengine nchini. Kwa nini leo mashine ya EFD iende kwa aliye Kariakoo peke yake, ni suala ambalo tunajiuliza kwa nini TRA wasingekaa wakatengeneza mfumo mzuri, au tukashirikiana awali kutoa mawazo, tukatengeneza ka-sheria ambako katamgusa kila mfanyabiashara mdogo."

"Huwa tunafanya vikao na TRA, lakini katika hili suala la EFD hatujawahi kushirikishwa kutoa mawazo yetu. Ni lazima ingeleta tija zaidi."

"Leo kuna baadhi wameenda TRA kukadiriwa biashara zao na yanafika mpaka Sh. 600,000, Sh. 800,000, lakini anaambiwa anunue mashine Sh.580,000, akinunua hiyo mashine kwa gharama hiyo, mezani pake patabaki na nini, hiyo ni changamoto,"

"Lakini hata kama ukimpatia mashine ya EFD anaihifadhi wapi kwa sababu biashara yake iko juani na kwenye mvua, ataichaji wapi na ikipigwa na jua, ikinyeshewa na mvua ni lazima itaharibika na gharama za matengenezo zitatoka wapi."

Juzi TRA Kariakoo ilisema itaanza msako mkali kwa wafanyabiashara na wateja wanaonunua na kuuza bila kudai na kutoa risiti, huku wakiwataka machinga wote kufuata utaratibu wa kutumia mashine za EFD watakazopewa.

## Tanzania mwenyeji mkutano kimataifa chakula

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameridhia Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Jukwaa la Mtandao wa Chakula Afrika (AGRF), utakaowaleta pamoja viongozi, watu mashuhuri na wadau wapya 3,000.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, mkutano huo utafanyika mwakani kwa mara ya kwanza nchini na utakuwa na mafanikio chanya.

Mkutano kama huu ulifanyika Septemba 5 hadi 9, mwaka huu, nchini Rwanda na Tanzania iliwakilishwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. Uliwaleta pamoja viongozi mbalimbali kwa kaulimbiu ya kukua, kushamiri na kuzawadia, hatua imara za mifumo thabiti ya chakula.

Alisema uamuzi huo umetangazwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia, Hailemariam Dessalegn katika Jukwaa la Mtandao wa Chakula Afrika (AGRF) nchini Marekani, ambalo pia Rais Samia alihudhuria.

Rais Samia alisema anatarajia mkutano huo utaendeleza uimarishaji wa mifumo ya chakula na kilimo katika vipaumbele vya serikali, kupeana taarifa na kutumia teknolojia ya kisasa kwa ajili ya mifumo imara ya chakula.

Alisema wadau watakaohudhuria watajadili namna ya kuimarisha biashara miongoni mwa miji mbalimbali, ili kuchangia usalama wa chakula, ukuaji na uvumilivu.

"Lengo lingine ni kushawishi nchi zote juu ya ajira kwa vijana ambapo kila nchi barani Afrika itaweka wazi mikakati yake ya malengo ya ajira hizo na namna ya kufanikisha," alisema Zuhura na kuongeza:

"Katika kuimarisha shughuli za kilimo serikali imeongeza bajeti yake karibu mara nne katika sekta hiyo kutoka Dola za Kimarekani milioni 126.7 kwa mwaka 2021/2022 hadi dola milioni 411.2 mwaka 2022/2023."

Rais Samia aliwasili nchini Marekani jana kuhudhuria mkutano wa siku tatu wa Wakuu wa Nchi wa Afrika na Marekani utakaohusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo pamoja na mikutano mingine ya kimkakati.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA MAFUNZO**

**KUMB : ETJ-BB-HS-PL-GEN-GE-0017**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Kampuni zenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Utoajii wa Mafunzo.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta yasiyosafishwa yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni, eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

Aina zifuatazo za mafunzo zitahitajika kwa Mradi wa Gati.

- Mafunzo kuongeza ujuzi Kazini
- Mafunzo ya Ufundi
- Warsha au mafunzo ya ustadi
- Mafunzo kutoka Asasi/ Mashirika ya kitaaluma

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Mwalimu aliyehitimu na kuthibitishwa ndani/ kimataifa;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kutekeleza kandarasi husika.
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika utekelezaji wa huduma sawa za mafunzo yanayohitajika,
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya Afya, mazingira na Usalama sehemu ya kazi, pamoja na vyeti vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti sawa
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **28 Desemba 2022 Saa 12 jioni Saa za Tanzania.**

Makampuni yatakayokidhi mahitaji yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

17194502

# Mnyukano wa kisheria waibuka mawakili wa Sabaya na serikali



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, jana akizungumza na mawakili wake Mosses Mahuna (katikati) na Silvester Kahunduka, wakati akisubiri kusikilizwa kwa rufani katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha. **PICHA: ALLAN ISACK**

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MNYUKANO wa kisheria uliibuka jana baina ya mawakili wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wa serikali kuhusu rufani iliyowasilishwa na Jamhuri dhidi ya kupinga uamuzi uliotolewa wa kumwachilia yeye na wenzake.

Katika mnyukano huo, mawakili wa Sabaya na wenzake watano ambao ni wajibu rufani katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, wamewasilisha mahakamani sababu mbili za kupinga kusikilizwa kwa rufani hiyo.

Wakati upande wa wajibu rufani ukiwasilisha hoja hizo, mawakili wa serikali kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), wamepinga kuwa hoja au sababu zilizotolewa hazina mashiko hivyo mahakama izitupilie mbali na kesi iendelee.

Katika kesi hiyo, wajibu rufani ni Ole Sabaya, Sylvester Nyengu, Enock Togolani, John Odemba, Jackson Macha, na Nathan Msuya.

Akitoa sababu ya kwanza kupinga kusikilizwa rufani hiyo namba 155 mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Salma Maghimbi, Wakili Mosses Mahuna kwa wajibu maombi Sabaya na Nyegu, alidai kuwa rufani hiyo haikuwa sawa kisheria ndiyo maana walitoa notisi ya kupinga kwa DPP baada ya mteja wake kufikishwa mahakamani.

Mahuna alidai kuwa rufani hiyo inakinzana na kifungu namba 379 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2022. Pia alidai kwamba kifungu namba 379 (B) kinaeleza kuwa rufani inatakiwa kufunguliwa ndani ya siku 45 tangu mahakama ilipotoa uamuzi au washtakiwa kuachiwa huru.

Alidai kuwa uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, ulitolewa Juni 10, 2022 na rufani iliwasilishwa mahakamani Oktoba 28, 2022 ikiwa ni miezi minne baadaye.

Wakili huyo alidai kwamba masharti ya kifungu cha 379 (A) yameweka wazi kwamba DPP alipaswa kutoa notisi ya kukata rufani ndani ya siku 30 na notisi hiyo ilitolewa June 24, 2022 ikiwa tayari zimeshapita siku 40.

Kwa mujibu wa nyaraka za DPP, alidai kuwa zinaonyesha kuwa alipokea nakala ya rufani Septemba 14, 2022 lakini rekodi za mahakama zinaonyesha walipatiwa nakala Septemba 13, 2022.

"Mheshimiwa Jaji napenda kusema rufani hii iko nje ya muda kwa siku 14 au 15 na itategemea kama itaanza kuhesaba kuanzia Septemba 13 au 14 mwaka 2022,"alidai Mahuna.

"Madam Jaji notisi ya kukata rufani inakinzana na rufani iliyowasilishwa mahakamani hapa kwa kuwa notisi ya rufani inaonyesha ni kwa watu saba ila rufani yenyewe inaonyesha ni watu sita. Kwa hiyo tunaona hakuna haja ya kuwapo kwa rufani hii, japokuwa kwa mujibu wa sheria namba 389 kifungu kidogo cha kwanza cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, DPP anaweza kumtoa mtu kwenye rufani kwa kutoa sababu kwenye notisi ya kukata rufani. Kutokana na sababu hizi, mbili tunaomba mahakama yako tukufu kutupilia mbali rufaa (rufani) hii, "alidai.

Akijibu sababu hizo, Wakili wa Serikali Mwandamizi Patrick Mwita, alidai kwamba ni kweli hukumu ilitolewa Juni 10,2022 na waliwasilisha kusudio la kukata rufani Juni 24,2022. Pia alidai kuwa hakuna ubishi kwa mleta rufani alitoa sababu za kukata rufani Oktoba 28, 2022.

"Tofauti iliyoko ni ndogo sana ni tafsiri ya kisheria tu. Kwa kuwa wanadai tangu kutolewa kwa hukumu, zilianza siku kuhesabika na zilisimama tangu tulipopeleka nia ya kukata rufani Juni 10, 2022 ndiyo sababu wanadai kuwa tuko nje ya muda," alidai Mwita.

Hata hivyo, Wakili Mwita alidai kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 379, kifungu kidogo 1(A) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jina, vikisomwa kwa pamoja hoja zao si sahihi.

"Tunasema si sahihi kwa kuwa Kifungu cha 3791 (B) kimeelekeza kuwa huwezi kukata rufani bila ya kutoa sababu ya kukata rufani na iko wazi kwa kuwasilisha sababu za kukata rufani ndani ya siku 45 baada ya kupokea nakala ya hukumu," alidai.

Alidai kwamba suala la ukomo wa muda limefafanuliwa katika Sheria ya Ukomo wa Muda Sura ya 89 kifungu cha 19(2), hivyo tafsiri ya Mahuna kudai kwamba inaanza kuhesabika tu baada ya hukumu si sahihi na huenda amechanganya mambo.

"Sababu yao ya kwanza haina msingi, hivyo tunaomba mahakama izitupilie mbali kwa kuwa muda unaaza kuhesabika pale tulipopata nakala ya hukumu. Hoja yao ya pili, kuhusu notisi ya kukata rufani ilikuwa Oktoba 28, 2022 ikionyesha kwamba itakuwa kwa watu sita lakini rufani yenyewe ni kwa watu saba, Wakili Mahuna ameipotosha Mahakama.

"Watson (Mwahomange) kwenye notisi ya rufani ameorodheshwa ila kwenye rufani hayuko, kwa kuwa nia ya kukata rufani ndio inaanzisha rufani lakini si rufani. Ukishapata nakala ya hukumu na kuangalia vitu ambavyo havikuwa sawa ndipo unapeleka notisi ya kukata rufani. Baada ya kuipitia na kuisoma hukumu tumeona hakuna haja ya kumkatia rufani.

Alidai kifungu cha 386 kitatumika pale rufani inapokuwa mbele ya mahakama, hivyo wamefuata utaratibu wa kisheria na hawaoni kama haki imekiukwa.

"Pia DPP anayo mamlaka kisheria kuchagua ni nani wa kumkatia rufani na tulivyoangalia na kuisoma nakala ya hukumu, hatupangiwi ni yupi wa kumkatia na kutokumkatia kwa kuwa hatupangiwi na mtu yeyote," alidai.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdalah Chavula, alidai kwamba sababu zilizotolewa na waleta rufani zinaungwa mkono na kesi ambayo wameiwasilisha mahakamani ambayo imeshawahi kutolewa uamuzi na Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Jaji Maghimbi aliahirisha kesi hiyo hadi leo atakapotoa uamuzi mdogo kama rufani hiyo itasikilizwa au la.

# Mamlaka yatoa msimamo kuruhusu matumizi bangi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema haiwezi na haina mamlaka ya kuruhusu matumizi ya bangi nchini kwa kuwa jambo hilo ni mtambuka ambalo linatakiwa kushirikisha wadau wengi kufikia uamuzi.

Aidha, mamlaka hiyo imeonya watu kutotumia kigezo cha kwamba Rais Samia Suluhu Hassan amefungua nchi kwa kuanza kujihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alisema hayo juzi wakati akihojiwa katika kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na luninga ya ITV kuanzia saa 3:00 usiku kila Jumatatu.

"Suala la kuruhusu bangi ni jambo ambalo ni mtambuka linatakiwa kuhusisha wadau wengi. Sisi kama mamlaka tunaweza kuwa wadau wa mwisho kabisa sababu sisi kazi yetu ni kudhibiti na siku zote huwezi kuruhusu matumizi ya bangi kabla hujafanya utafiti," alisema.

Kusaya ambaye alikuwa akijibu swali aliloulizwa kwamba kulikuwa na mjadala bungeni wa kuruhusu matumizi ya bangi, alisema nchi zilizoruhusu bangi inalimwa katika sehemu tofauti na si kila mtu anaruhusiwa kulima.

"Bangi zinazolimwa kwa ajili ya utafiti zinalimwa sehemu maalum na unakuta kuna uzio hadi kamera zinafungwa kwa hiyo sio kila mtu ataruhusiwa yale sio mahindi," alisema.

Kuhusu watu kudai Rais amefungua nchi kwa hiyo wanaweza kufanya lolote, alisema Rais amefungua nchi ina maana ni katika mambo yanayoruhusiwa na kukubalika kisheria.

"Suala la bangi haliwezi kuwa sehemu ya kufungua nchi, haramu itaendelea kuwa haramu mpaka pale ambapo kutakapohalalishwa na mamlaka zinazohusika," alisema.

Kusaya akizungumza suala la mirungi kuruhusiwa matumizi nchi jirani huku Tanzania ikipigwa marufuku, alisema kila nchi ina sheria zake na kuna sheria ambazo ni za Umoja wa Mataifa ambazo kila nchi inatakiwa kuzifuata lakini kuna sheria ambazo zinakuwa zinatawaliwa nchi kwa nchi.

Alisema pamoja na nchi jirani kuruhusu mirungi lakini wanaofanya biashara hiyo waheshimu mipaka wanapokutana na mpaka wa Tanzania wafahamu kwamba mirungi hairuhusiwi nchini mwetu.

"Sisi haturuhusu mirungi sababu wataalam wetu wamejiridhisha kwamba mirungi ni dawa za kulevya ambazo madhara yake sawa na dawa nyingine kwa hiyo sisi hatuwezi tukaiga, tukiona kitu fulani kina faida wataalam wetu ndio watatushauri kitu gani tukifanye," alisema.

**HABARI KITAIFA**

## Ubakaji, ulawiti watoto sasa tishio

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MATUKIO ya ubakaji wa watoto yamekuwa tishio nchini baada ya kubainika kuwa kwa kipindi cha miezi tisa, yameripotiwa 4,797 huku ulawiti kwa watoto wa kiume ukishika kasi.

Kutokana na tishio hilo, wadau wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), wametoa mwelekeo wa mambo saba yanayopaswa kufanyika ili kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake.

Mratibu wa MTAKUWWA Taifa, John Mwanga, aliyasema hayo jana jijini hapa katika kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mpango huo kwa awamu ya kwanza 2017/18 hadi 2021/22, kilichowezeshwa na mashirika ya WiLDAF, ICS na WFT.

Alisema katika takwimu za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani zinazotolewa na Jeshi la Polisi nchini kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, 2022 zimebainisha matukio ya ukatili yalivyoongoza kwa idadi kwa watoto.

Mwanga alisema mbali na ubakaji matukio ya shambulio la kudhuru mwili 3,322 ambayo kwa watoto wa kike ni 2,116 huku wa kiume ni 1,206.

"Matukio ya ulawiti yalikuwa 1,044 ambayo kwa watoto wa kike ni 166 huku wa kiume yakiwa 878. Kuwapa mimba wanafunzi ni 1,115 lugha ya matusi ni 1,858 kati ya hayo watoto wa kike ni 1,082 huku wa kiume ni 776," alisema.

Mratibu huyo alifafanua kuwa matukio ya shambulio ni 3,100 kati ya hayo wa kike ni 1,966 huku wa kiume ni 1,134.

"Matukio ya kujeruhi watoto ni 2,141 ambayo kati yake wa kike waliojeruhiwa ni 1,048 huku wa kiume ni 1,093," alisema.

Pia alibainisha kuwa kutokana na hali hiyo kunapaswa kuratibiwa maandalizi ya kampeni ya kitaifa ya kulinda maadili na kupambana na vitendo hivyo.

"Tuimarishe utoaji elimu ya malezi chanya ya watoto ili kuzuia ukatili, kuratibu uanzishwaji wa madawati ngazi mbalimbali kuanzia shuleni hadi vyuoni, na kuanzisha mabaraza ya watoto ngazi zote," alisema,

Kadhalika, alisema kukamilisha uundwaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zilizobaki 2,564 na kuzijengea uwezo wa kutimiza majukumu yake.

"Kusimamia utekelezaji wa sheria ambapo kwenye hili ni kuzifanyia mapitio sheria zenye shida katika kushughulikia masuala ya ukatili dhidi ya watoto,"alisema.

Akifungua kikao hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainabu Chaula, alisema: "Kuna mafanikio yamepatikana kwenye utekelezaji wa mpango lakini ni muhimu kujiuliza kwa nini vitendo vya ukatili bado vinaendelea kutokea licha ya jitihada mbalimbali za serikali na wadau."

# Wapinga kumhukumu anayedaiwa rushwa ngono

**Na Mary Geofrey**

WANAMTANDAO wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania, wamepinga kitendo cha kuingiza kipengele 25(ii) cha kumhukumu anayedaiwa rushwa ya ngono, katika sheria pendekezwa ya Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Kuwapo kwa kifungu hicho kunatajwa kuwa chanzo cha kuwalinda wenye mamlaka kuwanyanyasa, kuwakandamiza na kusababisha vifo vya watoto, wanawake na vijana wa kiume nchini.

Msimamo wa Wanamtandao huo unaojumuisha mashirika zaidi ya 150, ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Wanawake (Women Fund), Prof. Ruth Meena, katika kongamano la maadhimisho ya Kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia iliyomalizika Desemba 10, 2022 ambayo ni siku ya Haki za Binadamu Duniani.

"Tumeamua kwa makusudi kuendeleza kampeni yetu ya kitaifa yenye kaulimbiu, 'Vunja Ukimya; Rushwa ya Ngono Inadhalilisha na Inaua'. Tumeendelea kujenga uelewa wa rushwa ya ngono na madhara yake pamoja na kuleta mapendekezo yetu dhidi ya sheria pendekezwa ya TAKUKURU katika kipengele cha 25(ii)."

"Sisi wanamtandao tunaopinga rushwa ya ngono kwa pamoja tunaviomba vyombo vyote vinavyohusika na mabadiliko ya sheria hii ikiwa ni pamoja na ofisi ya Mwanasheria, Bunge letu na Rais Samia Suluhu Hassan, wasikubali pendekezo la kubadilisha hiki kifungu pendekezwa cha sheria hii."

Alisema sambamba na suala la rushwa ya ngono ni uwapo wa Sheria ya Ndoa inayoruhusu ndoa za utotoni kwa wasichana.

Prof. Meena, alisema wanawake walishangilia walipopokea uamuzi wa Mahakama Kuu kukiri kwamba kifungu kinachoruhusu mtoto wa kike aolewe akiwa na umri mdogo kwa ridhaa ya mzazi au mlezi, kinakiuka haki za mtoto kikatiba na zile zilizoainishwa katika sheria ya mtoto.

"Wasiwasi wetu sisi watetezi wa haki za wanawake na watoto, tunatambua uhuru wa mihimili yote ya utawala, tukiamini kwamba uamuzi wa mahakama kuu kuhusu sheria ni wa mwisho na hautenguliwi na mhimili mwingine wowote," alisema.

"Katika hali inayotupa utata wa uhuru wa hii mihimili ni pale Bunge letu linairudisha sheria hii ikajadiliwe na umma wa Watanzania baada ya uamuzi wa Mahakama Kuu kuibatilisha.

"Kwetu sisi tunaona ni kukinzana kwa mihimili miwili katika kulinda haki za msingi za mtoto wa kike na vilevile ni mbinu ya kumcheleweshea mtoto wa kike haki zake za msingi," alisisitiza.

Alisema wanamtandao wanalitaka Bunge kuheshimu uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu kuleta mabadiliko ya sheria hiyo ili kumlinda mtoto wa kike kupata haki zake za msingi.

Pia, alitoa wito kwa watendaji wa serikali kuendelea kuboresha sheria zinazowalinda Watanzania wote bila kujali jinsia.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph (kulia mbele), akimwongoza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa pili kulia), walipotembelea tangi la kuhifadhia maji eneo la uzalishaji maji kwenye chanzo cha Mzakwe jijini Dodoma jana. Wengine ni wajumbe wa Bonde la Maji Wami Ruvu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Royal Tour yazidi kuvutia watalii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha Januari hadi Oktoba, mwaka huu, Tanzania imepokea watalii 1,175,697 kulinganisha na watalii 716,741 walioingia katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Daniel Masolwa, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ongezeko la watalii nchini katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, mwaka huu.

"Idadi hiyo ni ongezeko la watalii 458,956 sawa na ongezeko la asilimia 64," alisema Masolwa

Pia alisema idadi ya watalii walioingia katika kipindi cha Oktoba, mwaka huu, ni 141,517 kutoka 92,345 iliyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka jana.

"Hii ni sawa na ongezeko la watalii 49,172 sawa na asilimia 53. Ongezeko hili la watalii limechangiwa na jitihada za serikali kukuza sekta hiyo ndani na nje ya nchi kupitia filamu ya The Royal Tour,"alisema Masolwa.

Alizitaja nchi ambazo zimeongoza kwa kuingiza watalii wengi nchini kwa bara la Afrika na nje kuwa ni Kenya ambayo imeongoza kwa kuingiza watalii 15,701 ikifuatiwa na Burundi 8,929, Afrika Kusini 3,802, Rwanda 3,715 na Uganda 3,229.

"Nje ya bara la Afrika nchi iliyoongoza kuleta watalii ni Ufaransa watalii 12,543 ikifuatiwa na Marekani 9,097, Ujerumani 8,874, Uingereza 6,514 na Italia 4,557," alisema Masolwa.

Kuhusu matumizi ya saruji kwa kipindi cha Januari hadi Septemba, mwaka huu, alisema yameongezeka kufikia tani 5,602,645 kutoka tani 4,891,726 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 14.5.

Alisema, matumizi ya saruji ni kiashiria kimojawapo cha ukuaji wa uchumi na katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka Januari hadi Machi 2022 matumizi ya saruji yalikuwa ni tani 1,906,095.

Pia alisema katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka Aprili hadi Juni matumizi yalikuwa tani 1,683,070 na robo ya tatu ya mwaka Julai hadi Septemba uzalishaji wa bidhaa hiyo ulipanda hadi tani 2,013,480.

Kuhusu ongezeko la matumizi ya huduma za mawasiliano nchini, alisema dakika bilioni 33.4 katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu, zimetumika kutoka dakika bilioni 25.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Usafiri sikukuu usiwe mtaji kutajirisha wenye mabasi*

**INAPOKARIBIA** kipindi cha mwisho wa mwaka na Sikukuu ya Krismasi, wakati wanafunzi na wafanyakazi wengi huchukua likizo kwa ajili ya kusafiri kwenda mikoani, usafiri huwa wa shida na nauli kupanda bei.

Kipindi hiki watu wengi huhangaika kupata usafiri na wanaofanyakazi kwenye mabasi yanayokwenda mikoani hugeuka miungu watu kwa kuwaringia wasafiri na kuwapangia bei wanazotaka wao.

Hali hii hujitokeza kila inapofika mwezi Desemba, kipindi ambacho watu wengi hupenda kusafiri kwenda mikoani kusalimia ndugu na jamaa.

Wenye mabasi hayo huanza kukata tiketi za wasafiri mapema na inapofikia kipindi cha wiki ya mwisho ya Sikukuu ya Krismasi, watu wengi hukosa usafiri kwa kuambiwa yameshajaa mapema.

Baadhi ya wamiliki na wahudumu wa mabasi hayo yaendayo mikoani hutumia kipindi hiki kujinufaisha kwa kuwapandishia abiria nauli wakijua kwa vyovyote watanunua tiketi kwa sababu hawana njia nyingine.

Wakati kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani kilipokuwa Ubungo, jijini Dar es Salaam, abiria katika kipindi cha sikukuu walikuwa wakisota kituoni hapo kuanzia alfajiri hadi jioni bila kupata usafiri.

Mazingira ya kituo hicho, sehemu kubwa ilikuwa wazi na kipindi cha mwezi Desemba huwa cha mvua na kukumbana na adha ya kunyeshewa kwa kusubiri usafiri.

Adha wanayopata kushinda pia kwenye jua huku wakiwa na watoto ni kubwa na wengine wanakuwa wameshakata tiketi na kuahidiwa basi litafika wakati wowote ili waweze kusafiri, lakini muda unapofika wa kusafiri huambiwa limepata tatizo hivyo waendelee kusubiri.

Kwa kukosa uwezo wa kukata tiketi kwenye basi lingine, huishia kusubiri na wakati mwingine mpaka jioni huku watoto wakilia njaa kwa kukaa kituoni muda mrefu.

Kutokana na adha hiyo wanayopata wasafiri, serikali iliamua kuingilia kati kwa kuiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), kuandaa utaratibu wa kuruhusu mabasi mengine yanayofanya safari za mjini kuruhusiwa kwenda mikoani katika kipindi hicho ili kutoa unafuu kwa wasafiri.

Latra iliamua kutoa vibali kwa mabasi kama Coaster ambayo yanakidhi vigezo vya kusafiri mikoani yachukue abiria kuwapeleka mikoani ili kuwaondolea adha hiyo.

Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, bado kuna suala la tiketi mtandao ambalo limekuwa tatizo kubwa kwa wanaotoa huduma hiyo ya usafiri.


Baadhi yao huwaambia abiria kuwa hawawezi kuwapatia tiketi mtandao mpaka mmliki wa basi aamue nauli ya siku hiyo. Hili ni tatizo na inaonesha jinsi gani wamiliki hao wanavyokwenda kinyume na agizo la serikali.

Abiria hupewa sharti kuwa wakitaka kukata tiketi ya basi wakubali kupewa ya karatasi na siku ya safari ndiyo wachukue tiketi mtandao ambayo huwa na bei elekezi iliyopangwa na serikali. Kwenye tiketi ya karatasi mmiliki wa basi ndiye anayepanga bei ya usafiri kwa siku hiyo na kutokana na shida ya usafiri, abiria inabidi akubaliane na bei hiyo ili aweze kusafiri.

Mabasi hayo yameruhusiwa katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, yafanyekazi usiku na mchana ili kuondoa kero hii wanayopata abiria kwa kusumbuliwa na wenye mabasi. Baadhi ya wamiliki husubiri kipindi hiki ambacho hukiita cha neema kujinufaisha kwa kujipangia bei wanazotaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Golden Kisapile, TUDARCo

# *Tuzingatie haya ajali zipungue*

**KUNA** madai kuwa mwishoni mwa mwaka kuna visababishi vingi vinavyoweza kuleta vifo, hata bila kutegemewa. Tena ipo imani kuwa ni kipindi cha ajali zinazotokea kitatanishi.

Kama kuna ukweli kwanini tusiwe makini barabarani na maeneo yanayoweza kukatisha maisha?.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria watu takribani milioni 1.35 hufariki kila mwaka kutokana na ajali barabarani zinazotokea zaidi kwenye nchi za uchumi mdogo.

Aidha, hugharimu nchi hizo karibu asilimia tatu ya mapato yake na asilimia 93 ya ajali hizo hutokea mataifa maskini ikiwamo Tanzania.

Ajali huua, kuleta ulemavu, kuharibu magari, miundobinu na madaraja kwa ujumla huambatana na hasara nyingi na maafa lakini cha kutia moyo ni kwamba ajali za barabarani zinaweza kupungua na hata kuzuilika.

Kikubwa ili kuzizuia hatua ya kwanza ni kuzingatia sheria za barabarani kama vile madereva ambao wanaendesha vyombo mbalimbali, watembeao na watumiaji wengine ambao ni kama raia wote.

Kwa mfano derava anaendesha gari huku anaongea na simu au anachati (kutongoa), anafungulia mziki mkubwa. Kwenye bodaboda madereva wanavunja sheria kwa kupenya bila kujali taa wala trafiki anayeongoza magari.

Lakini pia, wapo wafanyabiashara wanajitumbukiza na kupanga bidhaa barabarani wapendavyo. Si hivyo tu, pia wapo wanaoziona barabara kama sehemu ya mchezo wakiegesha magari kila wanapojisikia, kutumia magari mabovu yakiwamo yasiyo na taa, vioo wala breki.

Ni vyema kukumbusha madereva kuepuka vilevi kama pombe, sigara, dawa za kulevya na bangi kwa sababu pia ulevi ni chanzo cha ajali.

Si madereva pekee hata watumiaji wengine wanatakiwa kuepuka mambo hayo kwa sababu anaweza kuyumba na kusababisha ajali hata kama si dereva.

Kutumia simu barabarani ni hatari kwa sababu kuna punguza umakini na kusababisha ajali , ni vyema kusimama pembeni na kuongea au kuandika SMS, baada ya hapo kurudi kwenye usukani. Jingine muhimu ni vyema kuepuka kutumia foni masikioni na ni muhimu kupiga vita mambo hayo ili ajali zipunguzwe.

Wamiliki wa vyombo vya usafiri sambamba na madereva wanatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vyao vya usafiri vinapelekwa gereji kwa ajili ya matengenezo na uchunguzi angalau kwa kipindi maalumu kukabiliana na tatizo lolote kwenye injini na mfumo mzima wa chombo.

Ajali zitapunguzwa kwa kuheshimu vivuko vya watembea, taa na alama zinazotambulisha na kutoa tahadhari mbalimbali.

Hizo ni pamoja na alama za kutambulisha, mteremko au kona kali, madaraja, wenye mahitaji maalumu na wanaotembea.

Mamlaka zikiwamo Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS) na ule wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Mamlaka za Usimamizi wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuhakikisha miundombinu mibovu inarekebishwa na barabara zinakuwa imara ili kupunguza ajali mijini na vijijini.

Kuachana na kuendesha kwa mwendo kasi au spidi kubwa ni balaa barabarani yote yakichangia ajali , hivyo kuepuka kasi kubwa ni kupunguza ajali za barabarani.

Abiria na madereva wa pikipiki na bajaji wasijisahau wakumbuke wanatakiwa kuvaa kofia ngumu kwa sababu usalama wa mtu anayeendesha pikipiki unategemea kwa kiasi kikubwa uvaaji wa kofia ngumu kumlinda.

Dereva na abiria wanakingwa na upepo mkali, jua na ajali iwapo ataangukia kichwa ili kuepusha kifo au majeraha makubwa, hili nalo likizingatiwa ajali za barabarani zinaweza kupungua.

Kuvaa mikanda ni jambo muhimu si madereva pekee hata abiria hasa wa masafa yakiwamo magari ya mikoani.

Madereva wa vyombo vya moto wanatakiwa kuepuka kubeba mzigo kupita kiasi kwa sababu ukizidi huyumbisha chombo mfano, bodaboda kufunga magunia mengi ya mkaa yanayoziba vioo, kutanuka na kusumbua wengine barabarani husababisha ajali, hivyo wakizingatia hayo ajali zinaweza kupunguzwa.

# Mkuu wa mkoa ataka mkakati kukabili ukatili kijinsia Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amesema hali ya vitendo vya ukatili mkoani humo ni mbaya na kuitaka jamii kuwajibika kukomesha.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, katika kilele cha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili na wiki ya watoa msaada wa kisheria, alisema ni lazima hatua madhubuti zichukuliwe.

Aidha, alisema kwa kipindi cha miezi sita matukio 442 yaliripotiwa kwa Jeshi la Polisi.

Aliyataja matukio hayo na kesi kwenye mabano kuwa ni kubaka (24), shambulio la aibu (45), mimba kwa wanafunzi (49), shambulio la kudhuru mwili (86) na kutumia lugha za matusi (42).

"Katika jamii zetu ukatili umeshika kasi kubwa sana katika kipindi hiki, madhara ambayo yanasababishwa na vitendo vya ukatili ni kama vile kupoteza maisha, ulemavu wa kudumu, msongo wa mawazo, umasikini mkubwa unaotokana na kushindwa kuwajibika na kuongezeka kwa watoto wa mitaani," alisema RC Thomas.

Akizungumzia wiki ya watoa msaada wa kisheria katika Mkoa wa Ruvuma, alitaja moja ya kazi za watoa huduma hiyo kuwa ni kusaidia mtu anapokutwa na hatari ya kufanyiwa ukatili na uonevu mwingine.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Jeshi la Polisi nchini, kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, mikoa inayoongoza kwa ukatili ni Arusha, Tanga, Shinyanga, Mwanza na mkoa wa kipolisi wa Ilala, Dar es Salaam.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Ruvuma, Xsaveria Mlimira, alizitaja aina tatu za ukatili kuwa ni wa kimwili ikiwamo vipigo na kujeruhiwa.

Nyingine kuwa ni ukatili wa kingono ukiwamo ubakaji na ulawiti, wakisaikolojia ambao ni matusi na kejeli, ukatili wa kiuchumi ni kutelekeza familia na wa unyonyaji ni wa kutumikisha kwa kulipa ujira mdogo.

Mshauri mkuu wa masuala ya kijinsia na Mwakilishi wa Mradi wa Afya Yangu mkoani humo, John Toto, alisema katika juhudi za kupambana na ukatili wa kijinsia mradi huo kwa kushirikiana na ofisi ya Mganga Mkuu wameendesha mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma za afya 88 waliopata mafunzo ya kusaidia wahanga wa ukatili wa kijinsia.

**Kuanzia Januari hadi Desemba 2021, mikoa inayoongoza kwa ukatili ni Arusha, Tanga, Shinyanga, Mwanza na mkoa wa kipolisi wa Ilala, Dar es Salaam.**



Inspekta Msaidizi wa Jeshi la Polisi, (A/INSP) Allen Chittunda (kushoto), kutoka Idara ya Elimu Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Kilimanjaro akitoa elimu ya matumizi sahihi ya barabara kwa waumini wa dini ya kiislamu katika Msikiti wa Riadha, Manispaa ya Moshi juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# TGNP yataka ushirikishwaji wadau kuhusu mabadiliko ya Sheria ya TAKUKURU

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gema Akilimali, amesema mpango wa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa bila kuwashirikisha wanaharakati sio sawa.

Aidha, amesema TGNP imefuatilia kwenye ofisi mbalimbali za serikali kujua nani anaandaa mabadiliko hayo kinachoendelea ili itoe maoni yake, lakini hawajapata taarifa, kuna jitihada za kufanya marekebisho ya kutaka kumwondoa mwanamke kama mwathirika wa rushwa ya ngono.

"Kama kuna wachache wanashawishi ngono kwa wanaume tupewe jukumu la kuwaaibisha na kuwarekebisha na sio kuwaweka wanawake kwenye kundi la watuhumiwa wa kutenda kosa, wakati uhalisia rushwa ya ngono hutendwa na wanaume," alisema.

Alisema kuruhusu mabadiliko hayo ni kurudisha nyuma jitihada za muda mrefu za wanaharakati kupinga rushwa ya ngono ambayo imekuwa kikwazo kikubwa kwa ustawi wa wasichana na wanawake, kwa kuwa wenye sifa huachwa kwasababu kuna watu fulani wanataka rushwa hiyo hasa kwenye uongozi, ajira na huduma mbalimbali.

Mwenyekiti huyo aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa kilele cha siku 16 za kupinga ukatili, kwa kuwa na mjadala wa pamoja baina ya wanachama wa vituo vya taarifa na maarifa vya TGNP vya Dar es Salaam na Morogoro.

Alisema matukio ya ukatili yamekithiri na yanaanzia tangu nyumbani, lakini kuna jitihada za kumaliza kifamilia jambo ambalo linapaswa kukemewa, huku akiwataka wazazi kutokubali kuficha ili wayamalize wenyewe huku aliyetendewa kaathirika kisaikolojia.

Mmoja wa watoa mada, aliiomba serikali kuongeza adhabu kwa wanaobaka au kulawiti inapothibitishwa wahasiwe kutokana na kwamba zilizopo hazitoshelezi ndio maana matukio yanaendelea.

"Kama hilo linaonekana kubwa sana au halistahili basi tuwe na utaratibu wa kuwaaibisha kwenye mitaa yetu wajulikane wazi kwa matendo yao mabaya. Pia muhimu Sheria ya Ndoa ikarekebishwa ili mtoto aolewe akishafikisha miaka 18," alisema.

Naye Janeth John alisema kazi anayofanya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima ni kubwa inapaswa kuungwa mkono, na kwa muda mrefu kulikuwa na malalamiko kwamba viongozi hawafanyi hili na lile sasa amepatikana anayefanyakazi kwa moyo wote.

Aliwataka wazazi kufuatilia mienendo ya watoto pamoja na kuwa karibu nao ili waeleze changamoto wanazopitia na kwamba ni muhimu kuangalia kwa jicho la pekee maisha ya wanafunzi wa bweni kwa kuwa ndiko masuala ya ushoga na kusagana huanzia.

Naye Agness Lukanga alisema shuleni na nyumbani ni kitovu cha ukatili kutokana na wazazi/ walezi kutosimama kwenye nafasi zao bila kujua kwamba kinachotokea shuleni ni matokea ya kilichofanyika nyumbani.

"Ulinzi ni muhimu tangu nyumbani ili mtoto aonekane bora, likitokea jambo baya kwenye familia fulani siku hizi tunasemana badala ya kusaidia kurekebisha. Ukeketaji, vipigo, rushwa ya ngono vinafanyika nyumbani na tuko kimya," alisema na kuongeza:

"Tuhakikishe nyumbani ni mahali salama kwa yeyote, tuache kuwafundisha watoto kutoa na kupokea rushwa tangu nyumbani, kwamba ukifanya hiki nitakupa hiki inakwenda hadi shuleni atamwambia mwenzake nifanyie kitu fulani ili nikupe hiki,"alifafanua.

## KABWELA



HABARI KITAIFA

# Machinjio mpya kuchochea ukuaji uchumi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MACHINJIO ya kisasa ya mifugo ya Nguru Hills Ranch Ltd yaliyoko wilayani Mvomero, yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku, yameanza rasmi huku yakitarajiwa kuchochea ukuaji wa uchumi, ajira na kupunguza migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

Mradi huo wa kisasa unamilikiwa kwa ubia ya wanahisa watatu ambao ni Eclipse Investment LLC kutoka Oman yenye hisa asilimia 46, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma ( PSSSF) asilimia 39 na Kampuni ya Busara Investment (LLP) yenye hisa asilimia 15.

Akitoa taarifa kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema mradi huo umegharimu dola za Kimarekani milioni 15 sawa na Sh. bilioni 29 ambazo zimetumika kununua mashine na mitambo, kukarabati jengo la kiwanda, ujenzi wa mabwawa ya kutibu maji taka, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwandani na gharama za uendeshaji.

Kashimba alisema katika uwekezaji huo, wanahisa wamewekeza dola milioni 10 kati hizo PSSSF imewekeza dola milioni 3.9, hivyo kufanya kuwa na asilimia 39 ya hisa huku dola milioni tano ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Azania.

Alisema mradi huo una miundombinu muhimu ikiwamo eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta 2,328, eneo lenye uwezo wa kuchukua ng'ombe 10,000 na mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja na miundombinu ya maji inayohusisha visima vitano yenye uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa saa.

Soko la nyama inayozalishwa, alisema itauzwa nje ya nchi kwa asilimia 80 hususani nchi za Mashariki ya Kati ikiwamo Oman ambao ni miongoni mwa wanahisa na asilimia 20 kwa ajili ya soko la ndani.

Alisema machinjio hayo yametoa ajira ya moja kwa moja 350 na ajira zingine zaidi ya 2,000 zinazotokana na mnyororo wa thamani, soko la uhakika, kuongeza kipato kwa wafugaji ambao wanauza mifugo yao pamoja na kupunguza migogoro ya wafugaji na wakulima.

Kwa mujibu wa Kashimba, mradi huo ulianza mwaka 2018 lakini ugonjwa wa COVID -19 uliponza, ulisababisha mashine zilizoingizwa kutoka nje kuchelewa kufika wakiwamo wataalamu wake hadi kufikia, Julai mwaka jana, zilipoingia na kuanza kufungwa.

Alisema mradi huo pia utaongeza kipato cha wakulima kwa kununua mazao ambayo yatatumika kutengeneza chakula cha mifugo kwa ajili ya kunenepesha mifugo kabla ya kuchinja.

Waziri Ndaki, akizindua mradi huo, alisema umetafsiri dhamila ya serikali katika kupambana na umaskini kwa kutoa ajira kwa Watanzania, wafugaji kupata soko la uhakika la mifugo na kuongeza mapato ya serikali yatokanayo na kodi mbalimbali pamoja na kuleta fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nyama.

"Inapotokea wawekezaji katika sekta, tafsiri yake uwekezaji wao unakwenda kuinua wafugaji na wakulima ambao ndio kundi kubwa la Watanzania. Nawapongeza PSSSF na wabia wengine kwa kugusa kundi kubwa la Watanzania," alisema Ndaki.

Aliwataka wawekezaji kuzingatia viwango vinavyotakiwa katika soko la nje ili kuleta ushindani kwa vile mahitaji ya nyama nje ya nchi ni makubwa tofauti na kiasi kinachozalishwa.

Waziri alitolea mfano kwa sasa masoko ya nyama ya nje yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika nchi za Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Jordan, Bahrain, Kuwait, Hong Kong, Vietnam, Comoro na Kenya.




Meneja wa TEHAMA wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Kabora Mboya, akizungumza na wananchi wakati wa ufunguzi wa mchezo wa bahati nasibu wa Kampuni ya Gama, Dar es Salaam, jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Wilfred Magotti. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ma-DC Ubungo, Ilala kicheko mabilioni uboreshaji wa maji

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Wilaya ya Ubungo, Heri James na mwenzake wa Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, wamemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha Sh. bilioni 11.7 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika wilaya hizo, hivyo kuchangia upatikanaji wa huduma kwa wananchi 629,476.

Walizungumza hayo kwa nyakati tofauti tofauti wakati wakiwasilisha mada kwenye mdahalo wa maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru ulioandaliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

James alisema katika miaka 61 ya Uhuru, katika wilaya ya Ubungo, serikali imewezesha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii zikiwamo maji, elimu na afya.

Pia aliwapongeza DAWASA kwa kuhakikisha Ubungo inapata huduma ya majisafi na kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa maeneo ambayo hayajapata huduma.

Alisema serikali imetatua changamoto ya huduma ya majisafi katika wilaya ya Ubungo kwa kutekeleza mradi wa Sh. bilioni 65.4 pamoja na mradi wa Mshikamano (Sh. bilioni 4.8) ambayo yote inakamilika mwezi huu na kutoa huduma kwa wananchi wote wa Ubungo, Goba, Kibamba, Saranga na Mbezi.

"Nipende kumshukuru sana Rais Samia kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha za miradi ya maji ambayo ikikamilika itagusa maeneo mengi katika wilaya ya Ubungo yenye changamoto ya maji pamoja na miradi ya elimu na afya ambazo ni huduma muhimu kwa jamii," alisema.

Naye Ludigija alisema ndani ya miaka 61 ya Uhuru, serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo majisafi na usafi wa mazingira hususani kwenye maeneo ya kihuduma.

Alisema kwa sasa upatikanaji wa maji kwa maeneo ya mijini imefikia asilimia 95 ambapo wakazi wengi ya wilaya ya Ilala wamepata maji.

"Huduma ya maji imeimarika sana kutoka kipindi cha Uhuru mpaka sasa, maeneo kama Chanika, Pugu, Gongo la Mboto hadi Kisarawe sasa wanapata maji ya uhakika," alisema.

Pia alisema maeneo mengine kama Nzasa, Somelo utekelezaji wa mradi unaendelea na utapokamilika tatizo la maji litakuwa limekwisha kabisa na kwamba hayo ni mafanikio makubwa tangu nchi ipate Uhuru.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, aliwataka wananchi wa Kinondoni kuendelea kuwa na imani na serikali kwa kuwa imefanya kazi kubwa ya kuboresha huduma mbalimbali za kijamii.

Alisema serikali imefanikiwa kutekeleza miradi mikubwa yenye lengo la kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya majisafi, hususani maeneo ya Makongo, Goba, Salasala, Mivumoni, Tegeta, Wazo, Bunju na Mbweni.

# CCM yaibua madudu ujenzi kituo cha afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeshtukia matumizi ya Sh. milioni 250 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Mwaja, kata ya Mandewa Manispaa ya Singida na kuomba uchunguzi ufanyike kubaini madudu kwenye mradi huo.

Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Kata ya Mandewa wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata hiyo, Hamis Ireme, walisema hayo jana jana baada ya kutembelea mradi huo na kukuta milango iliyowekwa kwenye jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na maabara imepasuka na kuweka nyufa.

Katibu wa CCM Kata ya Mandewa, Yusuph Kijanga, akizungumza baada ya wajumbe wa kamati kukagua mradi huo, alisema chama hakijaridhishwa na ujenzi wa majengo ya OPD na maabara ambao ulisimamiwa na viongozi wa manispaa na kwamba hawatakuwa tayari kuupokea utakapokabidhiwa.

Kijanga alisema mradi huo ambao serikali ilitoa Sh. milioni 500 kwa awamu, Sh. milioni 250 zilizotolewa awamu ya kwanza na ujenzi kusimamiwa na viongozi wa Manispaa ya Singida ndio umebainika kuwa na kasoro, hivyo kutilia shaka mamilioni hayo yalivyotumika.

Naye Diwani wa Mandewa, Baraka Hamis, alisema Sh. milioni 250 zilizotolewa awamu ya pili kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, upasuaji, jengo la kufulia na vyoo ambao ulisimamiwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) ujenzi wake umekwenda vizuri hauna kasoro yoyote.

Alisema changamoto imejitoka katika Sh. milioni 250 zilizotolewa awamu ya kwanza kwa ajili ya ujenzi wa maabara na jengo la wagonjwa nje ambao ulisimamiwa na viongozi wa manispaa.

**HABARI KITAIFA**

# Usafi bahari chachu kufikia uchumi buluu

**Na Jenifer Gilla**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Ally Possi, amesema ili kufikia uchumi wa buluu hakuna budi kulinda mazingira ya bahari na viumbe vyake kwa kuzuia utupwaji wa taka na maji yanayobebwa na meli za mizigo kwa ajili ya kuweka uwiano.

Aliyasema hayo jana alipofungua warsha ya kikanda ya

Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti na Usimamizi wa Maji na Taka za Meli ulioandaliwa na Shirika la Bahari Duniani (IMO), jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na nchi wanachama kutoka mataifa mbalimbali.

Alisema ingawa hali ya uchafuzi kwa sasa sio mbaya, ni muhimu kwa Tanzania kulinda bahari hiyo kwa kuungana na dunia kuridhia mkataba huo kwa ajili ya kuweka kanuni na sheria itakazozitumia kudhibiti uchafuzi wa bahari na viumbe vilivyomo hapo baadaye.

**Elimu itakayotolewa kati warsha hiyo itasaidia kuhifadhi mazingira ya bahari dhidi ya maji yanayomwagwa na meli za mizigo.**

"Lakini ifahamike kuwa vyanzo vya maji hususani bahari vinasimamia Sera ya Uchumi wa Buluu, sasa bahari inapochafuka, inapoharibiwa sera ya uchumi wa buluu inakuwa ngumu kutekelezeka kwa sababu viumbe bahari vitapotea na vitendea kazi vya bahari vitaharibika," alisema.

Possi alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa una lengo la kuzingatia makubaliano ya kiitifaki ya kudhibiti umwagwaji wa maji bahari machafu ambao ulipitishwa mwaka 2004 na kuanzia kutumika mwaka 2007 ambao Tanzania ni mmoja wa wanachama.

Alisema Tanzania inaunga mkono kuridhiwa kwa mkataba huo kwa kuwa inaelewa umuhimu wa kulinda bahari na viumbe vilivyoko hasa katika kipindi hiki ambacho inaipa kupaumbele uchumi wa buluu kama moja ya vyanzo vya kuletea taifa mapato.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Kaimu Mkeyenge, alisema dhumuni la warsha hiyo ni kupata uwelewa ili kudhibiti maji yanayokuja na meli za mizigo kutoka nchi nyingine kumwagwa katika bahari na kuathiri ikolojia.

"Uchumi wa buluu unaweza usifikiwe kama haya maji hayadhibitiwi, kwa hiyo lengo kubwa la warsha hii ni kutoa uelewa mpana wa maana ya mkataba huu wa kimataifa ili wadau wawe na uelewa wa pamoja wa kulinda mzingira ya bahari na kuufikia uchumi huo," alisema.

Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Stella Katundu, alisema elimu itakayotolewa kati warsha hiyo itasaidia kuhifadhi mazingira ya bahari dhidi ya maji yanayomwagwa na meli za mizigo.

"Hayo maji yanayobebwa katika meli yana viumbe tofauti ambayo sio wa asili ya huku kwetu, kwa hiyo yakimwagwa katika bahari yetu viumbe hao wanaweza kuwa hatarishi kwa viumbe wa hapa kwetu jambo ambalo kimazingira sio sawa, kwa hiyo elimu itakayotolewa pamoja kupitia mkataba wa kuzuia vitendo hivyo tutasaidia kulinda mazingira yetu," alisema.

Stella alisema Tanzania ikiwa moja ya nchi wanachama wa IMO imeshaanza mchakato wa kupitia mkataba huo na hatua ilipo sasa ni kupokea maoni ya wadau wa usafiri wa baharini wa hapa nchini kisha watapeleka majibu ya kuuridhia ama kutoridhia.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Women Fund Tanzania, Prof. Ruth Meena (katikati), akisoma tamko la Wanamtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania, lilitolewa makao makuu ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo Dar es Salaam jana. Wengine ni wajumbe wa wanamtandao hao, Shamshad Rehematullah (kulia), Dk. Hellen Kijo-Bisimba, Rose Marandu na Clemence Mwombeki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mil. 900/- kukarabati hospitali

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Hospitali ya Mkomaindo, Halmashauri ya Masasi, mkoani Mtwara.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, Elias Ntiruhungwa, alitoa taarifa hiyo wakati wa kongamano la kumbukizi ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika lililofanyika mjini hapo.

Ntiruhungwa alisema lengo ni kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi na kwamba ni mafanikio makubwa yanayofanywa na serikali.

"Hospitali yetu imepata fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya majengo fedha hizo ni zaidi ya Sh. milioni 900 ambazo zinakwenda kuifanya hospitali yetu kuwa ya kisasa...na hapa tunampongeza Rais Samia Suluhu kwa kutupatia fedha hizi," alisema Ntiruhungwa.

Alisema Masasi ni miongoni mwa wilaya zilizofanikiwa kuboresha miundombinu, kuanzia sekta ya elimu, afya, barabara, umeme na maji na hiyo ni ndani ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema serikali zote zilizoongoza na iliyoko madarakani kwa sasa zimefanya kazi kubwa ya kimaendeleo ndani ya Wilaya ya Masasi na wananchi wanafurahia matunda ya serikali yao huku wakifurahia miaka 61 ya Uhuru.

Ntiruhungwa alisema Masasi wanaipongeza serikali ya sasa na zilizopita kwa kuipatia fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo tangu na kabla ya Uhuru.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa chache ambazo tangu kupatikana kwa Uhuru ziliundwa na sasa zimekuwa na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali za kijamii.

## Wanolewa uchukuaji wa vipimo vya DNA

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imetoa mafunzo kwa maofisa ustawi wa jamii wa mkoa wa Dar es Salaam ya kuwajengea uwezo kuhusu uchukuaji wa sampuli za vinasaba vya binadamu (DNA).

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alifungua mafunzo hayo jana jijini humo na kusema kundi hilo ni muhimu kwa kuwa linafanya kazi na jamii ya kuomba vipimo vya DNA kwa ofisi ya GCLA.

Alisema wameona kuna umuhimu kukaa na kundi hilo kuwaelimisha kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu ya Mwaka 2009.

"Tunawapa elimu ya upimaji wa DNA upoje, muda ambao unachukua kupata majibu ya kipimo, gharama za kipimo, sababu za kipimo kuchelewa na nani apewe majibu kwa sababu ndiyo mambo ambayo wananchi wanataka kujua kutoka kwao," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema wanashindwa kutoa takwimu za wanaopeleka mashauri kuomba vipimo vya DNA kwa sababu idadi kubwa ya mashauri inapitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Alibainisha kuwa eneo linaloongoza kwa kuwa na mashauri mengi ni makosa ya jinai, majanga na uchafuzi wa mazingira.

Dk. Mafumiko alisema kuhusu kujua uhalali wa watoto, idadi siyo kubwa kama wananchi wanavyodhani.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Nyamara Elisha, alisema moja ya matatizo katika majibu ya vipimo vya DNA ni wananchi kutokubaliana na matokeo ya vipimo vya kupata uhalali wa mtoto.

Alisema takwimu za wazazi kukataa watoto zinaongezeka nchini kulingana na ongezeko la idadi ya watu inavyoendelea kukua.

# TGNP yawanoa maofisa viungo jinsia wizara 10

**Na Maulid Mmbaga**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umetoa mafunzo kwa maofisa viungo wanaoshughulikia masuala ya jinsia katika wizara 10 ili kuwakumbusha umuhimu wa kujumuisha katika mipango na miongozo mbalimbali ya serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Naibu Mratibu wa Mafunzo kutoka TGNP, Anna Sangai, alisema masuala ya jinsia ni muhimu kwa kuwa yanahusisha makundi yote katika jamii kwasababu ndiyo waratibu wa suala hilo wizarani.

Alisema maofisa hao wakielewa dhana, miongozo na mipango ambayo serikali imeridhia ndani na nje ya nchi katika kufikia usawa wa kijinsia, mipango itakayopangwa na bajeti zitaelekeza kufikia wa kijinsia.

"Katika kulifanikisha hilo tumechagua wizara mbalimbali ikiwamo ya elimu, maendeleo ya jamii, maji na kilimo, kwasababu tunaamini zote hizo zinahusiana na jamii na kuna changamoto ambazo ili zitatuliwe zinahitaji tangu awali mipango na bajeti za wizara ziwe zimeelekezwa kutatua matatizo hayo," alisema Anna.

**Uelewa nao ni tatizo kutokana na hali halisi iliyoko, hatuna takwimu toshelezi ambazo zinaweza zikatuambia hali ilivyo katika kila sekta, sekta ya elimu inajitahidi.**

Naye Ofisa Maendeleo Mwandamizi kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorah George, alisema mafunzo hayo yanayoratibiwa na TGNP ni muhimu, na yanafanyika kipindi sahihi ambacho serikali inatarajia kuanza mchakato wa maandalizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Pia alisema wanawake nchini wanakumbwa na changamoto ya vikwazo katika kuwaletea maendeleo na hata kuchangia katika pato la uchumi, akieleza kwamba wanahakikisha bajeti za sekta zinazingatia na kuongeza fedha maalum ili kuhakikisha masuala ya jinsia na changamoto za wanawake zinashughulikiwa.

"Wizara yetu inaratibu masuala mbalimbali ikiwamo programu ya kitaifa ambayo Rais Samia Suluhu Hassan amehakikisha wanawake wanawezeshwa kiuchumi, 'commitment' ambayo aliifanya 2021 nchini Ufaransa ikiwa ni azimio mojawapo la Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha tunafikia usawa wa kijinsia," alisema Dorah.

Alisema katika kipindi hiki cha kutekeleza makubaliano hayo, mafunzo yanayotolewa na TGNP ni muhimu na yatasaidia wanawake kuwezeshwa na kuimarisha uchumi wa nchi.

Aidha, alieleza kuwa katika kila taasisi kuna mipango sera na sheria ambazo zinaongelea masuala ya jinsia, akibainisha changamoto inakuja katika utekelezaji kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa rasilimali fedha na uelewa.

"Uelewa nao ni tatizo kutokana na hali halisi iliyoko, hatuna takwimu toshelezi ambazo zinaweza zikatuambia hali ilivyo katika kila sekta, sekta ya elimu inajitahidi, lakini tunajitahidi kuhakikisha sekta zingine zinakuwa na takwimu hizo ili mipango tunayoipanga itatue changamoto zilizoko," alibainisha Dorah.



Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Isaac Njenga (kushoto), pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii, Damas Ndumbalo, wakigonganisha glasi wakati wa maadhimisho ya Miaka 58 ya Uhuru wa Kenya (Jamuhuri Day) jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Viongozi dini watoa neno kukithiri ukatili

**Na Moshi Lusonzo**

KUSHAMIRI kwa vitendo vya dhuluma dhidi ya watoto na wanawake kumeelezwa kuwa ni ishara jamii kutoka katika mafundisho ya dini yanayohimiza upendo na uadilifu.

Akizungumza hivi karibuni katika kongamano la siku tatu la viongozi wa Taasisi ya Maljis Ansarullah ya Jumuiya ya Kiislam ya Ahmadiya, Shekhe Ally Hamis Mbambwa, alisema kukithiri kwa matukio hayo kunaonesha jinsi watu walivyokosa uvumilivu na imani.

Alisema viongozi wa dini mbalimbali wana wajibu wa kutoa mafundisho ya kiroho kuanzia ngazi ya familia ambako malezi yanaanzia.

Shekhe Mbambwa alisema taasisi hiyo yenye kazi ya kusimamia mafundisho ya dini na ustawi wa jamii, inaendelea kutoa elimu ya malezi yanayozingatia utu na upendo kuanzia shule za msingi hadi vyuoni.

"Tunajua kuna kushamiri vitendo vya unyanyasaji na dhuluma kwa watoto na wanawake, kuenea kwa mambo haya inaonesha jinsi gani jamii imeshindwa kuzingatia malezi yanayohimiza upendo na hofu ya Mungu," alisema.

Akizungumzia kongamano hilo linalohudhuriwa na viongozi 200 kutoka mikoa yote, alisema mafunzo mbalimbali yanatolewa ikiwamo ukamilifu wa Quran na kuwafanyia matendo mema kwa watu wengine.

"Maljis Ansarullah tuna wajibu wa kusimamia mambo haya kutokana na umri wetu ambao wengi wetu tuna nguvu na akili ambazo zinaweza kusimamia kitu na kuleta matokeo chanya," alisema.

Naibu Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Dk. Swaleh Kitabu, alisema kazi kubwa ya chombo hicho ni kusimamia na kutekeleza mipango ya jumuiya kuleta maendeleo kwa jamii.

Alisema viongozi hao wanajifunza mambo mbalimbali ya kidini na kurudisha uzalendo ndani ya jamii.

"Tunahimiza kufanyakazi kwa kujitolea na kuboresha afya zetu kwa kufanya mazoezi, yote haya tunakwenda kutekeleza kikamilifu tukirudi katika maeneo yetu," alisema Dk. Kitabu.

Alisema Jumuiya ya Ahmadiya inajihusisha na kazi mbalimbali nchini ikiwamo miradi ya shule, hospitali, maji na mazingira.

# Mradi kuwanoa wanawake kiuchumi, uongozi

**Na Julieth Mkireri**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angella Kairuki, amezindua mradi wa uongozi na haki za kiuchumi kwa wanawake utakaotekelezwa katika mikoa sita na wilaya 18 nchini.

Mradi huo utakaotekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojishughulisha na Wanawake (UN Women) kwa ufadhili wa Serikali ya Finland unatarajia kugharimu Sh. bilioni 19.

Kairuki alisema lengo ni kuwaelimisha wanawake kutambua fursa za kiuchumi na kuwajengea uwezo wa kushiriki kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

"Mradi huu kwa kuanza utakuwa katika mikoa sita, lakini tunaendelea kutafuta wabia wengine kwa ajili ya kuifikia mikoa mingine ambayo haijaguswa, lengo wanawake watambue fursa zilizoko kiuchumi," alisema.

"Huwezi kumwambia mwanamke akashiriki mambo ya kisiasa wakati haelewi nyumbani kwake watoto watakula nini wataendaje shule tunataka kuwajenga katika maeneo yote," alisema Kairuki.

Aliwakumbusha wanawake kujiamini na wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia kujitokeza ili wahusika wachukuliwe hatua.

Balozi wa Finland nchini, Theresa Zitting, alisema serikali ya nchi hiyo itaendeleza ushirikiano kati yake na Shirika la Kimataifa la UN Women pamoja na Tanzania.

Katibu Tawala Mkoa wa Lindi, Ngusa Samike, alisema watumishi watakaoshiriki mradi huo wameshapatiwa mafunzo na hatua inayofuata ni kwa asasi na kushusha mafunzo hayo ngazi ya jamii.

Alisema mafunzo hayo yatamjenga mwanamke namna ya kumkomboa kiuchumi na kushiriki kugombea nafasi za uongozi.

Mkuu wa mradi huo kutoka UN Women, Erasmina Massawe, alisema mradi huo una malengo manne yakiwamo kufanya kazi kwa karibu na serikali za mitaa, kuibua fursa na kubadili mila desturi na kanuni.

Aidha, alisema serikali za mitaa, asasi za kiraia na redio za kijamii zitashirikishwa kikamilifu.

"Pia tutawajengea uwezo wanawake waweze kushiriki nafasi za uongozi kuanzia ngazi ya vijiji, kushiriki utengenezaji wa bajeti wenye lengo la kijinsia fursa kwa mwanamke katika kushiriki utekelezaji wake," alisisitiza.

Katibu Mkuu TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, aliishukuru Finland inavyoshirikiana na UN Women na Serikali ya Tanzania na kuahidi ushirikiano katika utekelezaji wa mradi huo.

Mradi huo wa miaka minne utatekelezwa katika mikoa ya Dar es Salam, Pwani, Arusha, Lindi, Mtwara na Singida, na asasi za kiraia zinazojihusisha na masuala ya wanawake.

HABARI KASKAZINI

## Maofisa elimu waagizwa kuwabaini watoto wenye mahitaji maalum

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amewaagiza maofisa elimu maalum nchini kuhakikisha wanasimamia uchunguzi wa awali wa watoto ili kubaini watoto wenye mahitaji maalum.

Kairuki alitoa agizo hilo jana alipokuwa katika Chuo cha Ualimu Patandi kilichoko wilayani Arumeru mkoani Arusha, wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa maofisa elimu watu wazima na maofisa elimu maalum.

Waziri Kairuki aliwataka maofisa hao kuhakikisha wanatumia vituo vya uchunguzi na kuwaelekeza watoto wenye mahitaji maalum katika shule stahiki ambazo wanapaswa kupelekwa ili wapate afua stahiki.

"Nafahamu mkiwabaini watoto hawa wenye mahitaji maalum watapata stahiki zao zinazotakiwa bila shida, hivyo lazima msimame katika kuwafanyia watoto uchunguzi wa kina ili kuwabaini," alisema Kairuki.



Pia alielekeza shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu zihusishe kikamilifu masuala ya elimu maalumu na elimu ya watu wazima, kwa kuhakikisha wanashirikiana na viongozi katika jamii kuratibu shughuli za elimu katika shule za msingi na sekondari.

Waziri Kairuki alisema: "Lakini nyie maofisa wekeni utaratibu wa kupokea wanafunzi wenye mahitaji maalum wa kidato cha kwanza, darasa la kwanza na awali kwa mwaka 2023, kwa kushirikiana na viongozi katika maeneo yao, ili kuweka mazingira bora kwa wanafunzi hao".

Pia aliwataka viongozi wa elimu katika ngazi ya shule, kata, halmashauri na mikoa kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji shuleni na kushirikiana na walimu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata umahiri uliokusudiwa badala ya kukaa ofisini.

Alisema kila mwalimu anapaswa kujiwekea malengo binafsi katika masomo anayofundisha na kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeshindwa kupata umahiri uliokusudiwa katika somo lake ifikapo mwishoni mwa kila mwaka.

**Nafahamu mkiwabaini watoto hawa wenye mahitaji maalum watapata stahiki zao zinazotakiwa bila shida, hivyo lazima msimame katika kuwafanyia watoto uchunguzi wa kina ili kuwabaini.**

# Shirika lakabidhi msaada wa vyoo shule ya msingi

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

**Kabla ya shirika hilo kujenga vyoo hivyo kulikuwa na uhitaji mkubwa kwamba wametoa misaada mbalimbali ikiwamo ujenzi wa darasa la awali.**

SHIRIKA la AKO la nchini Ujerumani kupitia tawi lake la Tanzania Community Support, limekabidhi mradi wa vyoo vya kisasa kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kambi ya Chokaa iliyoko Kata ya Naisinyai, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Hilda Kimath, akizungumza wakati akikabidhi mradi huo, alisema utengenezaji wa vyoo hivyo umegharimu Sh.milioni 68.

Alisema vyoo hivyo vya kisasa vina matundu 14 vitatumiwa na wasichana matundu nane na wavulana watatumia matundu sita.

Kimath alisema: "Kwenye vyoo hivyo vya wasichana matundu nane kiko kimoja cha walemavu na matundu sita ya wavulana pia kuna kimoja cha wenye ulemavu".

Diwani wa Kata ya Naisinyai, Taiko Laizer, alilishukuru shirika hilo kwa kuwajengea wanafunzi hao vyoo kwamba wameisaidia serikali kutimiza wajibu wake.

Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Halmashauri ya Simanjiro, Abdalah Hamis, amewataka walimu na wanafunzi kuhakikisha wanatunza miundombinu hiyo ili idumu kwa muda mrefu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Praxeda Tarimo, alisema kabla ya shirika hilo kujenga vyoo hivyo kulikuwa na uhitaji mkubwa kwamba wametoa misaada mbalimbali ikiwamo ujenzi wa darasa la awali.

"Pia AKO Tanzania wamesaidia ujenzi wa majiko ya wanafunzi wa darasa la awali na shule ya msingi, kadhalika wamefanikisha ujenzi wa mradi wa maji shuleni, kutoa chakula kwa wanafunzi, printa na mashine ya kurudufisha," alisema Tarimo.

Mwanafunzi wa darasa la sita wa shule hiyo, Christina Julius, alilishukuru shirika hilo kwa kuwajengea vyoo hivyo akisema kwamba vilivyokuwapo awali vilikuwa vimechakaa.

Alisema: "Sasa hivi tunajisitiri vyema tukiwa faragha na tumetengewa eneo maalumu la kubadili taulo za kike kwa wale wasichana wakubwa waliopevuka."



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (kushoto), akiteta na mawakili wake, katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, kabla ya kuanza kusikilizwa kwa rufani ya kesi ya uhujumu uchumi namba 27. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Mashirika yasiyo ya kiserikali yajengewa uwezo ujenzi miradi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA la DSW Tanzania limeendelea kuyajengea uwezo mashirika yasiyo ya kiserikali ngazi ya kitaifa ili yaweze kutekeleza miradi ya vijana.

Mkurugenzi wa Shirika la DSW Tanzania, Peter Owaga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika mafunzo ya siku tatu kwa wawakilishi wa mashirika kutoka mikoa minne ya Arusha, Dodoma, Mwanza na Dar es Saalam.

Mafunzo hayo yalienda sambamba na uzinduzi wa kitabu cha mchakato wa kutengeneza mpango mkakati.

Peter alisema kuwa kati ya wadau walionao wanaangalia mashirika yanayofanya kazi na vijana na wanawake, kwamba mashirika hayo yamekuwa yakitumia muda mwingi kuelimisha masuala ya afya ya uzazi.

Alisema mashirika mengine yamekuwa yakitumia vikatuni pamoja na kuwatumia watu wa makundi maalumu ili nao waweze kuifikia jamii yao kwa kupata huduma wanazotoa.

Meneja Uragibishi kutoka Shirika la DSW Tanzania, Philomena Marijani, alisema kuwa mradi huo unalenga zaidi wanawake na wasichana, huku ukiwa na malengo ya kuhakikisha wanapata huduma bora ambazo zinakidhi viwango na kuweza kufikia malengo yao.

Alisema: "Mradi huu mwisho wa siku ni kuona kunakuwapo kwa mazingira wezeshi ya usawa kwa vijana na wanawake kwa afya bora na hivyo kuweza kuondokana na matatizo mbalimbali yaliyokuwa yakiwakabili katika kupata huduma hizo".

Mwandishi wa kitabu hicho, Evans Lushakuzi, alisema lengo la kuandika kitabu hicho ni kusaidia viongozi katika mashirika yasiyo ya kiserikali kuweza kutengeneza mikakati yao ya maendeleo kwa kutumia mchakato uliopendekezwa katika kitabu hicho.

Alisema misingi ya kitabu hicho inaweza kutumiwa na jamii yoyote au taasisi za kimaendeleo pamoja na mashirika mbalimbali.

# Mganga Mkuu: Wafamasia feki washamiri Kilimanjaro

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Jairy Khanga, amesema mkoa huo unakabiliwa na uwapo wa wahudumu feki na wasio na sifa wanaouza maduka ya dawa baridi za binadamu.

Pia amesema wamiliki wa maduka hayo wanatuhumiwa kusambaza dawa, vitendanishi na vifaa tiba ambavyo havijasajiliwa.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao kazi cha siku moja kilichoandaliwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

"Wapo baadhi ya wamiliki wa maduka wasio waaminifu, husambaza dawa na vifaa tiba ambavyo hazijasajiliwa, hutoa huduma za kitabibu kinyume na sheria na wengine kununua dawa zinazotoka katika hospitali zetu hapa nchini.

"Hata hivyo, baadhi ya maduka hayana wasimamizi sahihi kama inavyoainishwa na kwenye sheria. Na kumezuka tabia kwa watoa huduma (wafamasia) kwenye maduka ya dawa kuacha cheti cha mtaalamu kwenye maduka zaidi ya moja na kwenda kufanya shughuli nyingine. Tukifika hapo na kubaini hivyo, hatua kali zitachukuliwa, haya ni maisha ya watu," alisema Khanga.

**Hawa ni wahujumu uchumi na wauaji, kwa kuwa wanafanya biashara haramu na zenye athari kubwa kwa afya za binadamu na wanyama.**

Aprili mwaka huu Mfamasia na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafamasia Tanzania, Benson Katundu, alinukuliwa akikemea ukiukwaji wa sheria inayosimamia maduka ya dawa muhimu, hasa watoa huduma wasio na taaluma ya dawa kuhudumia kwenye maduka ya dawa.

Wakati anafungua kikao kazi hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Willy Machumu, aliielekeza TFDA kuchukua hatua dhidi ya wamiliki wa maduka hayo wanaoitwa kwenye vikao kazi na kupuuzia wito huo.

"Hawa ni wahujumu uchumi na wauaji, kwa kuwa wanafanya biashara haramu na zenye athari kubwa kwa afya za binadamu na wanyama. Hatutawavumilia, kushindwa kufika bila kutoa taarifa ni kosa," alisema Machumu.

Katika kikao hicho Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa TMDA, Patrick Prochesi, alisema hivi sasa jitihada kubwa zinafanyika kwa kushirikiana na wadau na wamiliki wa maduka ya dawa, kuhakikisha dawa ambazo ni sumu na hazijasajiliwa zisiweze kuingia nchini.

Alisema: "Ni jukumu la TMDA kuhakikisha dawa na vitendanishi, vinavyotengenezwa na kuingiza nchini ni salama kwa binadamu na wanyama, hakuna bidhaa bandia au ambazo hazijasajiliwa zitaingia, licha ya mkoa huu kuwa mpakani.

"Wapo waingizaji ambao wanafuata taratibu zetu za kuomba vibali na kufuata dawa zao kwenye vituo rasmi, lakini wapo ambao hawazifuati na hupitisha njia zisizo rasmi hali ambayo wanahatarisha afya za watu na wanyama."



Mkuu wa Wilaya mstaafu wa Semanjiro, Samweli Kamote, akizungumza na wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga juzi katika kongamano la Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania, aliwaeleza jinsi alivyotembea pekupeku bila kuvaa viatu miaka nane kutoka nyumbani kwenda Shule ya Msingi Magila mkoani Tanga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wazalishaji wa ngozi walia kukosa soko

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZALISHAJI wa ngozi nchini wamelalamika kukosa soko la uhakika la ndani baada ya serikali kupiga marufuku usafirishaji wa ngozi kwenda nje.

Wakizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalumu, baadhi ya wafanyabiashara wa ngozi mkoani Kilimanjaro, waliiomba serikali kulegeza masharti kwa kuruhusu usafirishaji wakati mchakato wa kufufua na kuanzisha viwanda vya ngozi ukiendelea.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Woisso Original Products (WOP), Kenneth Woisso, alisema licha ya serikali kuweka jitihada mbalimbali katika kukuza soko la ngozi, ipo haja ya kutafuta masoko ya uhakika ili kufanya biashara hiyo ikue zaidi ya hapa ilipo kwa sasa.

"Kuuza bidhaa hiyo kwa mtu mmoja mmoja bila kuwa na uhakika wa soko, bado inaweza kuwa ni vigumu, lakini kama zitatumika njia nyingine, mfano balozi za Tanzania zinapaswa kuunganisha wanunuzi na wazalishaji wa humu ndani ili kuongeza wigo wa masoko zaidi.

"Wenzetu wa China wanajiweza kimtaji, kwa hiyo na sisi kama tunaenda kufanya nao biashara ni lazima tujipange kikamilifu, maana kwanza hatuna uzoefu lakini hata mteja mwenyewe hatujui kwa kumpata," alisema.

Mfanyabiashara mwingine, Faustine Sanga, akizungumzia tatizo la soko hilo, alisema kwa sasa biashara hiyo inaonekana kukumbukwa tofauti na ilivyokuwa kwa kipindi cha nyuma na kwamba jitihada hizo zikiendelea sekta hii itaenda kufikia mahali pazuri.

Alisema njia pamoja na mifumo inavyozidi kuimarishwa inaleta matumaini kwani kuna muda ulifikia biashara hiyo ikawa inahujumiwa sambamba na soko la ndani kudidimia kwa kiwango kikubwa.

Hivi karibuni serikali imeweka jitihada katika kufufua sekta ya ngozi ikiwa ni pamoja na kuongeza tozo kwa bidhaa za ngozi zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

# Naibu Waziri awafunda wanafunzi Wamasai elimu ya juu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Madini, Dk.Steven Kiruswa, amewapa somo wanafunzi wa jamii ya kifugaji ya kimasai wanaosoma elimu ya juu kutokubali kuitupa mila yao kwa sababu ya mabadiliko ya mfumo wa maisha.

Bali amewataka kuendelea kudumisha mila nzuri na desturi kwa ajili ya kuweka na kuhifadhi kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Alitoa ushauri huo jana jijini Arusha wakati wa mahafali ya kwanza ya Jumuiya ya Wanafunzi wa Jamii ya Kifugaji (AMASA).

Alisema: "Wanafunzi wangu hakikisheni mnaendeleza mila na desturi ambazo ni nzuri kwa ajili ya kuweka na kuhifadhi kumbukumbu kwa ajili ya vizazi vijavyo kwa kuwa kabila letu ni moja ya makabila nchini ambayo yanaendelea na utamaduni wake.

"Mila zote zina vipengele vizuri na vibaya lakini mimi nimewasihi na kuwasisitiza wanafunzi waendeleze kudumisha mambo mazuri ikiwamo mavazi yao ya asili, ujasiri na tabia ya kuheshimu watu katika jamii," alisema.

Dk.Kiruswa ambaye ni Mbunge wa Longido alisema katika safari yake ya elimu ameandika hadithi za jamii ya Kimasai maandiko zaidi ya 200 na hadi sasa ameshatafsiri maandiko 70.

Pia alisema kuna umuhimu kwa jamii hiyo kutoa fursa kwa watoto wa kike na wakiume kupata elimu kwa kuwa awali walijikita zaidi kwenye suala la mila kuliko kuwapeleka wanafunzi shuleni.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Wafugaji Tanzania (TPCF), Joseph Parsambei, alisema wamefanikiwa kupiga hatua baada ya kuwekeza na kuwahamasisha wanafunzi wa Kimasai kusoma ili kwenda kuikomboa jamii yao .

"Jamii za wafugaji kimsingi ni muhimu zipate elimu kama mpango mbadala kwa kuwa hali halisi ya ufugaji imekuwa ngumu hivyo kutokana na mazingira yenyewe," alisema Parsambei.

Alisema moja ya matatizo yanayowakabili Wamasai ni kuwapo kwa baadhi ya sheria ambazo haziungi mkono suala la ufugaji.

Ukurasa 15




**UCHAGUZI UWT TAIFA: Mary Chatanda aeleza 'alivyopindua meza' akivuka vikwazo kama 'hupati kura yangu'**

Ukurasa 18



M23 waendelea kupoa ni baada ya Marekani kuiwakia Rwanda

Ukurasa 19



**ALI HASSAN MWINYI+ UHURU 61**
**Anabakia bingwa kutibu uchumi uliokuwa 'ICU'**

siasa
JUMATANO DESEMBA 14, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

# Kura katika NEC-CCM kielelezo cha mambo, uchaguzi unaokuja



Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, akifurahi pamoja na wanachama wakati wa Mkutano Mkuu wa Dodoma.
**PICHA :CCM**

**Na Ani Jozeni**

HALI ya kawaida kwa wana CCM inaanza kurudi tena na kwa maana hiyo chama kinaweza kujitamba kuwa kinarejea kuwa kama kilivyokuwa hadi ulipofanyika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kwa na demokrasia pana, uhuru wa kutosha na pia kujiamini zaidi,

Kabla ya uongozi wa awamu ya tano siasa, na hasa ndani ya CCM, inaweza kuelezwa kuwa ilikuwa ikuhusishwa na mambo mengi kuanzia kuwapo ambao wanadaiwa walikuwa wakipigania kupata nafasi katika uongozi wa chama, lakini pia wakiwamo watiania wengi kuanzia ubunge na udiwani.

Kwa baadhi ya wagombea hao ilikuwa ni kwa ajili ya nafasi katika chama, kwa wengine ikawa ni matayarisho ya fursa za ubunge na kwa upande fulani udiwani au kwenye maeneo ya kuteuliwa.

Kupata nafasi ya kuchaguliwa katika chama tawala kunafungua njia kulingana na umri au viwango vingine kadhaa vya mgombea kwa mfano elimu na taaluma ili kufikia malengo tofauti.

Ni yale yanayohitajika ili mtu kuonekana na kupata alama fulani za kisiasa, kuwa anaweza kuwasaidia watawala katika ngazi moja au nyingine kufanikisha malengo, iwe ni katika chama chenyewe, au serikalini.

Nafasi serikalini zina vianzio vya kitaaluma kwa upande mmoja na utii wa kisiasa kwa upande wa pili, ambako kufahamika kitaaluma ni kazi ngumu, ila kuwika kisiasa na kupata fursa ni kama radi kila mmoja ataiona na kuisikia.

Licha ya kuwa matukio ya rushwa yalikuwepo na katika maeneo kadhaa uchaguzi mwaka huu na hata mwingine kufutwa, huku viongozi akiwamo Katibu Mkuu Chongolo na Makamu Mwenyekiti (Bara), Abdulrahaman Kinana kukemea, ni wazi kuwa ule woga uliokuwepo awali wa kutokuwepo mienendo kama hiyo umepungua, au haupo.

Inawezekana woga kuhusu suala hilo unaanza kuondoka ila pale wagombea walipovuka mpaka kuna hatua zilichukuliwa, licha ya kuwa siyo rahisi kusema kama zilichukuliwa bila kumwonea mtu haya, au zilitangulizwa na uangalifu kiasi fulani. Inabidi kufanya utafiti wa hapa na pale, kama si upelelezi, kujua hatua zilikuwa na 'macho' au hapana kwani zikiwa na macho zinaweza kuona haya; na kama hazina kuangaliana huenda watafinywa wote waliohusika.

Eneo mojawapo la mabadiliko yaliyotangazwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan ni ajira ya Makatibu wa Itikadi na Uenezi wa Mikoa, halafu kupanuliwa kwa idadi ya wajumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) ya Taifa ili chama kiwe na wakilishi zaidi katika maeneo tofauti.

Itakumbukwa kuwa idadi ya wajumbe wa NEC ilipunguzwa wakati wa usimamizi wa Mwenyekiti John Magufuli, kwani kulikuwa na madai kuwa kugombea nafasi hizo kulichochea rushwa na zikawa ni ngazi ya kutafuta wajumbe kugombea kuteuliwa kushika bendera ya CCM uchaguzi mkuu.

Mwenyekiti huyo akataka NEC ya wachapa kazi na siyo ya wawakilishi wa wale wenye 'safari ya matumaini,' iwe ubunge au hata urais.

Yako mabadiliko katika maeneo hayo kwa sababu CCM inahisi imebana sana ari ya makada wake kufikia uongozi, ikiangaliwa kuwa Tanzania ni nchi pana yenye wingi wa watu, hivyo kubana nafasi kuwa takriban 60 halafu na wenyeviti na makatibu wa mikoa ni tatizo kiasi fulani, hata ingawa wapo wanaoteuliwa.

Bado hata hivyo umuhimu wa wenyeviti na makatibu wa mikoa utaendelea kuwepo hasa pale kiti cha urais kinapokuwa wazi, na hilo linangoja kufanyika 2030.

Ina maana uongozi ulioingia madarakani utakuwa na kazi rahisi kiasi, na hautakuwa na mivutano kwani CCM inakuwa na umoja pale kiongozi akiwa anaendelea kukaa madarakani muhula mwingine. Tatizo linaanza pale nafasi hiyo ikifikia tamati kwa mwenye muhula wa pili, kwani wenye matumaini inabidi wajipange na kwa vile uchaguzi wa CCM unakuja katikati ya muhula wa utawala, ina maana

**INAENDELEA UK. 20**

# CCM Zanzibar yawaambia wanachama kumekucha

## •Makamu Abdulla akiwapa kijembe wanaosaka vyeo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**



Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Makamu Mwenyekiti wa CCM mstaafu,Ali Mohamed Shein, alipowasili katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui kutoka Dodoma, kwenye Mkutano Mkuu wa 10 wa chama hicho. **PICHA: IKULU**

HAWAKUKOSEA wahenga waliosema kuwa chanda chema huvikwa pete, ndivyo alivyohitimisha safari yake ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk Ali Muhammed Shein, aliyekiongoza chama hicho kwa muda wa miaka 10.

Disemba 7 mwaka huu Chama cha Mapinduzi kimefanya chaguzi zake ambazo kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Visiwani Zanzibar, kimemtangaza Dk Hussein Ali Mwinyi, ambaye pia ni Rais wa SMZ kuwa Makamu wa CCM, kukiongoza.

Anakuwa Makamu Mwenyekiti wa kwanza aliyezaliwa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ambayo watangulizi wake wote ni waliozaliwa kabla ya Mapinduzi hayo yaliyofanyika miaka 58 iliyopita.

Akizungumza visiwani humo baada ya kushika nafasi hiyo, Dk Mwinyi anasema uchaguzi umekwisha na kazi iliyopo sasa ni kukijenga chama ili kiendelee kushika dola.

Anawaambia wana CCM kuwa chama kimeshakamilisha chaguzi zake na hakuna mwingine hadi 2027 hivyo ni lazima kushikamana na kuondoa tofauti zao ili kuendelea kujenga nchi na chama chao.

Anasisitiza kuwepo na umoja na mshikamano katika ya wanachama na viongozi ili kusonga mbele kwa kuwa na nguvu na kushinda katika uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2025.

"Naomba tuwe wamoja tusiendeleze makundi yaliyokuwepo siku za nyuma uchaguzi umekwisha sasa ni kukijenga chama chetu na mshikamano wetu ndiyo utakaotuvusha na kupata ushindi mwaka 2025," anasema.

Makamu huyo, anaahidi kusimamia vyema utekelezaji wa ilani ya CCM kupitia serikali anayoiongoza katika kuongeza kasi ya utekelezaji wa ahadi alizowaahidi wananchi.

"Tutasukumana kweli kweli ndani ya serikali tuyatekeleze yote kwani yapo mambo kadhaa ambayo tumesema vipaumbele katika utekelezaji wa ilani yetu ikiwemo miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, bandari, maji, umeme na matumizi ya mifumo ya teknolojia. Tutakwenda kwa kasi ili mwaka 2024 ilani itakuwa imetimizwa," anaahidi.

Vipaumbele vyingine anasema ni huduma za kijamii ikitaja afya, elimu,nyumba za makazi za gharama nafuu, kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mikopo, ajira na kutengeneza mazingira bora ya wafanyabiashara wadogo kufanyakazi zao mambo ambayo yameshaanza kufanyika, anasema.

Akizungumzia suala la amani na utulivu Rais Mwinyi, anawaomba Wazanzibari na Tanzania kwa ujumla kuendeleza amani na usalama katika nchi waliyonayo kwani hakuna mbadala wa amani na usalama katika taifa lolote.

Anamshukuru mtangulizi wake Makamu Mwenyekiti mstaafu Dk. Ali Mohammed Shein, kwa kumkabidhi kijiti hicho na kuahidi kufata nyayo zake kwa sababu ameacha hazina katika chama ikiwamo uadilifu, uchapakazi na kukataa majungu na fitina na mambo hayo amewafundisha na ameyazingatia.

Anamwombea kwa Mungu aendelee kuwa na afya njema ili waendelee kuchota hazina alizonazo katika kukijenga chama chao na kuutumia ushauri wake maridhawa.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Hemed Suleiman Abdulla, anamhakikishia Makamu Mwinyi kwamba serikali anayoingoza itaendelea kufanya kazi kwa miongozo na kasi anayoitaka hasa katika kukamilisha ilani ya CCM kabla ya mwaka 2025.

Anasema yapo maeneo ambayo wameshafikia na kufanya mambo makubwa kwa kiwango cha asilimia 112.

"Kasi ambayo umetuelekeza na juhudi tulizonazo, watendaji wako itaongezeka mara mbili zaidi ya chama na serikali ili kufikia malengo tuliyoyakusudia na tunaamini atakayeshindwa na kasi hiyo basi atatusubiri mbele," anasema Abdulla.

Anabainisha kwamba ni imani yake watendaji wote wataongeza kasi, bidii na ubunifu ili kuweza kuitekeleza ilani kwa kumuunga mkono Rais Mwinyi na Makamu Mwenyekiti wa CCM kufikia ukamiishaji wa majukumu yake.

"Niwaombe watendaji wenzangu tusimkwaze Makamu Mwenyekiti kutekeleza majukumu yake yale tunayoyaweza tukayamalize na yasiowezekana tuyapeleke kwake ili kupata mwongozo tuyamalize," anasisitiza.

Anawaomba wanachama kuendelea kuimarisha umoja na mshikamano na kuimarisha kazi waliyopewa ya kuwatumikia Wazanzibari na Watanzania mwaka 2025 kazi yao iwe rahisi.

Sambamba na hayo anawaomba wanachama na viongozi kujenga chama chao na kusimamia serikali yao ili kufikia malengo waliyokusudia, majungu, fitina wanaotaka vyeo kwa nguvu bila stahili wajue kuwa vyote hivyo havina nafasi.

"Wakati huu ni lazima CCM kuwa wamoja na kama umekuja kwenye chama kutafuta cheo kwa majungu, fitna basi hufai nimeyasema haya kwani tayari wapo wanaopanga safu na watatuma watu kuja kwako na watakwenda kwa Mwenyekiti Rais Samia ili wapate cheo na wengine ni viongozi," anasema Abdulla.

Anampongeza Makamu Mwenyekiti mstaafu kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kukijenga chama kwani mpaka anakabidhi kijiti chama bado kipo imara na wataendelea kuchota busara zake

Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi Taifa, Shaka Hamdu Shaka, akiwa kwenye mapokezi hayo, anasema mambo makubwa yanakwenda kufanywa na Makamu Mwinyi baada ya kukabidhwa dhima na amana ya kuwa Rais wa Zanzibar na dhamana hiyo wataimaliza 2030 na wanaamini jahazi hilo atalivusha salama.

Moja ya mambo ambayo ndani ya CCM hakuna lawama ni kwamba chama hakijafanya makosa katika kupata viongozi wa kuvusha taifa upande wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Katika jambo ambalo kwa upande wa Zanzibar hatujawahi kufanya makosa ni kupata mwanachama na mwanaCCM wa kumkabidhi dhamana na amana wa kuliongoza taifa hili kwa hakika Dk. Mwinyi unastahili. Mungu akupe maisha marefu utuvushe Wazanzibari kwa salama na amani na tunakuamini wewe ni nahodha jasiri sana", anasema.

Anawaomba wana CCM wenzake wasipoteze muda wa malumbano na majibizano kwani wanakazi ya kujenga chama na Zanzibar.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdullah Juma Sadala, anasema CCM ni maarufu inafahamika kwa utamaduni wake wa kupeana madaraka na kupokezana vijiti kwa salama na amani ambayo ndiyo alama ya mshikamano wa chama chao.

## UCHAGUZI UWT TAIFA:

# Mary Chatanda aeleza 'alivyopindua meza' akivuka vikwazo kama 'hupati kura yangu'

**Na Sabato Kasika**



Mwenyekiti mpya Mary Chatanda, baada ya kupindua meza kwenye uchaguzi wa UWT Taifa uliofanyika Dodoma karibuni. **PICHA: CCM**

"BAADA ya uchaguzi, baadhi ya waandishi waliandika Mary Chatanda, apindua meza kibabe. Ni kweli katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa UWT Taifa, niliibuka mshindi. Lakini lazima nikiri kwamba kuifikia na kuipindua meza haikuwa kazi rahisi."

Ndivyo anavyoeleza Mwenyekiti wa UWT Taifa, aliyechaguliwa hivi karibuni anapozungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, akielezea ushindi alioupata dhidi ya mpinzani wake mwenyekiti wa zamani Dk. Gaudensia Kabaka.

Anasema hakutarajia kushinda, kutokana na vikwazo alivyokuwa akikutana navyo wakati wa kampeni, ikiwamo kuambiwa hadharani na baadhi ya wanachama wenzake kuwa hawatampa kura, wala asijisumbue.

"Ukiwa na roho nyepesi unaweza kukata tamaa, lakini kwa kuwa mimi ni mwanasiasa, ninajua kuwa mambo kama hayo kwenye mchakato ni ya kawaida, sikukata tamaa na mwisho nimeibuka na ushindi," anasema mwenyekiti mpya.

Anafafanua kuwa katika uchaguzi huo, alikuwa anamhofia mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Dk. Kabaka, kwa maelezo kwamba mtu akiwa kwenye uongozi na yumo kwenye kinyang'aniro ni vigumu kumshinda kwa wepesi.

"Lakini imetokea, nimepindua meza na kuibuka na ushindi licha kukutana na vikwazo wakati wa kampeni, ambavyo nilivichukulia kama vya kawaida kwani kila mgombea ana kundi lake, wapambe na washabiki wanaomuunga mkono," anasema.

**ALIVYOPINDUA MEZA**

Mary mbunge wa zamani wa Korogwe Mjini, anaibuka mshindi kwa kura 527 dhidi ya mpinzani wake Dk. Gaudensia aliyepata 219, katika uchaguzi uliofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.

Ukisimamiwa na Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda anamtangaza Mary kuwa mwenyekiti mpya wa (UWT) Taifa, huku nafasi ya makamu ikichukuliwa na Zainabu Shomary. Aidha, aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, akiangushwa vibaya kwa kuambulia kura nane.

Mary anaeleza kuwa hakuwa na hofu kwa wagombea wengine wapya kama yeye bali alimhofia aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo kwa maelezo kuwa alikuwa na nyenzo zote za kumfanya ashinde.

"Kwa kuwa na mimi nilikuwa nimejipanga na nimejitoa kwa ajili ya kuwatumikia wanachama wenzangu, nimejikuta nikipindua meza kwa kuibuka na ushindi huo ambao ni wa wana UWT wote," anasema.

**KUVUNJA MAKUNDI**

Mwenyekiti huyo anasema, uchaguzi umekwisha na sasa kilichobaki ni wanachama wote wa UWT kujenga jumuiya hiyo na chama kwa kuachana na makundi na kuunganisha nguvu pamoja ndilo jambo linalotakiwa sasa .

"Wakati wa kampeni tulipokuwa tunajinadi na kuomba kura, kila aliyeshiriki uchaguzi alikuwa na watu wake, lakini kwa kuwa uchaguzi umemalizika , hatuna budi kuungana na kuwa wamoja kama ilivyo kawaida ya CCM," anasisitiza Mary.

Mary anasema kwa umoja wao wanaweza kufikia malengo waliyojiwekea, ikiwamo kuimarisha jumuiya hiyo upya kiuchumi, kisiasa na kimaendeleo, na kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu na ndiko kukwama kutimiza malengo yao.

Aidha, mwenyekiti huyo anasema, pamoja na UWT kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika nyanja za uongozi, watahamasisha uwajibikaji wenye weledi ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kwenye uongozi wake.

"Lakini pia UWT itakemea maovu kwa wanawake watakaoonyesha uzembe na kutowajibika kikamilifu wakati wa kutekeleza majukumu yao, na ikibidi tutapendekeza hatua za kuchukuliwa," anasema Mary.

> "Lakini pia UWT itakemea maovu kwa wanawake watakaoonyesha uzembe na kutowajibika kikamilifu wakati wa kutekeleza majukumu yao, na ikibidi tutapendekeza hatua za kuchukuliwa," anasema Mary.

Anaeleza kuwa chini ya uongozi wake, atachukua hatua iwapo wataona na kuthibitisha vitendo vyovyote vinavyoashiria uzembe, kukosa maadili na hujuma kwa kiongozi yeyote dhidi ya mwanamke mwenzake.

"Tupo tayari kufanya kazi kwa kushirikiana na wanachama wote wa UWT bila ubaguzi, pia tutashirikiana na watakaotoa ushirikiano kwetu, hatuna tatizo sababu hakuna uchaguzi usio na makundi," anaongeza.

**MALENGO YAKE**

Mwenyekiti huyo anasema UWT ina malengo mengi ikiwamo kusimamia uhamasishaji kwa ajili ya kupata wanachama wapya wengi zaidi, kuimarisha miradi mbalimbali ili kujiinua kiuchumi.

"Kwa miaka mitano ambayo tutaongoza jumuiya hii, tumepanga kuongeza wanachama wa UWT hasa kwa kuzingatia kwamba hii ni miongoni mwa nguzo kuu za chama chetu cha Mapinduzi," anasema.

Anaongeza kuwa jumuiya hiyo ina miradi mbalimbali ikiwamo ya majengo, mashine za kusaga na mingine midogo midogo ambayo wanakusudia kuhakikisha inaimarika kwa manufaa ya UWT na chama .

"Pamoja na hayo, tunakusudia kushirikiana na serikali na wadau wengine kwa ajili ya kupambana na vitendo vya ukatili katika jamii, kwani vimekuwa kama jambo la kawaida huku baadhi ya watu wakiumia, kupoteza maisha na hata kuathirika kwenye maisha" anasema.

Anafafanua kuwa jumuiya itashiriki kikamilifu kutoa elimu ndani, kwa njia ya mikutano ya hadhara, makongamano na semina, ili kurejesha maadili ambayo yamepotea na kusababisha vitendo vya ukatili kuongezeka.

Anasema suala la kuhimiza maadili mema si la serikali na wadau wengine bali hata UWT inahusika, na kwamba kwa kushirikiana na wadau wote wa kupinga ukatili, vitendo hivyo vinaweza kuisha ndani ya jamii.

"Tutafuata dira na mwelekeo na mipango kazi ambayo tayari ilishaandaliwa kwa mustakabali wa jumuiya, miongoni mwake ni maendeleo ya UWT lakini pia kupambana na vitendo vyote vya ukatili katika jamii," anasema.

# Mikoa vinara ukatili wanawake yaanikwa, wadau wapendekeza mbinu kuukomesha

**Na Sabato Kasika**

MAADHIMISHO ya Siku 16 za Kupinga Ukatili 2022 yamekamilika na mikoa vinara wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto, imewekwa wazi, huku ikielezwa kuwa matukio mengi yapo vijijini kuliko mijini.

Mikoa hiyo inayotajwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu LHRC Anna Henga akikariri taarifa ya Haki za Binadamu ni Arusha, Manyara, Lindi, Tanga na Temeke (mkoa wa kipolisi).

Hayo yamo katika tamko la kituo la siku 16 za uanaharakati wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, huku akisema mwaka jana Tanzania ilishuhudia kuongezeka kwa ukatili wa wanawake na watoto.

"Taarifa ya Haki za Binadamu iliripoti matukio 23, 685 ya ukatili dhidi ya wanawake kuanzia Januari hadi Desemba mwaka jana, huku kukiwa na ongezeko la matukio 2, 859," anasema Anna.

Anafafanua kuwa kuna ukatili wa kijinsia unaohusisha ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia, kiuchumi na ukatili wa kidijitali ambao nao umekuwa ukiwatesa wanawake zaidi. Katika taarifa ya haki za binadamu ukatili wa kimwili na kingono umeongoza zaidi ya ukatili mwingine.

"Ukatili wa wenza umekuwa mkubwa sehemu za vijijini kwa asilimia 53 kuliko mijini ambako ni asilimia 45. Asilimia 30 ya wasichana wanapitia ukatili wa kingono kabla ya kufika umri wa miaka 18, huku asilimia 58 ya wanawake na asilimia 40 ya wanaume wakiamini kuwa mume ana haki ya kumpiga mke kwa sababu zozote," anasema.

**MAUAJI YA WANAWAKE**

Anna anaongeza kuwa mauaji ya wanawake na wasichana yanaongezeka na si kitu kipya duniani, na kwamba vitendo hivyo vinaendelea kuwa vingi nyakati hizi.

"Mwaka huu Jeshi la Polisi liliripoti matukio 472, 544, mwaka 2018, yalikuwa 487, wakati 2019 matukio 531, mwaka 2020 matukio 554 huku yakihusisha mauaji ya wanawake kutokana na ukatili wa wenza, uchawi, imani za kishirikina, yasiyo ya wenza na mashambulio," anasema.

Anaongeza kuwa jambo la kutafakarisha zaidi, ni mauaji ya makusudi ya wanawake yanayoendelee kukabaliwa na jamii, kuvumilika na kutafutiwa sababu kiubaguzi na upendeleo.

Anataja aina ya mauaji ya makusudi ya wanawake nchini kuwa ni yale yanayotendwa na wenza wa waathirika wawe waume, wachumba, wapenzi au mtu ambaye tayari kaachana na muathirika na tukio.

"Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO), ulionyesha kuwa asilimia 35 ya mauaji ya wanawake duniani yamefanywa na wenza. Katika kulinganisha utafiti huo ilibainika kuwa ni asilimia tano tu ya mauaji ya wanaume yanayosababishwa na wenza wao," anasema.



Mateso na ukatili kama vipigo kwa wanawake na wasichana vinaongezeka na kinamama wanajiuliza wakimbilie wapi? . **PICHA: MTANDAO**

Anasema hapa nchini, mauaji ya wenza yanahusishwa na ukatili wa wenza na yameendelea kuathiri wanawake, na kufafanua kuwa taarifa ya Haki za Binadamu ya 2019/2021, iliripoti matukio zaidi ya 50 ya mauaji ya wenza.

"Katika ripoti hiyo, waathirika wanawake ni zaidi ya asilimia 95. Haya ni mauaji ya wanawake yanayoendelea kuogezeka kwa kasi nchini. Mwaka huu kumekuwa na matukio mengi ya mauaji ya wenza ikiwamo lile la Mwanza ambapo mume alimpiga mkewe risasi na yeye kujiua" anasema.

**MILA, DESTURI**

Mkurugenzi Mtendaji Anna anasema mauaji ya wanawake yanayohusiana na mila na desturi ni mauaji ya makusudi, katika kutekeleza mila na desturi fulani kwenye jamii.

"Kwa mfano ukeketaji umeendelea kuonekana mikoa ya Mara, Manyara, Arusha, Singida na Dodoma. Wasichana wengi hupoteza maisha wakati au baada ya kitendo cha ukeketaji," anasema.

Anasema ukeketaji una madhara mbalimbali ikiwamo maambukizi pamoja na kuvuja damu nyingi, na kwamba bado jamii hizo zimeendelea kushiriki vitendo hivyo vya mila zilizopitwa na wakati.

"Tujuavyo na tunavyosikia, ukeketaji sasa umeshamiri kwa miezi hii huko mkoani Mara, na tunalaani vikali kitendo cha baadhi ya wananchi kuchapisha kadi za mialiko, kwa ajili ya kusherehekea ukeketaji.

Mbali na muaji ya wanawake yanayotokana na mila na desturi, anasema yapo mengine yanayohusina na ukatili wa kingono, ambayo husababisha kifo kwa muathirika wa kitendo hicho.

"Vitendo vingi vya ukatili wa kingono humuathiri zaidi mwanamke, vinaweza kuwa vya ubakaji wa watu wengi au ubakaji wa aina nyingine yeyote. Wanawake ambao ndio waathirika wa ukatili wa kingono zaidi, hupoteza maisha kutokana na vitendo hivyo," anasema.

Anataja mauaji mengine ya wanawake kuwa ni yale yasiyo ya wenza, kwamba hutokea pale mtu asiyefahamiana na muathirika na kuwaua wanawake kwa sababu zake binafsi.

"Kwa mfano katika taarifa ya ya 2018 ya Haki za Binadamu kulikuwa na mtu mkoani Mwanza aliyewalaghai wanawake kimapenzi na kisha kuwaua. Mauaji haya yanaweza kuwa sehemu yoyote na kwa mtu yeyote japo waathirika wengi huwa wanawake," anasema.

Anasema hapa nchini mauaji hayo yameendelea kuongezeka akitolea mfano mauaji ya Mto wa Mbu Arusha ambayo wanawake ndio walikuwa waathirika zaidi, na kwama wanawake ambao ni waathirika zaid mauaji haya ni nwanafunzi, wafanya kazi katika sehemu za starehe na wanawake wanaofanya biashara ya ngono.

"Lakini kuna mauaji ya makusudi ya wanawake na visababishi vyake ni wivu hasa pale inapohusu mwenza au mtu uliyeachana naye, kulazimisha tendo la ngono, pombe na ulevi, matatizo ya akili, umaskini, ukosefu wa uwezeshaji kiuchumi kwa mwanamke," anasema.

Anaongeza kuwa uvumilivu, ukosefu wa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia, sheria, imani za kishirikina mila na desturi zilizopitwa na wakati na kutokuwa na usawa wa kijinsia, vinachangia mauaji hayo.

**MAPENDEKEZO LHRC**

Anna anapendekeza serikali kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu hali za wanawake, watoto, wasichana na haki za binadamu kwa ujumla ili kuleta mabadiliko ya tabia.

Mkuu wa Dawati la Jinsia la LHRC, Getrude Lyabene, anasema kuna haja pia ya kuboresha huduma za jamii, haki na kuhakikisha wanawake wanapata msaada pale wanapofanyiwa ukatili ikiwamo kuwa na nyumba salama na huduma za kisaikolojia.

"Tunapendekeza kutungwa sheria mahsusi ya kupinga ukatili wa kijinsia au ukatili wa majumbani kwa ajili ya usalama zaidi wa wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia na ukatili wa majumbani," anasema Getrude.

Anaongeza kuwa ni vyema kurekebisha sheria zote kandamizi kwa wanawake ambazo zinaendelea kuleta changamoto katika ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na ufurahiaji wa haki za wanawake.

Getrude anasema hatua hiyo ihusishe pia sheria ya ndoa na mirathi, huku akiongeza kuwa itungwe sheria au sera kuruhusu watoto wanaopata ujauzito kurudi shule kikamilifu, ili kukata mnyororo wa umaskini utakaoendelea kuwaweka katika hatari ya kufanyiwa ukatili.

"Hili ni pamoja na kufuta au kurekebisha sheria zote zinazomnyima mtoto wa kike haki za kufurahia haki yake ya elimu ikiwamo sheria ya ndoa, lakini pia kuhakikisha sheria zilizopo zinazomlinda mwanamke dhidi ya ukatili zinatekelezwa ipasavyo," anasema.

Anaongeza kuwa hilo linahusisha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeridhia, pia kuendelea kufanya utafiti na kukusanya taarifa kuhusu mauaji ya makusudi ya wanawake nchini.

THOMAS NGAWAIYA

# Shuhuda anayebainisha shangwe za uhuru zilivyotikisa kijijini kwao

## •Akiwa na miaka 13 hakulala alizunguka mitaani kushangilia

**Na Sabato Kasika**

SHAMRAMSHAMRA za kusherehekea Uhuru wa Tanganyika zilifanyika nchini kote mijini na vijijini, huku baadhi ya Watanganyika wakifurahia kwa kula na kunywa baada ya kusikia mkoloni ameondoka na kuwaachia nchi yao.

Japo mambo yalinoga zaidi huku mengi yakifanyika Dar es Salaam, mwanasiasa mkongwe na shuhuda wa 'uhuru day' Thomas Ngawaiya, anasema hata nyumbani kwao Singa Kibosho, mkoani Kilimanjaro mambo yalikuwa moto sawa na kusema hakuna kulala.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili anasema alikuwa kijana mwenye miaka 13 akisoma darasa la tano Kibosho Middle School, mkoani Kilimanjaro, akitamba kuwa alishuhudia kila kitu kilichofanyika kijijini kwao.

Anafafanua kuwa siku hiyo ya uhuru, walipofika shuleni asubuhi, mwalimu mkuu mwafrika Joseph Ashangali, aliwakusanya kwenye paredi akatangaza kuwa nchi imekuwa huru na kwamba wakazunguke na bendi ya shule mitaani wakiimba na kushangilia.

"Tulizunguka tukiimba nyimbo mbalimbali na kuwafanya wazazi nao wakawa wanafuatilia nyuma hadi shuleni kuuliza nini kimetokea, ndipo mwalimu mkuu akawaambia nchi iko uhuru," anasema.

Anaeleza kuwa baada ya mwalimu kuwaambia na kuwafafanulia, waliondoka na kushangilia na kwamba wapo waliokwenda kunywa na kuandaa chakula kwa ajili ya kusherehekea.

Ngawaiya mbali na kuzunguka mitaani na bendi ya shule, anaongeza kuwa siku hiyo ya uhuru, mwalimu mkuu aliamrisha wapishi kuwapikia chakula kizuri ili wale wafurahie na kusherehekea uhuru wa nchi yao.

"Chakula ambacho wanafunzi walikipenda ni buruga ambayo ni ngano iliyochanganywa na soya na kupika kama ugali , kwani kilikuwa kitamu sana, kwa wiki tulikuwa tunakula mara moja, siku hiyo ya uhuru haikuwa ya buruga, lakini mwalimu akaamuru tupikiwe," anasema.

Anafafanua kuwa aliporudi nyumbani, alikuta wazazi nao wameandaa mlo wa nguvu ambao ulikuwa ni wali kwa nyama, na kwamba kawaida walikuwa wakila wali mara moja kwa mwaka hasa wakati wa sikukuu ya Krismasi na Pasaka.

"Lakini siku hiyo ya Desemba 9, wazazi walibadili utaratibu na kupika ubwabwa tukala tukafurahia sikukuu hii kuu ambayo kwa kweli ni kumbukumbu nzuri ya kutoka kwenye makucha ya mkoloni," anasema.

Ngawaiya anaeleza kuwa miongoni mwa matukio ambayo anaendelea kuyakumbuka wakati nchi inapata uhuru, ni mlo wa shuleni na nyumbani, ambao uliandaliwa rasmi kusherehekea nchi kuwa huru.



Thomas Ngawaiya

### AMFAHAMU NYERERE

Anasema mara baada ya nchi kupata uhuru, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alikuwa akitembelea mkoa wa Kilimanjaro mara kwa mara, na kwamba alifika hadi shuleni kwao na kusababisha wapigane vikumbo kwa lengo la kutaka kumuona.

"Nakumbuka alipofika shuleni alisaini cheki, sikumbuki ya shilingi ngapi, ila tulishuhudia tukio katika paredi, huku tukipigana vikumbo, ili kuhakikisha kila mmoja anamuona Waziri Mkuu wa Tanganyika Julius Nyerere," anasema.

Ngawaiya anakumbuka kuwa awali walidhani kuwa Nyerere ni 'pande la mtu' mwenye maguvu lililopigana na mkoloni na kufanikiwa kumwondoa nchini, lakini walipomwona walijua ni wa kawaida kama wengine.

"Vikumbo vyote kwenye paredi vilikuwa ni kutaka kumuona huyo aliyesababisha Tanganyika ikapata uhuru ni mtu wa aina gani," anasema.

Anaongeza kuwa tukio hilo la kumshangaa Nyerere halikuwa kwao tu bali hata wazazi wao nao walijitokeza kwa wingi wengine wakawa wamepanda juu ya miti, ili kumuona aliyeweza kumfukuza mkoloni.

Anafafanua kuwa wengi wao walidhani Nyerere jitu la miraba minne linaloweza kumkamata mtu na kumharibu kwa sekunde chache, na kumbe walichokuwa wakidhani sicho.

"Yaani kwa ujumla, tukio la kupata uhuru lilikuwa na mvuto wa aina yake kijijini kwetu na pia ujio wa Nyerere shuleni kwetu pia ulisababisha kuwapo kwa umati mkubwa wa watu," anasema.

Ngawaiya anasema, ujio wa Nyerere shuleni kwao ulifanyika miezi mitatu tu baada ya nchi kupata uhuru, na kwamba watu walikuwa na shauku kubwa ya kumuona aliyesababisha wawe huru.

"Lakini pia miaka 13 baada ya uhuru, vilianzishwa vijiji vya ujamaa kwenye mikoa mbalimbali nchini kwa lengo la kuwaleta wananchi pamoja, ili wajiletee maendeleo wakiwa pamoja," anasema.

Anafafanua kuwa, mkoa wa Kilimanjaro hasa maeneo ya Wachaga vijiji vya ujamaa vilianza kabla ya opereshени ya mwaka 1974, kwa maelezo kwamba walikuwa wajamaa tangu muda mrefu.

"Nyerere hakuhangaika na kwetu kwani alikuta tayari tunaishi katika vijiji vya ujamaa ambavyo alikuwa akivitamani kwa lengo la kurahisisha shughuli za maendeleo kwa wananchi," anasema.

### UHURU NA KAZI

Ngawaiya anasema baada ya nchi kupata uhuru, Nyerere alihimiza suala la uhuru na kazi, kwa maana kwamba watu wafanye kazi kwa juhudi ili wajiletee maendeleo badala ya kubweteka tu kwa kuwa wako huru.

"Kaulimbiu ya Uhuru na Kazi ilikuwa inalenga hilo, kwamba watu wako huru na sasa wachape kazi kwa ajili ya kujiletea maendeleo na pia kuinua uchumi wao na wa nchi yao," anasema.

Anafafanua kuwa kaulimbiu hiyo inaendelea kutumiwa na viongozi waliopo sasa, lengo likiwa ni kuhakikisha taifa huru la Tanzania linazidi kupiga hatua kwenda mbele.

"Kwa mfano Rais Samia Suluhu Hassan amefuta maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru na kuagiza Shilingi milioni 960 ambazo zingetumika katika sherehe zielekezwe kujenga mabweni ya shule za wahitaji," anasema.

Anasema sasa pesa zitakwenda kuboresha miundombinu ya shule ikiwamo ujenzi wa mabweni, na kwamba hatua hiyo ni mwendelezo wa kaulimbiu ya uhuru na kazi.

Anaongeza kuwa nchi ilishapata uhuru, na sasa kinachoendelea ni kazi tu kama ambavyo Rais mwenyewe amekuwa akisema kuwa kazi iendelee, na kwamba kufuta sherehe ni jambo la kawaida.

"Sisi ambao tunajihusisha na masuala ya utawala bora, tunaona Rais amefanya jambo jema linalohusiana na uhuru na kazi, ili kuharakisha maendeleo ya nchi yetu," anasema.

# M23 waendelea kupoa ni baada ya Marekani kuiwakia Rwanda

## •Msemaji wao atubu kuahidi wataacha vita



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Anthony Blinken, akionyesha msimamo wa kupinga uwepo wa M23 DRC..
**PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

WAASI wa M23 wamekubali kuondoka DRC baada ya shinikizo la Marekani dhidi ya Rwanda inayodaiwa kuwa inahusika na kuwawezesha, linaripoti gazeti la The Brussels Times la Ubelgiji.

Wiki iliyopita waasi hao wanaripotiwa kukubali kuondoka mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kusema kwamba wanaunga mkono juhudi zozote za kikanda za kuleta amani.

Maamuzi hayo yanakuja baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, kuongeza shinikizo kwa serikali ya Rwanda kuondoa madai yake ya kuwaunga mkono waasi.

Waasi hao wanaoaminika kuwa ni kundi la wakala wa Rwanda, linatuhumiwa kusababisha vifo vya mamia ya raia, Marekani ikiongeza shinikizo la kidiplomasia kwa Rwanda.

Juhudi ambazo zinaweza kuwa zimechangia moja kwa moja au kwa kiasi zinatokana na tangazo la Alhamisi iliyopita la msemaji wa M23 kwamba waunga mkono juhudi za kikanda za kuleta amani ya muda mrefu DRC," huku pia wakiomba mkutano na msuluhishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mpatanishi, Uhuru Kenyatta.

Akiongea kwa simu Blinken anaitaka serikali ya Rwanda kusitisha msaada wowote wa nje kwa makundi yasiyo ya kiserikali yenye silaha nchini DRC, ikiwa ni pamoja na usaidizi wa Rwanda kwa M23.

Waziri Blinken anaeleza kuunga mkono kwa dhati upatanishi wa kikanda na mazungumzo yanayoongozwa na Angola na EAC na kuonyesha "wasiwasi mkubwa juu ya athari za mapigano kwa raia wa Congo ambao wameuawa, kujeruhiwa na kufukuzwa kutoka kwa makazi yao," taarifa hiyo inasema.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda Vincent Biruta, akijibu simu hiyo kwenye Twitter, anasema "tofauti katika uelewa wa suala hilo bado zipo, na mtazamo mbaya na potofu wa jumuiya ya kimataifa unaendelea kuzidisha tatizo." Kwa mara nyingine, Biruta anakanusha madai kwamba

> Akiongea kwa simu Blinken anaitaka serikali ya Rwanda kusitisha msaada wowote wa nje kwa makundi yasiyo ya kiserikali yenye silaha nchini DRC, ikiwa ni pamoja na usaidizi wa Rwanda kwa M23.

Rwanda inawasaidia waasi hao.

Lakini licha ya wapiganaji wa waasi wa Machi 23 maarufu M23 kukubali kujiondoa katika maeneo wanayokalia kwa mabavu mashariki mwa DRC na kuahidi kuendelea na mazungumzo ya amani, kama ilivyokubaliwa katika muafaka wa mikutano ya usuluhishi ya kilele iliyofanyika Luanda kati ya Wakongo na mamlaka ya Rwanda, nchi inayotuhumiwa kufadhili uasi, vita inarindima.

Cha kushangaza ni mapigano kuripotiwa kuwa yanapamba moto hasa wiki iliyopita.Kundi hilo lenye silaha, ambalo halikuwepo katika mazungumzo ya hivi karibuni ya kupata suluhu ya mgogoro wa mashariki ya DRC limeomba kukutana na wapatanishi wa kikanda wanaofanya juhudi za kumaliza mzozo huo.

Waasi hao wanasema wako tayari kuondoka katika eneo linalokaliwa kwa mabavu mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na litaunga mkono juhudi za kikanda za kuleta amani licha ya kutowakilishwa katika mazungumzo ya kusaka amani, lakini wanashambulia raia.

Genge hilo linaloongozwa na Watutsi lenye silaha ambalo linaonekana kuwa ni mawakala wa Rwanda wanaoungwa mkono na nchi hiyo, madai ambayo Rais wa Rwanda Paul Kagame, anayakanusha linasema, liko tayari kuanza kujitenga na kujiondoa kwenye vita.

Taarifa ya msemaji wa M23 Lawrence Kanyuka, ya wiki iliyopita inatoa hakikisho hilo, lakini bado hali si shwari.

Anasema M23 inaunga mkono juhudi za kikanda za kuleta amani ya kudumu nchini DRC na Kanyuka anasema, pia akithibitisha dhamira ya kundi hilo katika makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyofikiwa na viongozi wa Angola mwezi uliopita.

Waasi hao wanaoongoza mashambulizi mashariki mwa DRC na ambayo viongozi wa Kinshasa wanawaelezea kuwa ni vuguvugu la "kigaidi", hapo awali walijinasibu kuwa hawawezi kushirikiana wala kuwa sehemu ya hatua zilizokubaliwa katika mazungumzo ya kutafuta amani ambayo wanadai walitengwa.

Jumanne iliyopita Kanyuka pia alipendekeza kukutana na kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kikanda ili kujadili mikakati mbalimbali na akarudia ombi lake la kukutana na mpatanishi wa mgogoro wa DRC rais wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta,

Kenyatta akiwakutanisha waasi hao kwenye duru ya hivi karibuni kwenye mazungumzo ya amani yenye lengo la kumaliza mzozo huo, ambao yalikamilika nchini Kenya Jumanne iliyopita.

Wawakilishi wa takriban vikundi 50 vilivyojihami vilivyo katika eneo lenye hali tete, lenye utajiri wa madini mashariki mwa DRC walihudhuria, lakini M23 haikuwepo. Kundi la waasi lilitengwa baada ya kushindwa kujiondoa na kupokonya silaha kwa muda wa mwisho wa kusitisha mapigano.

Jumanne iliyopita jijini Nairobi makundi mengine yenye silaha yalikuwepo kwenye mazungumzo hayo ya amani na kulaani uwepo wa wapiganaji wanaoungwa mkono na mataifa ya kigeni nchini DRC, ambao wanaongeza tatizo la uasi kuwa kubwa.

Kwa miongo kadhaa, nchi jirani za Uganda na Rwanda zimepata faida kubwa kutokana na madini ya DRC ni madai yanayotolewa na wachunguzi na wafuatiliaji mbalimbali.

Waasi wanaongeza kuwa tatizo la makundi ya kigeni yenye silaha na yanayoungwa mkono na mataifa makubwa kama halitatatuliwa, na kama jeshi la Kongo halitaweza kulinda nchi hakuna njia wapiganaji hao wataweka chini silaha zao.

Kenyatta alirejea hisia hizo akisema "Tatizo ni makundi ya kigeni yanayojihusisha na Kongo kuacha uharibifu," anasema katika mazungumzo hayo, akiongeza kwamba waasi hao wanapaswa "kuiacha Congo kwa amani."

M23 ilianza kujulikana miaka 10 iliyopita ilipoiteka Goma, kabla ya kufurumushwa mwaka 2013. Lakini imekuwa ikifufuka kila mwaka na safari hii ikifanya makosa kadhaa na kupata nguvu licha ya kushinikizwa na vikosi vya Congo na vya kikanda pamoja na Umoja wa Mataifa kuondoka.

***AL JAZEERA NEWS/ BRUSSELS TIMES***

JUKWAA LA VIONGOZI

ALI HASSAN MWINYI+ UHURU 61

# Anabakia bingwa kutibu uchumi uliokuwa ‘ICU’

## •Mwasisi uliberali Vs ujamaa, ubinafsishaji

**Na Gaudensia Mngumi**



MIAKA 61 ya Uhuru inayoadhimishwa Desemba 9, ni wasaa mwingine wa kutazama mambo mengi Tanzania inayojivunia. Mojawapo ni ushujaa na ushupavu wa viongozi wake, kila mmoja akifanyakazi inayoacha alama kwa taifa.

Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, akizaliwa Mei 8, 1925 ni ‘Baba wa Taifa’ anayechukua kijiti miaka 24 baada ya uhuru, kutoka kwa mwasisi Julius Nyerere. Ni wazi kuwa wiki iliyopita maadhimisho ya miaka 61, alitafakari mengi.

Kama mpigania uhuru , raisi na jenzi wa Tanzania ya leo, Nipashe inampandisha Mwinyi jukwaani kuangazia jinsi alivyojitoa kulitumikia taifa akichukua uongozi kuanzia 1985 hadi 1995.

Azimio la Arusha, lilianzisha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea rasmi mwaka 1967. Lilipoanza lilionekana kama upanuzi wa nafasi ya kiuchumi na serikali na chama tawala-TANU kumiliki uchumi. Sheria ya utaifishaji viwanda na uwekezaji wote ilifuata, vyote vikatoka mikononi mwa sekta binafsi na kuhodhiwa na serikali .

Aidha, usambazaji wa bidhaa nao ulikuwa ukifanywa na serikali kupitia miundombinu ya usambazaji. Hata hivyo udhibiti wa uchumi haukuongeza uzalishaji au ufanisi kwenye sekta ya viwanda badala yake, ulitegemea zaidi ruzuku, misaada na ulifanyika bila kulenga faida na kufikia miaka ya 1970 kuelekea 1980 hali ilikuwa ngumu, taifa likikosa bidhaa na huduma muhimu.

Uhaba ulikuwa mkali na mdororo wa kiuchumi wa miaka ya 1980 ulitikisa mno. Kampuni za Biashara za Mikoa (RTCs) na maduka ya ushirika ndicho kilikuwa chanzo pekee cha bidhaa kuanzia vyakula, sukari, vifaa vya ujenzi, redio na betri pia.

Ugavi ulidhibitiwa na kila bidhaa ikawa adimu , wafanyakazi wa RTC na maduka ya ushirika wakawa na nguvu sana na ‘wapigaji wakuu,’wateja walalahoi wakakosa huduma lakini wenye pesa waliwapa hongo na kupewa upendeleo na huo ukawa mwanzo wa wafanyakazi hao kuwa mabilionea.

Hata hivyo, kupungua kwa fedha wahisani na misaada ya wafadhili katika miaka ya 1980 kuondoka, vita vya Uganda, mtikisiko wa uchumi duniani, kuongezeka mzozo kati ya Benki ya Dunia na IMF kuhusu sera za marekebisho ya uchumi kuliongezeka yote yakakoleza matatizo makubwa ya uchumi.

Licha ya uchumi kudhibitiwa na serikali, ulishuka, mfumuko wa bei ukikaribia asilimia 25,uchumi usio rasmi ukapanda, magendo, usafirishaji haramu biashara kama kahawa, ulikuwa umekithiri mipakani. Mwishowe, hali akizidi kuwa mbaya na umaskini ukakithiri.

Ufisadi ukazidi kuimarika, mashirika ya umma kuyumba, kila kitu kwenda mchomo na ilipofika 1985, Rais Julius Nyerere, aliona hana cha kufanya bali kung’atuka .

### MWINYI NA UKOMBOZI

Nyerere aliachia ngazi lakini kiuchumi nanga ilikuwa imepaa, anamwachia Rais Ali Hassan Mwinyi, jukumu la kuusukuma na kuuinua tena uchumi, akianza na mipango ya marekebisho kwa kufikia makubaliano na IMF na Benki ya Dunia maarufu taasisi za Bretton Woods.

Lengo ni kupambana na ufisadi wa mali za umma, lakini pia kuwa na uchumi wa soko huria au uliberali mamboleo, kupunguza ukubwa wa serikali yenye mawaziri kibao na manaibu, kudhibiti mfumuko wa bei, kuondoa serikali kwenye kuendesha uchumi kama kumiliki viwanda, kampuni, shule, magari na kuachia kazi hizo kwa sekta binafsi.

Haikuwa kazi nyepesi kwa Rais huenda Mwinyi hakulala akifanyakazi usiku na mchana. Nchi ilikuwa taabani hata unga ulikuwa taabu, ukinunua viatu sokoni unapewa vya mguu mmoja, hata ndala hazikupatikana.

### MAAMUZI MAGUMU

Rais Mwinyi anafanya maamuzi magumu. Ni kama nahodha aliyezama maji kina kirefu, mawimbi makali,miamba, papa na dhoruba na kuendesha chombo.

Anaamua kudhibiti na kujenga tena pamoja na kukuza uchumi uliokuwa taabani. Bila fedha wala akiba.Wakati mwingine alikuwa akitangaza bajeti mara mbili Juni na Desemba.

Kwanza anaubadilisha kutoka uchumi hodhi kuwa huria au wa uliberali. Anafanikwa uchumi ukianza kidogo kuimarika. Licha ya serikali yake kuwa na mzigo mkubwa wa madeni mfano kwenye shule za sekondari, magereza, taasisi za elimu, madeni ya umeme na maji lakini pia kudaiwa na taasisi za kimataifa, alipambana.

Ikumbukwe hata serikalini hakukuwa na hali bora. Watumishi wa umma ofisi zao zilikuwa taabani, nyingine hazikuwa na maji na huduma nyingi zilidora. Mishahara ilikuwa kiduchu bila marupurupu, hata pensheni za wastaafu wa umma zilikuwa ndogo mno na kazi kuzipata.

Pengine Rais Mwinyi, alibeba jambo ‘lisilowezekana’ au kulazimika kuunda vyuma ‘vilivyoliwa na kutu’.Hata mitizamo ya viongozi wa umma, wahadhiri vyuo vikuu na umma wote ulimshangaa mtizamo wake katika kuisuka upya Tanzania iliyoonekana kuwa ya kibeberu. Bila kujali lawama nyingi zilizokuwa zikitolewa dhidi yake, alipambana.

Serikali yake haikuepuka tuhuma za rushwa. Wakati wote misemo kama ‘nchi imeuzwa’ ‘ruksa’, chukua chako mapema ilitamalaki. Aidha,malalamiko kuwa mshahara hauitoshi wala hakuna kipato cha kugharamia riziki ya kila siku na wimbo wa hali ngumu ulisikika kila mahali.

Rais Mwinyi, alifanya maamuzi magumu pia kwenye nishati mwaka 1993 mgawo wa umeme ulipiga hodi na shida ya kukatwa na kukatika ikazaliwa rasmi. Hakukaa kimya aliishughulikia hata kualika wawekezaji kuzalisha umeme binafsi, ukiwa ujio wa kampuni ya IPTL ya Malaysia.

Baada ya Mwinyi kujenga tena ukuta uliobomoka, kurekebisha karibu vitu vingi na kuweka utaratibu mpya wa mtiririko wa uchumi na kulegeza masharti, aliigusa Sheria ya Fedha na Uchumi, nyingine ni ya Benki ya 1992 ili kuruhusu kuanzishwa maduka ya fedha, benki za kigeni kam Meridian BIAO na Greenland Bank ya Uganda zikatua nchini.

Alianzisha ubinafsiaji mwaka 1995 kampuni ya RJ Reynolds ikinunua asilimia 51 ya hisa za Kampuni ya Sigara -TCC, kadhalika mwaka 1993 Tanzania iliingia ubia na Kampuni ya Bia ya Afrika Kusini (SABMiller) kuendesha kampuni ya bia-TBL.

Hakuishia hapo anasimamia mageuzi kiuchumi na kisiasa pia akifanikisha kuwepo sera na sheria ya vyama vingi 1993 na kufanikisha uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1995.

### MSINGI KWA MKAPA

Rais Benjamin Mkapa, anaingia madarakani kwenye uchaguzi wa 1995 ulioshirikisha vyama vingi. Akifanyakazi akianzia kuimarisha na kusimamia misingi aliyoiweka Rais Mwinyi na awamu ya pili.

Anaanza kurejesha imani ya mataifa ya nje na kuyashirikisha kwenye kujenga uchumi wake kwa kuvutia uwekezaji mpya wa moja kwa moja kutoka nje (direct foreign investments).

Anasimamia juhudi mpya za kupunguza deni la Tanzania baada ya kutekeleza masharti na mipango kadhaa iliyoandaliwa na awamu ya Mzee Mwinyi na Desemba 2001 wahisani wanaifutia Tanzania deni la Dola za Marekani bilioni 3.

Ukuaji wa kweli wa uchumi ukaanza kukua kuanzia asilimia tatu hadi nne kwa mwaka ukiwa ni mwendelezo wa kupunguza mfumuko wa bei, kuongeza uzalishaji, kusimamia kodi bila kusahau kuboresha sekta ya utumishi wa umma na uwajibikaji.

Ukuaji huo wa uchumi ukafanikisha utekelezaji wa baadhi ya hatua za muda mfupi na mrefu ili kupunguza hali mbaya na mdororo wa uchumi lakini pia kupambana na vichocheo vya rushwa na kujenga sekta ya umma imara.

# Kura katika NEC-CCM kielelezo cha mambo, uchaguzi unaokuja

INATOKA UK. 13

uongozi utakuwepo wakati purukushani ya kumpata mgombea wa 2030 itakapoanza.

Wenye ndoto hizo watakuwa wameingia katika 'kipimajoto' cha kugombea ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa na ujumbe huo ni muhumi kwani ni kujipanga upya.

Ukiangalia au kusikiliza orodha ya nani waliopata kura nyingi zaidi katika ujumbe wa NEC jijini Dodoma wiki iliyopita unapata kielelezo cha haraka 'mtiania' anaweza kuungwa mkono kiasi gani, na kama uungwaji mkono hautoshi, aongeze raslimali au abwage manyanga.

Isitoshe, watiania wakuu hawakuwa katika kinyang'anyiro hicho, ila unaweza kuangalia kuungwa mkono kwa wapambe wao ukapata picha nani mtiania ambaye labda anapendwa zaidi CCM.

Kwa mfano Joseph Kasheku 'Msukuma' akipata kura nyingi kwa NEC anabeba bendera ya nani, au Stephen Wassira anaporudi tena analeta ujumbe gani?



Kutafuta undani wa maswali hayo inabidi kusikiliza minong'ono ya shughuli za wale wanaoitwa 'wapambe' katika siasa ambayo kimsingi ina maana ya wasaidizi wa karibu, au 'machawa' kwa wanamuziki au waigizaji.

Katika mandhari ya siasa inaelekea kuaminika kuwa kuna kasi wanafanya, iwe ni 'kumpamba' mtu kwa maana ya kumsemea mema, ambayo ni dhaifu, ila ni kumpamba kwa maana ya kuwepo naye wakati wote, kama kuongezea uwepo wake mwenyewe. Mtawanyiko wa kura hizo unaashiria kitu fulani, na mojawapo ni kuwa waliokuwa karibu zaidi na mwenyekiti wa awamu ya tano walipata kura nyingi zaidi kuliko wapambe wa wazi wa hivi leo.

Kuna vielelezo vingine vya 'mfumo wa mfumo wa fahamu wa CCM' ambao unaweza kuangaliwa ni kwa njia gani ulijitokeza na ulidhihirisha nini, yaani kwa maeneo ya kura za ndiyo na hapana.

Ujumla wake au kura kuharibika siyo muhimu ila udiriki wa kura ya 'hapana,' na kama unajitokeza au labda unapangwa. Kura za Makamu Mwenyekiti Bara za hapana zilikuwa tatu, Makamu Mwenyekiti Zanzibar zikawa mbili na Mwenyekiti Taifa ikawa kura moja.

Wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi miaka mitano iliyopita, hapakuwa na kura ya 'hapana' kuelekea kwa mgombea uenyekiti taifa, hali ambayo haionyeshi udiriki, ila upenyo kihisia.

Uwepo wa kura moja au zaidi za hapana ni kielelezo kuwa chama kinakiri kuwa wapo wasioridhika na uongozi wa juu wa chama, nao wanawakilishwa pia katika hadhara hiyo.


Watu wanafarijika pale walio madarakani wanapokiri, au kuhakikisha kuwa ipo ishara, kuwa wapo wanaowapinga, ila wanakiri kwa kiasi kidogo sana kuwezesha hisia kuwa wanaweza kukabiliana na upinzani katika uchaguzi huru na wa haki. Ukiwauliza watakwambia 'Roma haikujengwa kwa siku moja,' demokrasia itajengwa hatua kwa hatua, na pia 'chururu si ndondondo.'

## CHEMSHABONGO NA -00 30 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Sayari tunayoishi
5. mfuasi wa chama
6. jambo la maana
9. fuatisha matendo ya mwingine
11.mkate mdogo wa kukaangwa kwa mafuta 12.kanya
14.nchi kubwa duniani
16.desturi
17.upungufu wa kitu
19.chama kikubwa cha Upinzani Angola 21.kipaumbele


Chini:
1. hafifu
2. neno la kuuliza
3. eneza habari
4. tandaza kitu kama nguo
7. weka pembeni chombo cha usafiri
8. haribika na kutoa harufu
10.kuwa wa kwanza kufanya jambo 12. ruhusu kitu au mtu atende jambo 13.Soni
15.neno la kuuliza
18.alika mtu kwako 20.labda



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

NAJISI
ADAMU
NANASI
ADABU
IMARISHA
IBARA
KATAA
TAPANYA
MSIBA
OANA
AGANA
SHABANI
UHAI
ABRA
MATAA

BAA
PUA
NOA
NANI
JANA
SUSA
AINA
SAA
UBAYA
KATA




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | A | M | A | | S | O | M | A |
| A | D | A | N | A | | | B | |
| T | A | K | A | T | A | | A | |
| A | B | U | | H | I | M | O | |
| | U | N | G | A | N | A | | |
| | | D | A | R | A | S | A | |
| U | L | I | M | I | | A | | K |
| | O | | B | | D | A | K | A |
| A | M | B | I | W | A | | | K |
| | E | | A | | I | B | U | A |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | I | K | I | O | | R | A | I |
| O | M | A | N | I | | I | | R |
| K | A | M | I | L | I | S | H | A |
| O | N | A | | I | B | A | | N |
| | I | T | A | | A | L | A | |
| S | | A | | A | D | A | B | U |
| H | | | U | F | A | | I | |
| A | | U | | Y | | A | R | I |
| T | A | M | B | A | A | | I | |
| I | | A | | | U | Z | A | O |





# Hospitali ya Kanda yaanza kudhibiti vifo vya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, imeanza mikakati maalumu ya kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa kuanza kutoa mafunzo kwa wauguzi wa baadhi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Hospitali hiyo imeanza kutoa mafunzo hayo kwa wauguzi wa mikoa ya Mbeya na Songwe kwa kuwapatia mbinu za kuwahudumia watoto wachanga wakiwamo wale wanaozaliwa na matatizo.

Daktari Bingwa wa Watoto kutoka hospitali hiyo, Dk. Rehema Marando alisema takwimu zinaonesha vifo vya watoto wachanga ni karibu asilimia 47 kati ya watoto wote walio chini ya miaka mitano.

Alisema mafunzo waliyoyatoa kwa wataalamu hao yanalenga kukabiliana na tatizo hilo kwa kupunguza takwimu za vifo hivyo hasa kuhakikisha kundi hilo linapata huduma sahihi.

"Takwimu ambazo zipo Tanzania zinaonyesha kati ya vizazi hai 1,000, watoto 20 wanafariki, kwa hiyo tumeona tuna kila sababu ya kujengeana uwezo ili kupunguza vifo hivi," alisema Dk. Rehema na kuongeza:

"Kati ya hawa wataalamu kuna ambao wako kwenye vitengo wanafanya kazi na tunataka wapate vitu vipya na kwa ambao hawana mafunzo hayo nao waweze kujua ili kuboresha utoaji wa huduma kwa kundi hili," aliongeza.

Mkuu wa Idara ya Watoto katika hospitali hiyo, Dk. Nuru Mlimu, alisema vipo vifo vya watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika ikiwa wahudumu wa afya watatumia vema ujuzi walionao na kuwataka wauguzi hao kuwa sehemu ya watakaosaidia kuzuia vifo hivyo.

Baadhi ya wahudumu wa afya na madaktari waliopatiwa mafunzo hayo, walisema yatawasaidia kuongeza ujuzi wa namna ya kuwahudumia watoto wachanga.

Mmoja wa wataalamu hao, Hamza Yunge, alisema ili kuhakikisha wataalamu wanaokoa maisha ya watoto wanakuwa wengi, watahakikisha wanawafundisha na wenzao ambao hawakupata nafasi ya kushiriki.

Alisema kwenye mafunzo hayo walipata mbinu mpya ambazo hapo awali hawakuwa nazo na kwamba baadhi ya mbinu walikuwa nazo lakini kupitia mafunzo hayo wamekumbushwa

Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. France Rutwashoba, aliwataka wahudumu hao wa afya kwenda kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao.

Alisema serikali imewaamini na ndiyo maana imewaajiri na kuwapatia mafunzo ya kuwaongezea uwezo hasa katika kuokoa maisha ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

"Kwenye kituo chako utakaporudi tafadhari tuone mabadiliko ya kupungua kwa vifo ama ikiwezekana kuviondoa kabisa, badilisha mtazamo wako namna ya kumhudumia mtoto hivyo vyote tunavyoweza kuvifanyia kazi kwa muda mfupi twende tuanze kuvifanyia kazi," alisema Dk. Rutwashoba.

# Polisi mguu sawa kuzuia uhalifu wakati wa sikukuu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeanza maandalizi ya kukabiliana na uhalifu wakati wa Sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya kwa kuwataka wananchi kutoa taarifa wanapobaini wahalifu ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uhalifu wao.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu namna Jeshi la Polisi mkoani Mbeya lilivyojipanga kuelekeza katika sikukuu hizo.

**Watakuwapo askari wenye sare na ambao watakuwa wamevalia kiraia ili kudhibiti matukio ya aina yoyote yatakayotokea kwenye makazi ya wananchi.**

Kamanda Kuzaga aliwataka wananchi kutokuwa na hofu ya kutendeka uhalifu wa aina yoyote ndani ya mkoa huo kwa maelezo kuwa jeshi lake limejipanga kudhibiti wahuni wote.

Alisema ili kufanikisha jambo hilo wananchi wanatakiwa kushirikiana kwa kila namna na jeshi hilo kwa kutoa taarifa za mapema kwa jeshi hilo ama kwa viongozi wa serikali.

Kamanda Kuzaga alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakishindwa kuripoti matukio ya uhalifu yanapotokea kwa kuhofia kutambulika na wahalifu hao, hivyo akawahakikishia kuwa taarifa hizo zitakuwa za siri.

Aidha alisema wakati wa sikukuu hizo jeshi hilo litafanya doria katika maeneo yote ya mkoa ili kubaini matukio ya uhalifu ambayo yatajitokeza.

Alisema watakuwapo askari wenye sare na ambao watakuwa wamevalia kiraia ili kudhibiti matukio ya aina yoyote yatakayotokea kwenye makazi ya wananchi.

Hivyo aliwatahadharisha watu wote wanaopanga kufanya matukio ya uhalifu kuacha mara moja kwa maelezo kuwa jeshi hilo limejipanga kuwashughulikia.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na baadhi ya wananchi kwenye moja ya maghala ya kusambazia mbolea za ruzuku jijini Mbeya juzi mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Spika wa Bunge akerwa upatikanaji mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amekerwa na utaratibu wa baadhi ya mawakala wa mbolea kupeleka mbolea za aina moja kwa wasambazaji hali inayowafanya wakulima kutopata baadhi ya mbolea hizo kwa wakati.

Juzi Dk. Tulia alifanya ziara ya kukagua hali ya usambazaji wa mbolea kwa wakulima katika maduka yanayouza mbolea za ruzuku na kubaini baadhi yakiwa na aina moja pekee ya mbolea, huku wakulima wakihitaji kupata aina zote za mbolea.

Akiwa Uyole Dk. Tulia alibaini baadhi ya maduka yakiwa na mbolea za kupandia pekee, kwamba baadhi ya wakulima walisema huwa wanalazimika kwenda kwenye maeneo mengine kutafuta mbolea za kukuzia.

Dk. Tulia alisema kitendo cha wakulima kupata mbolea kwenye maeneo tofauti kinasababisha kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na hivyo kufanya ruzuku ya serikali kuanza kukosa maana.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Tulia alimpigia simu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa utaratibu wa kusambaza mbolea.

"Maeneo mengine tulikopita kuna mbolea za aina zote lakini hapa ni eneo la pili tunakuta aina moja ya mbolea, sasa hapa lazima tumuulize Waziri wa Kilimo ambaye ndiye anasimamia usambazaji wa pembejeo hizi," alisema Dk. Tulia.

Baada ya maelezo hayo alimpigia simu Waziri Bashe ambaye aliagiza Wakala Mkuu ambaye anasambaza mbolea kwa mawakala wenye aina moja ya mbolea kuwasiliana na kampuni zingine ili yapeleke mbolea kwa wasambazaji hao.

Waziri Bashe alisema ataendelea kufuatilia hali ya usambazaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima kwa kuhakikisha zinapatikana kwa wakati na wakulima wanauziwa kwa bei elekezi.

Pia aliwataka mawakala wa usambazaji wa mbolea kuhakikisha mbolea zinawafikia wakulima kwa wakati na kuepuka kufanya vitu ambavyo ni tofauti na makubaliano ya mikataba waliyoingia na serikali.

Baadhi ya wakulima walisema hali ya upatikanaji wa mbolea katika maeneo yao siyo ya uhakika na hivyo wakaiomba serikali kulishughulikia tatizo hilo mapema ili waendane na msimu wa kilimo.

Mmoja wa wananchi hao, Geofrey Mwaigaga, alisema asilimia kubwa kwenye maeneo yao wanapata mbolea ya kupandia lakini ya kukuzia haipatikani jambo ambalo linawapa wakati mgumu.

Alisema serikali imefanya jambo jema kuweka ruzuku kwenye pembejeo hizo lakini kwenye upatikanaji wake ndiyo tatizo ambalo linakwamisha jitihada zao za kuongeza uzalishaji.



HABARI DODOMA

# RC abaini utapeli uuzwaji viwanja chanzo cha maji

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amebaini baadhi ya wananchi wameanza kuuziana viwanja kwenye chanzo kikuu cha maji eneo la Makutupora, ambalo walihamishwa miaka ya nyuma.

Senyamule aliyasema hayo jana wakati wa mkutano kati yake na viongozi wa Mamlaka ya Bonde la Wami Ruvu, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) pamoja na wadau wengine uliofanyika jijini hapo.

"Kuna baadhi ya watu wameanza kuvamia eneo hili la Bonde la Makutupora lililohifadhiwa kwa sababu ni chanzo kikuu cha maji kwa Jiji letu la Dodoma nawaonya tutawachukulia hatua za kisheria waondoke haraka, tumebaini wananchi waliohamishwa miaka ya nyuma ndio wanaowauzia wageni maeneo katika chanzo hiki," alisema.

Alisema kikao hicho kimetoa maazimio ya kuwaondoa haraka watu hao ili kulinda chanzo hicho cha maji.

**Kwa kushirikiana na Kambi ya JKT Makutupora walifanikiwa kuwaondoa wachimbaji mchanga waliokuwa wakifanyakazi hizo kwenye bonde hilo.**

"Serikali iliwahamisha wananchi waliokuwa wanaishi jirani na chanzo hicho kwa lengo la kulinda maji yanayozalishwa kwenye eneo hilo, eneo la ekari 348 lilifanyiwa fidia kwa wananchi waliondolewa lakini kuna baadhi waliofidiwa wameanza kuwauzia wageni viwanja kinyume cha sheria,"alisema.

Aidha, alisema kuna eneo la ekari 255 litaanza kutunzwa kwa kupandwa miti na baada ya hapo watashirikiana na mamlaka ya bonde hilo na uongozi wa jeshi ili kuimarisha ulinzi kwa wavamizi wa eneo hilo.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema bonde hilo linazalisha maji asilimia 90 yanayozalishwa na mamlaka hiyo.

Joseph alisema DUWASA wataendelea kutoa ushirikiano kwa uongozi wa Bonde la Wami Ruvu ili kuhakikisha chanzo hicho cha maji kinalindwa kwa nguvu zote kwa ajili ya kulinda afya za watumiaji wa maji hayo.

Alifafanua kuwa kuna wageni wasiojua mipaka ya bonde hilo wamekuwa wakiuziwa viwanja na wenyeji wanaolizunguka eneo hilo bila kupitia uongozi wa vijiji vilivyoko jirani.

Kadhalika Kaimu Ofisa Kidakio wa Bonde la Wami Ruvu, Ofisi ya Dodoma, Felisiana Mpanda, alivitaja vijiji vilivyovamiwa ni Veyula Juu, Chihikwi, Mzakwe, Gawaye na Zanka.

"Hivi karibuni kuna mtu mgeni aliuziwa hekari 300 za ardhi na hakujua lakini aliondolewa, tunaomba wananchi wanaohitaji kununua viwanja kwenye vijiji hivyo vilivyoko karibu na bonde hilo kuwasiliana na uongozi wa bonde la Wami Ruvu ili kupata ushauri kabla ya kufanya mauziano,"alisema.

Pia alisema kwa kushirikiana na Kambi ya JKT Makutupora walifanikiwa kuwaondoa wachimbaji mchanga waliokuwa wakifanyakazi hizo kwenye bonde hilo.



Ofisa Mifugo kutoka Bodi ya Nyama Tanzania TMB, John Kiboma (kulia), akisimamia uteketezaji wa nyama iliyochinjwa katika machinjio isiyosajiliwa na serikali Kizota jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: PAUL MABEJA**

## 'W'biashara tumieni anwani za makazi kukuza biashara'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAIMU Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Aloyce Mwagofi, amewataka wafanyabiashara kutumia anwani za makazi kwenye biashara zao kwa kuwa zina manufaa ya kijamii na kiuchumi.

Alitoa ushauri huo jana wakati wa kikao kazi kilichowashirikisha wafanyabiashara wakubwa wa mkoa huo kilichohusu utoaji wa elimu ya umuhimu wa kutumia anwani na postikodi. Mwagofi alisema dunia ya sasa inatembea kwa kasi ni muhimu kuzingatia umuhimu wa anwani.

"Wafanyabiashara ni kundi la mkakati linaloelewa haraka na linasaidia kufikia malengo ya kijamii yaliyoko, kama nilivyosema dunia ya sasa inatembea na wanaoitembeza ni wafanyabiashara, mifumo yoyote inayokuja inawezesha biashara kufanyika au mifumo yenyewe ni biashara,"alisema.

Alisema kwa sasa mfanyabiashara popote alipo anaagiza bidhaa nje ya nchi badala ya kusafiri kufuata bidhaa na kukumbana na vikwazo mbalimbali.

"Nchi moja inaweza kufanya biashara na nchi nyingine kubwa ni namna nitakavyoweza kukuuzia, dunia tuliyonayo ni ya kibiashara zaidi," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Clarence Ichwekeleza, alisema mfanyabiashara mwenye anwani kamili inarahisisha kufikiwa kwa haraka.

"Anwani kamili lazima iwe na jina la mtaa, jina la barabara, namba ya nyumba na kata namba zake zimewekwa ambazo ni postikodi, ni muhimu kufikiwa kwa urahisi kupata huduma za kijamii na kiuchumi,"alisema.

Alisema wafanyabiashara hao watapewa elimu ya matumizi ya mfumo wa kidigitali ili wawe wa kwanza kutumia.

# Waziri akemea matumizi nyavu haramu Bwawa la Mtera

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (pichani), amewataka wananchi wanaoishi jirani na Bwawa la Mtera kuacha kutumia nyavu haramu katika shughuli zao za uvuvi.

Wiki kadhaa zilizopita Nipashe lilichapisha ripoti maalum kuhusu hali ya uvuvi katika Bwawa la Mtera na maisha ya familia za wavuvi zilizotelekezwa.

Katika ripoti hiyo ilieleza ugumu wa maisha unavyozikabili familia hizo kutokana na samaki kukosekana kwenye bwawa hilo.



Akiwa katika eneo hilo jana, Simbachawene alisema: "Msitumie nyavu za timba ambazo zina sumu, zinaua mazalia ya samaki na hata kwa mtumiaji wa samaki, waliovuliwa kwa nyavu hizo anaathirika."

Simbachawene ambaye ni Mbunge wa Kibakwe alieleza kuwa bwawa hilo linashindwa kuwa endelevu kwa sababu hakuna shughuli za uvuvi zinazoendelea kutokana na kukosekana kwa samaki.

"Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kushirikiana na maofisa uvuvi katika maeneo yanayozunguka Bwawa la Mtera muandae andiko ambalo litasaidia kuja na mkakati wa uvuvi endelevu katika bwawa hilo," alisema.

Aliongeza kuwa: "Hii itasaidia kutengeneza vikundi vya wavuvi vitakavyopewa uwezeshaji, ili kupita kwa wavuvi wenzao kuwaelimisha juu ya athari zinazotokea kutokana na wavuvi kutumia nyavu haramu".

Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Fransisco Mwanga, alisema uvuvi wa kutumia nyavu haramu aina ya timba ni hatari madhara yake inapogusana na samaki ni kushindwa kuzaliana.

"Elimu imetolewa kwa wavuvi na wakati mwingine kupigwa faini lakini bado wameendelea na uvuvi haramu uliosababisha samaki kutozaliana," alisema.

Mmoja wa wananchi wa eneo hilo, Hussein Mkwizu, alisema suala hilo linapaswa kuwa ajenda ya kudumu kwenye vikao vya maendeleo vya kijiji ili kujenga uelewa wa pamoja kwa wananchi kuondokana na uvuvi haramu.

Alisema: "Lazima kuwe na kikosi kazi kitakachohusisha wabunge wa majimbo yote yanazunguka Bwala la Mtera kitakachojikita katika kuelimisha umma, maana hakuna kambi ambayo imezunguka Bwawa la Mtera ambayo haijapitia hiii shida, sasa hivi kila mtu anafikiria namna tatizo hili linavyoweza kutatuliwa na lisijirudie."



# SMZ yaanza kufanya mageuzi elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeadhimia kufanya mageuzi makubwa katika mfumo wa elimu kwa kuunda kikosi kazi cha mageuzi ya elimu.

**Wizara imeunda kikosi kazi hicho baada ya kuwapo malalamiko mbalimbali juu ya uhitaji wa kuendelea kuboresha elimu.**

Kikosi hicho imeshakamilisha kazi na kuikabidhi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa.

Akisoma muhtasari wa ripoti ya mageuzi ya mfumo wa elimu Zanzibar, katika kikao maalumu, Mwenyekiti wa kikosi kazi, Ahmada Rai alisema ripoti hiyo imeibuliwa matatizo mbalimbali yanayokwamisha maendeleo ya elimu Zanzibar.

Alisema miongoni mwa matatizo hayo ni uhaba wa miundombinu ya kujifunzia katika mfumo wa elimu, uhitaji wa madarasa na msongamano wa wanafunzi madarasani ambao unaathiri matokeo ya mfumo wa elimu.

Rai alisema matatizo mengine ni uzoefu katika usimamizi na mipango ya walimu, mgawanyo mbaya wa ajira kwamba kuna walimu wengi kuliko mahitaji ya masomo ya sanaa na lugha kwa zaidi ya asilimia 77.

"Tatizo ni kutogawa vizuri rasilimali ya walimu na kutozingatia mahitaji katika kuajiri walimu, lakini tumegundua udhaifu wa mafunzo kwa walimu ambapo walimu wengi wana mapungufu katika elimu wanayoipata," alisema.

Alisema kukosekana kwa taasisi ambayo inasimamia mafunzo ya walimu Zanzibar kumechangia kwa kiasi kikubwa kupata walimu wasio na sifa na mbinu muhimu ya kuwafundisha vijana. Rai alisema tatizo lingine waliloliona kwa walimu ni uhamishaji wa walimu usiozingatia mahitaji, baadhi ya shule walimu wamehamishwa bila ya uwapo wa taarifa, maslahi duni ya walimu hali ambayo imesababisha walimu kukosa ari ya kufanya kazi.

"Tumegundua kuwa walimu wengi wanatoka maeneo ya mjini na wanasomesha maeneo ya vijijini bila ya kuwa na usafiri na badala yake walimu wanachelewa kufika shule na wengi wanawahi kuondoka na ufundishaji unakuwa hauna ufanisi na matokeo yake wanafunzi hawapati elimu wanayotarajia kuipata," alisema.

Alisema kukosekana kwa utaratibu wa kitaasisi katika uteuzi wa nafasi za uongozi na usiozingatia sifa mfano kwa walimu wakuu kwamba hakuna utaratibu wa kuchagua walimu wakuu wenye uwezo na wengi walioteuliwa hawana sifa.

Rai alisema: "kukosekana kwa walimu wakuu shuleni wenye uelewa na utaalamu wa kuongoza shule, tusitegemee kupata tija nzuri katika mfumo wa elimu."

Alisema zaidi ya asilimia 80 ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne wanapata ufaulu wa daraja la nne au sifuri na asilimia chini ya 20 wanaopata daraja la kwanza hadi la tatu na matokeo yake wanafunzi wachache wanamaliza kidato cha nne wenye uwezo wa kuendelea na elimu ya juu katika mfumo wa elimu.

Alisema pia mifumo dhaifu ya uendeshaji na usimamizi wa sekta ya elimu, uhaba mkubwa wa rasilimali fedha, kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaorejea na wanaokatisha masomo katika ngazi ya msingi na sekondari na idadi ndogo ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya ufundi, kati na juu.

Waziri wa Elimu, Lela Muhammed Mussa alisema, wizara imeunda kikosi kazi hicho baada ya kuwapo malalamiko mbalimbali juu ya uhitaji wa kuendelea kuboresha elimu.

Alisema kikosi kazi hicho kina wajumbe kutoka taasisi mbalimbali za Zanzibar na Tanzania Bara.

## 'Tasnia upigaji picha ipewe msukumo kutunza historia'

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJA Mkuu wa Mgahawa wa 'Cape Town Fish Market' ulioko Shangani mjini Zanzibar, Lewis Chadamoyo, amesema historia nzuri ya nchi itabakia katika kumbukumbu kwa miaka mingi endapo tasnia ya upigaji picha itapewa msukumo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza katika sherehe ya kuwatunuku vijana walioshiriki shindano la kupiga picha lililobuniwa na mgahawa huo.

Chadamoyo alisema kazi hiyo ina heshima kubwa duniani na imewapa watu wengi umaarufu na utajiri kwa kupiga picha zinazovutia ambazo huelezea taswira halisi ya maeneo na nchi mbalimbali.

"Kijana anapoamka na kuzunguka mitaani kutafuta kitu kinachoweza kumpatia picha nzuri, ni sehemu ya matumizi mazuri ya akili, hivyo jamii na mamlaka zinapaswa kuthamini mchango wake kwa kumpa moyo ili afanye vizuri zaidi," alisema.

Aidha, aliwapongeza vijana wote waliowasilisha picha zao katika shindano hilo la pili, akiwataka wengine kutosita kushiriki mwakani.

Katika shindano hilo vijana 15 walijitokeza kuwania tuzo, ambapo washindi watatu wa kwanza walipewa zawadi za fedha, vyeti.

Akizungumza baada ya kupokea zawadi, mshindi wa kwanza Hamed Mohammed Salum aliyepata Sh.milioni moja alisema siri ya ushindi wake ni hamu ya kuonesha taswira njema ya nchi yake ya Zanzibar na maisha halisi ya Wazanzibari.

Mmoja kati ya wakazi wa Mji Mkongwe, Deepak Josh, alipongeza kazi iliyofanywa na wapigapicha, akisema hatua hiyo ina mchango mkubwa wa kuiuza Zanzibar kimataifa.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhamed Mussa (katikati), akizungumza na wajumbe baada ya kukabidhiwa ripoti ya kuleta mapendekezo ya mageuzi ya mfumo wa elimu katika ukumbi wa mkutano wa wizara hiyo Mazizini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 'Zanzibar haina rekodi chafu ukiukwaji haki za binadamu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema rekodi ya haki za binadamu visiwani Zanzibar ni nzuri na hakuna kesi za kushtakiwa kwa ukiukwaji wa haki hizo katika taasisi za kimataifa.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Faki Hamad, aliyetaka kujua kwa kiasi gani serikali imejipanga kupambana na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Akijibu swali hilo Waziri Suleiman alisema serikali imeingia makubaliano kutekeleza mikataba ya kimataifa katika kuona haki za binadamu zinalindwa ikiwamo kuunda baadhi ya taasisi kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Alisema tume hiyo huwasilisha ripoti yake kila baada ya miaka minne katika vyombo vya kutunga sheria kuonesha kwa kiasi gani masuala hayo yanatekelezwa kikamilifu.

"Mheshimiwa Spika niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba hakuna matukio ya kushtakiwa kwa Serikali ya Zanzibar katika matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu, tumekuwa makini tukilinda haki hizo kwa mujibu wa katiba," alisema.

Alisema serikali imekuja na utaratibu kwa wananchi uitwao "Sema na Rais Mwinyi" ambao wananchi wanawasilisha malalamiko yao kwa serikali katika maeneo mbalimbali ikiwamo ukiukwaji wa haki za binadamu.

Alisema utaratibu huo umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuyapatia ufumbuzi matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na serikali kuyafanyia kazi pamoja na ukiukwaji wa haki za binadamu kwa wananchi.



# Wananchi wafyeka mazao yao wakisherehekea siku ya tohara

**Na Mathias Marwa,** TARIME

SHEREHE za tohara zinazofanyika katika maeneo mbalimbali wilayani Tarime mkoani Mara zimebadilika kuwa sehemu ya uharibifu wa mazao baada ya baadhi ya watu kufyeka mashamba wakati wa shamrashamra za sherehe hizo.

Hali hiyo inayoendelea kujitokeza wilayani humo imeelezwa inatishia ustawi wa mazao na hivyo kusababisha kuwapo na upungufu wa chakula.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe wilayani humo umebaini wakati wa sherehe hizo baadhi ya watu huvamia mashamba na kufyeka mazao yakiwa shambani bila sababu za msingi kwa kisingizio cha kusherehekea.

**Wazee wa mila wa kabila hilo wamelaani vitendo hivyo na kuviita kuwa ni vya kinyama na kuvilinganisha na uhujumu uchumi.**

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyankoni Kata ya Itiryo, Anthony Nyamhanga, aliviita vitendo hivyo kuwa ni vya kihuni na ameitaka jamii kukemea na kuchukua hatua kali dhidi ya watu wanaotekeleza vitendo hivyo.

Nipashe limebaini kuwa wananchi hao hufanya vitendo hivyo kwa kufyeka mshamba ya watu wakati wanapokuwa katika maandamano ya sherehe hizo, lakini hakuna anayefyeka shamba lake mwenyewe.

Pia sherehe hizo za tohara zinazoendelea katika kabila la Wakurya katika ukoo wa Wairegi wilayani Tarime zimebadili sura na kuwa sehemu ya maafa hali ambayo inawapa wakati mgumu wakulima wa mazao mbalimbali katika maeneo yao.

Jamii hiyo ya Wairegi imeanza uharibifu huo hivi karibuni huku wakitembea wakiwà na silaha za jadi yakiwamo mapanga na sime ambazo huzitumia kukata, kufyeka mahindi na migomba.

Wazee wa mila wa kabila hilo wamelaani vitendo hivyo na kuviita kuwa ni vya kinyama na kuvilinganisha na uhujumu uchumi.

John Mwera ni mmoja wa wazee wa mila wa Bwiregi, aliwataka wananchi kuwakamata wanaofanya vitendo hivyo ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Mwera alisema: "Mila na utamaduni wa Wakurya hauruhusu uhalifu wa aina yoyote ufanyike ndani na nje ya jamii, lengo ni kudumisha mila kwa amani bila kuvunja sheria za nchi."



Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Kituo cha Polisi wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Inspekta Elius Skanda, akipokea cheti cha kutambua mchango wao katika kupambana na ukatili wa kijinsia kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Manispaa ya Kahama, Singano Machumu, hafla iliyofanyika Kata ya Kilago jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# 'Walengwa TASAF limeni mazao yanayostahimili ukame'

**Na Halima Ikunji,** SIKONGE

WALENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani Sikonge mkoani Tabora wameshauriwa kulima mazao yanayostahimili ukame.

Wito huo ulitolewa juzi wilayani Sikonge na Ofisa Kilimo wa Kata ya Pangale, Josephine Mzoo.

Alisema wakulima wanapaswa kulima mazao yanayohimili ukame yakiwamo ya viazi, mihogo ili kukabiliana na njaa katika msimu wa kilimo kwa mwaka huu.

Alisema kwamba mvua za mwaka huu ni chache kulingana na utabiri wa hali ya hewa unavyoonyesha kuwa zitanyesha chini ya wastani.

Mmoja wa wanufaika wa TASAF, Nalea Kitumbo, alisema watalima mazao yanayostamili ukame ili kupata chakula katika msimu huu wa kilimo.

Mnufaika mwingine Pili Mgalula alisema utabiri wa hali ya hewa unaoonyesha mvua za mwaka huu zitanyesha chini ya wastani jambo ambalo wanalazimika kulima mazao yanayostamili ukame.

Akizungumzia manufaa aliyoyapata kupitia TASAF, Zafarani Husein, alikiri kunufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kusomesha watoto, kuanzisha miradi, kufuga mbuzi, kuku na bata.

Alisema tangu ajiunge na TASAF mwaka huu ameweza kulima na anatarajia kupata magunia manane ya mahindi.

Alisema: "Tunaishukuru sana serikali kwa kutuondolea umaskini huku vijijini kwetu, kama sio fedha hizo mimi ningekuwa nimeshakufa, lakini kutokana na fedha hizo zimenisaidia kimaendeleo".

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Sikonge, Claud Nkanwa, alisema walengwa hao wameendelea kupewa mafunzo ya namna ya kuwekeza katika rasilimali ili kujiendeleza kiuchumi.

# Wapewa elimu namna kujikinga magonjwa yasiyoambukiza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WATOA huduma za afya 630 wamepewa mafunzo maalum ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

Mafunzo hayo ya siku tano yalifanyika mkoani Mwanza kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Chama cha Kisukari Tanzania (TDA) yalifunguliwa na Mwenyekiti wa Wakufunzi wa Mafunzo kutoka Hospitali ya Taifa Mhimbili (MNH), Dk. Mwanaada Kilima.

Dk. Kilima alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo watoa huduma hao ili kuwawezesha kuelimisha jamii katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema serikali imeandaa mpango mkakati wa tatu wa kitaifa wa kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo na kwamba mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Aliongeza kuwa mkakati huo unatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango mkakati wa afya wa taifa wa mwaka 2021 hadi 2026, unaolenga kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya.

Alisema mpango huo unalenga kuboresha kiwango cha huduma za kinga, tiba na huduma tengemano za magonjwa hayo kuanzia ngazi za jamii mpaka taifa.

Dk. Kilima alisema moja ya mikakati iliyopo ni kuimarisha huduma za msingi kwa kuvijengea uwezo vituo vya afya 600 kwa kuwapa mafunzo watoa huduma za afya juu ya utoaji huduma za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema lengo ni kuwafikia watoa huduma za afya msingi wapatao 3,000 kutoka mikoa 26 ifikapo Desemba mwaka 2023.

Mganga Mkuu Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, alisema magonjwa hayo yanachangia vifo kwa takribani asilimia 33 na hali hiyo inazidi kuwa mbaya kadri miaka inavyozidi kwenda.

"Miaka ya 1980 hadi 1990 hali haikuwa hivi sasa hivi inaongezeka miaka inavyoongezeka, sisi wakati tunasoma tulikuwa tunasema ni magonjwa ya ulaya na wenye pesa hatukutegemea hali itakuwa hivi katika nchi yetu hali inazidi kuwa mbaya, hivyo serikali imeamua kuweka jitihada ili kwenda sambamba na kupunguza tatizo hilo," alisema Dk. Rutachunzibwa.

Alisema kwa sasa kumekuwa na uvumi ambao kila mtu anaongea neno lake na kwamba watoa hudumu hao wanapaswa kutumia elimu watakayoipata kutoa taarifa sahihi kwa wananchi.

Dk. Rutachunzibwa alisema wananchi wanapaswa kujengewa moyo wa kujitokeza kupima na kutambua afya zao ili kujua namna ya kukabiliana na magonjwa hayo.

# DRC yashutumu waandishi wa Rwanda

**Congo (DRC)**

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imelaani vikali kile ilichoeleza kuwa na uwepo haramu wa waandishi wa habari wa shirika la Rwanda katika eneo la Congo.

Wizara ya habari ya DRC ilidai jana kuwa vyombo vya habari vya propaganda vilikuwa vikisindikizwa na wanajeshi waasi wa M23 na wanajeshi wa Rwanda hadi maeneo mengi ya mashariki mwa nchi hiyo.

"Kitendo hiki kinapaswa kuvuta hisia za jumuiya ya kitaifa na kimataifa kwa kampeni mpya ya Rwanda ya uongo na upotoshaji wa ukweli, kuendeleza ushuhuda wa uongo wa wenyeji na kupotosha ukweli kuhusu mauaji ya halaiki," ilisema.

Aidha, pamoja na madai hayo Rwanda imekuwa ikikanusha kuhusika na ghasia zinazoendelea nchini DRC.

Wiki iliyopita Marekani ilitoa wito kwa Rwanda kusitisha uungaji mkono wake kwa kundi la waasi la M23 lakini Rwanda ilisema jukumu hilo linafaa kuwekwa kwa DRC.

Taarifa hiyo ilitolewa kukiwa na uchunguzi wa Umoja wa Mataifa (UN) uliogundua kuwa takriban raia 131 nchini DRC walikufa katika shambulio la Novemba lililofanywa na kundi la waasi la M23.

Ripoti ya UN iliyotolewa wiki iliyopita, ilisema mauaji hayo yalifanyika katika vijiji viwili Kishishe na Bambo, katika wilaya ya Rutsuhuru, jimbo la Kivu Kaskazini mashariki.

DRC ilisema serikali yake imedhamiria kufuata njia za kisheria dhidi ya wale waliohusika na uhalifu wa kimataifa ikiwa ni pamoja na mauaji ya halaiki huko Kishishe.

**BBC**

**"Kitendo hiki kinapaswa kuvuta hisia za jumuiya ya kitaifa na kimataifa kwa kampeni mpya ya Rwanda ya uongo na upotoshaji wa ukweli, kuendeleza ushuhuda wa uongo wa wenyeji na kupotosha ukweli kuhusu mauaji ya halaiki," ilisema.**

# Rais Ukraine aomba msaada G7

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ameziomba nchi tajiri duniani za kundi la G7 kuipatia nchi yake gesi ya ziada pamoja na silaha ili kuisaidia nchi hiyo kujinusuru na baridi kali ya msimu ambayo inatishia kusababisha mateso zaidi kwa mamilioni ya raia.

Akizungumza kwa njia ya video jana, Rais Zelensky, alisema msimu wa baridi kali umesababisha taharuki nchini humo kutokana na miundombinu yake ya nishati kusambaratishwa na mashambulizi ya anga ya Russia.

Rais Zelensky alifanya mkutano kwa njia ya video na viongozi wa G7, na kusema kuwa nchi yake inauhitaji wa kiasi cha mita za ujazo bilioni mbili za gesi ya ziada itakayowasaidia katika kipindi hiki cha baridi kali.

Hivi sasa nchini Ukraine theluji imetanda na mifumo yote ya nishati imesambaratishwa na mashambulizi ya anga ya Russia, na kubainishwa kuwa raia wengi wanakabiliwa na hali ya baridi kali bila ya umeme wala mifumo ya kusambaza joto majumbani mwao.

Pia Rais huyo alitoa wito kwa viongozi wa G7 kutuma silaha zaidi katika nchi yake ikiwemo vifaru vya kijeshi vya kisasa, mizinga na makombora ya masafa marefu.

"Nawatolea mwito muongeze msaada kwa ajili ya Ukraine katika suala la gesi. Ugaidi dhidi ya mitambo yetu ya umeme umetufanya tutumie kiasi kikubwa cha gesi kuliko tulivyotarajia, na ndiyo sababu tunahitaji msaada zaidi katika kipindi hiki cha baridi. Tunazungumzia mita za ujazo bilioni mbili za gesi, ambazo zinahitaji kununuliwa," alisema.

Aliongeza kuwa kinachochochea alichokiita kiburi cha jeshi la Russia ni uwezo wa silaha walionao, huku baadhi ya wananchi wa Ukraine kama Oleg Klyutshko mzee wa miaka 62 wanasema hawaogopi baridi kali lakini wangependelea zaidi kuona mashambulizi ya Russia yanasitishwa, na kwamba wanaweza kuvumilia hali yoyote ile.

Serikali ya Ukraine ilisema asilimia 40 ya miundombinu yake muhimu ya nishati imeharibiwa kabisa wakati wa mashambulizi ya Russia yakiendelea kuilenga nchi hiyo.

Wizara ya nishati ya nchi hiyo ilitoa taarifa ikisema mashambulizi ya makombora ya Russia yameharibu mitambo yake yote ya umeme unaotokana na mvuke wakati miundo mbinu yake mingine muhimu pia ikiharibiwa.

Kampuni ya umeme ya (YASNO) ilisema inalazimika kuweka mgao wa usambazaji umeme katika mji mkuu wa Kiev, na kwamba asilimia 40 ya usambazaji umeelekezwa katika miundombinu muhimu. Kampuni ya mafuta na gesi ya (DTEK) ilisema wataalamu wake wanahangaika muda wote kutafuta vifaa kukarabati miundombinu ya nishati iliyokwisha haribiwa na Russia na imefikia makubaliano na wasambazaji wa Ulaya (ABB) na Simens.

Kwa mujibu wa Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, viongozi wa kundi la G7 wamekubaliana kuhusu maeneo muhimu ya kushirikiana katika msaada wa fedha kwa ajili ya Ukraine.

Hata hivyo ilibainishwa kuwa, mkutano wa Paris unatarajiwa kuchangisha mabilioni ya dola kwa ajili ya kuwasaidia raia wa Ukraine kukabiliana na msimu wa baridi kali.

**DW**



Hali ya ubaridi ilivyokithiri nchini Ukraine. **PICHA:MTANDAO.**

# Marekani kuipatia Afrika dola bilioni 55

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imetangaza msaada wa dola bilioni 55 kwa nchi za Afrika, ndani ya kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Tangazo hilo lilitolewa jana wakati Rais Joe Biden akijitayarisha kuwa mwenyeji wa viongozi wa nchi za Afrika, katika mkutano ulioanza jana jijini Washington DC.

Biden anafanya majadiliano na kundi dogo la viongozi wa Afrika kuhusu chaguzi zitakazofanyika mwaka 2023 na demokrasia barani Afrika.

Mshauri wa usalama wa taifa wa 'white house' Jake Sullivan, alisema Marekani inaleta rasilimali mezani wakati wa kongamano hilo, akiongezea kwamba nchi yake ina nia ya dhati kulisaidia bara la Afrika kuliko nchi nyingine.

Biden aliwakaribisha kwa chakula cha jioni takriban viongozi 50 wa Afrika, ambao wanatarajiwa kutangaza uanachama wa Afrika katika muungano wa nchi 20 tajiri duniani.

Aidha, aliahidi kuongoza juhudi za Afrika kuwa na mwanachama wa kudumu katika baraza la usalama la umoja wa mataifa. Pia ilibainishwa kuwa atateua mjumbe maalum kufuatilia utekelezaji wa mambo yatakayojadiliwa katika kongamano hilo.

**VOA**

## MATANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**CHRISTIAN KAMUGISHA KAIJAGE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPOT YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA TAE528915 ILIYOTOLEWA NA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI(UHAMIAJI) MWAKA 15/11/2022, KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA CHOCHOTE CHA POLISI
**POLISI TAARIFA ARU/ARU/RB 477744/22**

### KUPOTEA KWA CHETI



**ISAYA PROSPER MATHIAS**
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye namba za usajili **(INDEX NUMBER S0853/0154/2015)** kilichotolewa na baraza la mtihani kupitia shule ya sekondari ya kizwite mwaka 2015.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi au piga cm namba 0747092974.
**MOR/MOR/RB/480475/2022**

### KUPOTELEWA NA CHETI



**SIGFRID BALTAZARY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S316/0291** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Kibasila Secondary School mwaka 1997. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/480598/2022.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA.4/2022**
**Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya**
**MAREGESI BENJAMIN MANYAMA........MAREHEMU**
**NA**
**MATALA MORICE MANYAMA......MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75 na 76)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa Mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 9 Februari mwaka 2023.
**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01 Mwezi wa Desemba, 2022

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MILTON RICHARD ALOYO** anatngaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 588 DLP, CHASSIS NAMBA: MD2B15BX2NWC97349** na **ENGINE NAMBA: JVXWNC04961 .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: KW/RB/5129/2022**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROSE ISSAYA MOLLEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T742DEP** aina ya **TOYOTA IST**.Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya polisi
**DOD/DOD/RB/434058/2022.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 222 YA MWAKA 2022.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU MELKIOR MATEI MBWAGAI**
**SUZANA MELKIOR MBWAGAI...........................1 MWOMBAJI**
**PAULINA PETER MSENYE............................2 MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa na uthibitidho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15 wa mwezi wa Februari, 2023.

Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 08 mwezi wa Novemba, 2022.

NAIBU MSAJILI

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PRIMA HERMAN KWEKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 210 CKA ,** CHASSIS NAMBA: **NCP610002087** na ENGINE NAMBA: **1NZ2253682.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA :
**ARU/ARU/RB/478504/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na 71/....2022**
**JINA LA MDAI: FARAJA ROBERT**
**JINA LA MDAIWA: ALDO GEORGE MGAO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:ALDO GEORGE MGAO................MDAIWA**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Kuomba kuvunja ndoa na kupatiwa talaka . Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 14/12/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07/12/2022

### KUPOTEA KWA VYETI



**RACHEL GOODLUCK MANJIRA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0491-0051 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KILOMENI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015, **CERTIFICATE OF ACCOUNTANCY** chenye usajili namba **DSM/BCA/16/35857** kilichotolewa na **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY** mwaka 2017 na cheti cha **DIPLOMA OF ACCOUNTANCY** chenye usajili namba **DSM/DA/17/44190** kilichotolewa na T**ANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY (TIA)** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI CONTROLL NAMBA**:9910835214553**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI



# DIAMOND, THE GAME WANA JAMBO LAO

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Naseeb Abdul 'Diamond Platinumz', amethibitisha ujio wa wimbo wake mpya aliomshirikisha mwana Hip Hop kutoka nchini Marekani, Jayceon Terrell Taylor maarufu kama 'The Game'.

Taarifa hiyo imeenea kwa kasi baada ya kuonekana kwa komenti ya nyota huyo kwenye moja ya chapisho la ukurasa wa Instagram wa Diamond, lililohusu onyesho lake litakalofanyika Kigali nchini Rwanda.

Kwenye chapisho hilo, rapa The Game aliweka komenti ya emoji za moto kama kiashiria cha kupendezwa na kazi za Diamond.

Miaka ya hivi karibuni, mwanamuziki Diamond amewavutia wasanii wengi wakubwa kutoka mataifa mbali mbali, ikiwamo Marekani.

## JOTI APANIA TUZO MCHEKESHAJI BORA

MSANII wa vichekesho, Lucas Mhuvile maarufu Joti, amefunguka na kuweka wazi namna alivyojipanga katika kuhakikisha anaipambania tuzo ya mchekeshaji bora katika tuzo za filamu zinazotarajiwa kufanyika Arusha Jumamosi wiki hii.

Joti ameeleza namna alivyo na kitete pamoja na hofu kwenye kinyang'anyiro hicho kwa msimu wa pili huku akifafanua zaidi hana shaka na ubora wa kazi zake.

Amewaomba Watanzania na wapenzi wa kazi zake kumpigia kura kwenye vipengele viwili alivyofanikiwa kuingia katika kinyang'anyiro ikiwamo kipengele cha filamu bora ya ucheshi na mchekeshaji bora.



Katika kipengele hicho kinawaniwa na wasanii mbalimbali akiwamo Mkojani, Gladness Kifaluka, Tabu Mtingita pamoja na Braza K.

Aidha, filamu bora ya vichekesho ambazo zimefanikiwa kuingia ni 'Usipite Jeshini' ya Joti, Mama Mkwe ya Tabu pamoja na msanii Braza K katika vichekesho vya futuhi, Gladness Kifaluka wa filamu ya Kitimtim na Mkojani akiingia na filamu ya Ugaigai.

Hata hivyo, Joti ameeleza namna kuwapo kwa tuzo hizo kumesaidia sana tasnia ya filamu kukua na kuimarika kutokana na uwapo wa ushindani pamoja na serikali kutambua mchango wa tasnia ya filamu.

"Kwa mara ya pili nashiriki tuzo hizo, kwa mwaka jana zilifanyika Mbeya na nilifanikiwa kushinda tuzo mbili ikiwamo mchekeshaji bora wa mwaka 2021 pamoja

## MOBETTO ASHEREHEKEA SIKU YA MAMA YAKE

MAMA wa mwanamitindo, Hamisa Mobetto, Shufaa Lutigunga, aliadhimisha siku yake ya kuzaliwa Jumatatu ya Desemba 12, mwaka huu.



Huku akisherehekea siku hiyo maalum katika maisha yake kupitia mtandao wa Instagram, Shufaa alimshukuru Mungu kwa hatua hiyo na kujitakia heri ya siku yake ya kuzaliwa.

"Bi mzuri kazaliwa leo," aliandika.

Makumi ya wanamitandao walimiminika kwenye ukurasa wa Instagram wa mama yake Mobetto na kumtakia heri ya siku ya kuzaliwa.

Wasanii mashuhuri wakiwamo Jacqueline Wolper, Mwijaku, Fayvanny na Kassim Mganga walijumuika na Hamisa kumsherehekea mama yake.

"Siku ya kuzaliwa yenye furaha zaidi kwa Malkia wangu Mama Mobetto, nakupenda kutoka na mwezi na kurudi," aliandika Hamisa.

Aidha, alimtaja mama yake kama mama bora na kumtakia maisha marefu.

"Mungu akuweke kwa ajili yangu mama yangu. Nakupenda. Asante kwa kuwa mama yangu katika kipindi hiki cha maisha na nikipata nafasi ya kukuchagua katika maisha yangu mengine bado nitakuchagua wewe," alisema.

# SERENGETI BYTES YATANGAZA MSIMU WA TUZO ZA KIDIGITALI

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa Tuzo za Kidigitali Tanzania (Tanzania Digital Awards) kwa mwaka 2022, umezinduliwa rasmi jijini Dar es Salaam jana ambapo kwa mwaka huu utakuwa na jumla ya vipengele 12 vitakavyopigiwa kura ili kupata mshindi katika kila kipengele.

Programu hiyo ya tuzo iliyoanzishwa na Serengeti Bytes mwaka 2020, inalenga kukuza uwajibikaji, ubunifu, na uvumbuzi katika matumizi ya teknolojia za kidigitali nchini.

Katika msimu wa kwanza na wa pili wa tuzo za Tanzania Digital Awards, ulipata mwitikio mzuri kutoka kwa wadau mbalimbali na Watanzania kwa ujumla ambapo zaidi ya mapendekezo 60,000 yalipokelewa huku kura 250,000 zikipigwa kutoka kwa wananchi, kuchagua washindi 108 katika vipengele mbalimbali.

Taasisi za umma, makampuni, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi, walipendekezwa na kupigiwa kura katika vipengele vikuu 12 katika msimu wa mwaka 2021.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo jijini Dar es Salaam jana, Michael Mallya, Ofisa Uendeshaji wa Kampuni ya Serengeti Bytes, ambao ni waandaaji wa tuzo hizo alisema kwa mwaka huu Tanzania Digital Awards imeendelea na idadi ya vipengele vikuu 12 na vipengele vidogo 52.

Alivitaja vipengele vikuu kuwa ni Uvumbuzi Kidigitali, Benki Kidigitali, Mawasiliano ya Simu Kidigitali, Burudani Kidigitali, Msoko na Biashara Kidigitali, Vyombo vya Habari Kidigitali, Serikali Kidigitali, Uchechemuzi Kidigitali na Diplomasia Kidigitali. Nyingine ni Tuzo ya Chaguo la Watu na Tuzo ya Heshima.

Mallya alisema baada ya mchakato wa uteuzi mapendekezo, kamati ya ufundi ambayo ina jukumu la kufanya tathmini itawachuja wateule kwa kila kipengele na majina yatawekwa kwenye tovuti kwa ajili ya kupigiwa kura kuanzia Januari 5 - 26, mwakani.

"Baada ya kukamilika kwa mchakato wa kupiga kura, kamati ya kiufundi itafanya tathmini ya kura na kuidhinisha washindi tayari kwa hafla ya tuzo ambayo imepangwa kufanyika Februari 25, mwakani," alisema.

Alisema uzinduzi wa msimu wa 2022 umekwenda sambamba na kuzinduliwa kwa mchakato wa kupendekeza wawania tuzo ambapo umeanza jana hadi Desemba 27, mwaka huu, ambao utafanywa kupitia fomu ya mapendekezo inayopatikana kwenye tovuti ya Tanzania Digital Awards.

"Wadau na kila mmoja ana uwezo wa kupendekeza watu wanaoweza kuwania tuzo hizo katika kipengele kinachofaa, makampuni na watu binafsi wanaweza kujipendekeza katika vipengele mbalimbali kutokana na sekta zao," alisema.

Mallya alisema katika msimu miwili iliyopita ya tuzo hizo, imekuwa na ushindani wa hali ya juu na wa kusisimua, hivyo wanatarajia tuzo hizo kuwa na msisimko zaidi mwaka huu.

"Tangu kuzinduliwa kwake mwaka 2020 Tuzo za Tanzania Digital Awards zimekua na kuongeza thamani katika ekolojia ya teknolojia za kidigitali nchini. Mwaka jana tuliona msimu wa kusisimua na wenye ushindani. Tuliongeza vipengele vikuu viwili zaidi kufuatia mapendekezo ya wadau mbalimbali lengo likiwa ni kuongeza ushirikishwaji wa sekta ambazo tayari zinafanya vizuri kupitia teknolojia za kidigitali," alisema.

Aidha, Mallya alisema wananchi na wadau wanatakiwa kutembelea tovuti ya Tanzania Digital Awards (www.digitalawards.co.tz) kwa taarifa zaidi kuhusu vipengele, vigezo, upendekezaji, upigaji kura na udhamini au kwa maelezo ya ziada, unaweza kuwasiliana na waandaaji kupitia barua pepe info@digitalawards.co.tz/partnerships@digitalawards.co.tz au kupitia simu kwa nambari +255 737 957 082.




Afisa Uendeshaji wa Kampuni ya Serengeti Bytes, Michael Mallya (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa msimu wa tatu wa Tuzo za Kidigitali Tanzania (Tanzania Digital Awards), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Afisa Mawasiliano wa kampuni hiyo, Nicole Kyakula. **MPIGAPICHA WETU**

# Zahera ataka wa4 wapya Polisi Tanzania

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Mwinyi Zahera, amewaelekeza mabosi wa timu hiyo kumtafutia wachezaji wapya wanne kwenye kipindi cha dirisha dogo akiwamo straika mwenye uwezo wa kufunga mabao manane mpaka 10 kwa msimu.

Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Robert Munisi, amebainisha hilo jana akielekeza mipango kuelekea dirisha dogo la usajili baada ya timu hiyo kutofanya vema kwenye mzunguko wa kwanza.

Munisi alisema baada ya kupata mapendekezo hayo kwa sasa wameanza kuyafanyia kazi kwani kwa kuanza mazungumzo na baadhi ya wachezaji na wanaamini watafanikiwa.

"Tunasubiri dirisha lifunguliwe msikie jeuri yetu, kocha wetu ametuelekeza tusajili wachezaji wanne, anataka straika mmoja mwenye uwezo wa kufunga mabao kwa wastani wa nane mpaka 10 kwa msimu, kiungo mshambuliaji mwenye uwezo wa kupiga pasi za mwisho, beki wa pembeni na beki wa kati, tumeshaanza mazungumzo na baadhi ya wachezaji naamini tutafanikiwa," alisema Munisi.

Alisema wanajua kuwa dirisha dogo mahitaji yanakuwa mengi na wachezaji ni wachache, lakini wamejipanga vizuri kupambana na hiyo hali.

"'Mzunguko wa pili hatutaki kupoteza kizembe, tunataka tukikosa pointi tatu tupate moja, tulikuwa tuna shida huko nyuma, tukaliondoa benchi letu ya ufundi, kwa hiyo tunahitaji sasa kuongeza wachezaji wachache baada ya kumpata mwalimu ili tupambane, huku kwenye kushuka hatupo," alisema Makamu Mwenyekiti huyo.

Polisi Tanzania ndiyo timu inayoburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, ikiwa na pointi tisa katika michezo 15 iliyocheza.

## Uhamiaji yapania mzunguko wa pili

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Uhamiaji FC imesema imejipanga kufanya mapinduzi makubwa katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar utakaoanza Januari mwakani.

Ligi Kuu ya Zanzibar kwa sasa ipo mapumziko kuelekea michuano ya Kombe la Mapinduzi pamoja na usajili wa dirisha dogo ambalo lilifunguliwa rasmi jana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu ya Uhamiaji FC, Abdi Saleh, alisema katika kipindi hiki cha mapumziko wanaisuka upya timu hiyo ili kuhakikisha inafanya mapinduzi ya matokeo mazuri katika mzunguko wa pili.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo hivi sasa wanayafanya ni kuziba mapengo ya wachezaji katika nafasi zote ambazo zilikuwa na mapungufu katika mzunguko wa kwanza hususan safu ya ushambuliaji pamoja na ulinzi ambapo tayari wamewapata wachezaji watakao wasajili ili kuziba pengo hilo.

## Uchaguzi TaBSA warudishwa nyuma

**Na Hadija Mngwai**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limefanya mabadiliko ya uchaguzi wa Chama cha Mchezo wa Baseball na Softball nchini (TaBSA), ambapo sasa utafanyika Ijumaa wiki hii badala ya Jumapili kama ilivyokuwa hapo awali.

TaBSA wanatarajia kufanya uchaguzi wa viongozi mbalimbali kuanzia mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu, katibu msaidizi, mweka hazina na wajumbe wanne wawakilishi wa wachezaji katika klabu na shule.

Viongozi wengine wanaotarajia kuchaguliwa siku hiyo ni Mkurugenzi wa Ufundi wa Baseball na Mkurugenzi wa Ufundi Softball.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo Cha Uhusiano na Mawasiliano wa BMT, Naaja Bakari, amesema usaili wa nafasi hizo unatarajia kufanyika kesho badala ya keshokutwa, katika ukumbi wa Shule ya Sekondari Azania Dar es Salaam.

"Kuna mabadiliko kidogo kuelekea kwenye uchaguzi wa viongozi wa chama hicho, sasa utafanyika Desemba 16 badala ya Desemba 18, mwaka huu," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**FELIX HUYOOO ARSENAL**
KLABU ya Arsenal imepewa nafasi kubwa ya kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Atletico Madrid Januari, mbele ya Paris St-Germain, Manchester United na Aston Villa. ***(Marca)***

**FERNANDEZ KUTUA LIVERPOOL**
LIVERPOOL ina makubaliano kimsingi na Benfica ya kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez, mwenye umri wa miaka 21. ***(La Capital)***

**SOUTHGATE KUENDELEA ENGLAND**
CHAMA cha Soka cha England, FA, kinamtaka Gareth Southgate kuendelea kuwa kocha wa England. ***(Bild)***

**RODGERS AFIKIRIWA ENGLAND**
CHAMA cha Soka cha England, FA, kinamuona Kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers, kama kocha mwenye nafasi nzuri kuichukua timu ya taifa, lakini si Frank Lampard au Steven Gerrard. ***(Star)***

**MUDRYK SAFI ARSENAL**
KUNA "nafasi nzuri" ya Arsenal kumsajili winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk, katika dirisha la Januari, kwa chini ya dau la pauni milioni 86 ambalo Shakhtar Donetsk ilikuwa ikitaka ili kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Athletic)***

**ANCELOTTI ATAKIWA BRAZIL**
BRAZIL wanamtaka Carlo Ancelotti kurithi mikoba ya Tite kama kocha baada ya kutolewa kwenye Kombe la Dunia. ***(UOL Esporte)***

**TIELEMANS AWANIWA ARSENAL**
KLABU ya Leicester City ipo kwenye mazungumzo na Arsenal katika jaribio la mwisho la kumuuza Youri Tielemans Januari, kabla ya kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 25, kumaliza mkataba wake msimu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

**MOUKOKO KUTUA CHELSEA**
CHELSEA imeanza mazungumzo ya kumsajili mchezaji wa Ujerumani, Youssoufa Moukoko, mwenye umri wa miaka 18 kwa uhamisho wa bila malipo kutoka Borussia Dortmund Julai. (***Nicolo Schira***)

**DEMBELE AWINDWA PSG**
KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kumsajili winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele, mwenye umri wa miaka 25 kutoka Barcelona. ***(El Nacional)***

**LEAO KUONGEZEWA MKATABA**
AC Milan ipo kwenye mazungumzo na mchezaji anayesakwa na Chelsea na Manchester United, Rafael Leao, mwenye umri wa miaka 23 kuhusu kuongezewa mkataba. ***(Gazzetta dello Sport, Through Goal)***

**MAN NA MIKATABA MIPYA**
MANCHESTER United itaweka wazi kifungu cha kuongeza mkataba kwa golikipa wa zamani wa Hispania, David de Gea, mwenye umri wa miaka 32, beki wa kushoto wa England, Luke Shaw (27), na kiungo wa kati wa Brazil, Fred (29), pamoja na mshambuliaji wa England, Marcus Rashford (25), na mlinzi wa kulia wa Ureno, Diogo Dalot, 23. ***(Manchester Evening News)***

**MAX KUTUA LEEDS**
KLABU ya Leeds United inapanga kumnunua beki wa kushoto wa PSV Eindhoven na Ujerumani, Philipp Max, mwenye umri wa miaka 29 Januari. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO: NEYMAR ATARUDI KOMBE LA DUNIA NA NGUVU

Bado ni mdogo, ninaamini anaweza kucheza tena, nina furaha sana kwamba ameonyesha...

**DOHA, Qatar**

NEYMAR "atarejea akiwa na nguvu zaidi" baada ya Brazil kuondolewa katika Kombe la Dunia, kwa mujibu gwiji wa soka wa nchi hiyo, Ronaldo Luis Nazario de Lima.

Brazil walitupwa nje ya Kombe la Dunia na Croatia kwa mikwaju ya penalti, licha ya Neymar kuifungia bao katika kipindi cha pili cha muda wa nyongeza.

Bluno Petkovic alisawazisha zikiwa zimesalia dakika nne kabla ya mchezo kumalizika, na Rodrygo na Marquinhos wakakosa mikwaju yao ya penalti huku Croatia ikifuzu kwa nusu fainali hiyo kwa mara ya pili mfululizo.

Neymar alikuwa apige penalti ya tano kwa Brazil, lakini kukosa kwa wachezaji wenzake kulimaanisha kwamba hakupata nafasi hiyo na nyota huyo wa Paris Saint-Germain aliachwa akimwagaa machozi baada ya kutolewa.

Ronaldo, ambaye alishinda Kiatu cha Dhahabu wakati Brazil ikinyanyua Kombe la Dunia la 2002, anatumaini Neymar atarejea kutoka kwenye masikitiko yake huko Qatar.

"Nadhani kwa sasa anasikitishwa na kuondolewa," alisema Ronaldo akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni kawaida kwake kujisikia hivyo, lakini nina uhakika atarejea akiwa na nguvu zaidi na kuendelea kuichezea timu.

"Bado ni mdogo, na ninaamini anaweza kucheza Kombe lijalo la Dunia. Nina furaha sana kwamba ameonyesha ulimwengu kujitolea kwake kwa timu ya taifa na kwamba amejitunza katika kipindi cha miezi sita iliyopita.

"Ni muhimu sana kwetu, hivyo natumaini atapona haraka na kurejea akiwa na nguvu zaidi akiwa na PSG na Selecao."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 423,

MECHI KALI

FRANCE
VERSUS
MOROCCO

1 | 1.52
X | 3.79
2 | 6.79

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARSENAL WAONGOZA MBIO KUMNASA MUDRYK

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imefanya mazungumzo na Shakhtar Donetsk kuhusu winga, Mykhaylo Mudryk, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ni mmoja wa washambuliaji wanaohitajika sana Ulaya hivi sasa, na Shakhtar wako tayari kumuuza, lakini kwa bei sahihi tu.

Shakhtar wamesema hadharani kwamba Mudryk kwa sasa thamani yake ni euro milioni 100.

"Yeyote anayetaka kumsajili Mudryk lazima alipe kiasi kikubwa cha fedha, vinginevyo hatuwezi kumuuza," alisema Mkurugenzi wa Soka wa Donetsk, Darijo Srna mwishoni mwa wiki.

Mudryk mwenyewe hajaficha nia yake ya kutaka kuhama na alikuwa karibu kujiunga na Brentford katika majira ya joto na kisha akaona dili linalowezekana na Bayer Leverkusen likishindikana.

AC Milan, Juventus, Ajax na Newcastle United pia zimemtazama kwa karibu katika miezi ya hivi karibuni, lakini 90min inaelewa kuwa Arsenal sasa wanaonekana kuongoza katika mbio za kumnasa.

'Washikabunduki' hao wamelenga kusajili fowadi mpya wakati wa dirisha la Januari baada ya kushindwa kumpata Raphinha majira ya joto.

Pia, wanamtaka kiungo na beki, lakini mshambuliaji mpya anaibuka kama kipaumbele chao cha kwanza.

Moussa Diaby, Christian Pulisic na Joao Felix pia wamejadiliwa na uongozi wa klabu hiyo, lakini Mudryk ndiye mchezaji ambaye anaonekana kuhitajika zaidi.

Vyanzo vya karibu na Arsenal vinaamini kuwa wako tayari kuvunja rekodi ya klabu yao ili kumleta Mudryk Kaskazini mwa London, lakini inabakia kuonekana kama wanaweza kukubaliana na Shakhtar.

# Hadji: Morocco inaweza kufanya maajabu Qatar

**DOHA, Qatar**

MOROCCO inaweza "kufanya miujiza" chini ya kocha Walid Regragui, amesema kiungo wa zamani na Kocha Msaidizi, Mustapha Hadji.

Simba wa Atlas hao wametinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Dunia, na ni taifa la kwanza la Afrika kufika hatua hiyo na leo Jumatano watacheza na Ufaransa.

Akiwa amemrithi Vahid Halilhodzic Agosti, Regragui amesimamia ushindi dhidi ya Ubelgiji, Hispania na Ureno kwenye michuano hiyo.

Hadji aliichezea Morocco katika michuano miwili ya Kombe la Dunia (1994 na 1998), huku akiwa kocha msaidizi wa taifa lake kuanzia 2014 hadi mapema mwaka huu.

Gwiji huyo mwenye umri wa miaka 51, amefurahishwa na kile alichokiona, akiiambia L'Equipe: "Hapa Morocco, ni wazimu, kinachotokea kwa timu ya taifa ni cha ajabu.

"Ni miezi miwili au mitatu tu tangu Walid Regragui awasili katika timu ya taifa. Kulikuwa na mzozo na Vahid.

"Kocha mpya aliweza kupata maneno na njia ya kuwatoa wachezaji bora na kutengeneza timu yenye ari kubwa. Na timu inacheza kwa moyo na hali ya juu."



,809,300

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 15/12/22 | 23:00 | GD Estoril vs Famalicao | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 2. 15/12/22 | 23:00 | Viseu vs Tondela | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 3. 16/12/22 | 11:45 | Newcastle Jets vs Brisbane Roar | 2.44 | 3.49 | 2.64 |
| 4. 16/12/22 | 15:30 | Abha vs AL Tai | 2.71 | 3.16 | 2.61 |
| 5. 16/12/22 | 21:30 | Santa Clara vs FC Arouca | 2.23 | 3.17 | 2.97 |
| 6. 16/12/22 | 22:00 | FCV Dender EH vs Jong KRC Genk | 2.45 | 3.56 | 2.52 |
| 7. 16/12/22 | 22:00 | Roda Kerkrade vs PEC Zwolle | 2.66 | 3.55 | 2.34 |
| 8. 16/12/22 | 22:00 | NAC Breda vs Almere City | 2.71 | 3.50 | 2.33 |
| 9. 16/12/22 | 22:00 | Helmond Sport vs Den Bosch | 2.32 | 3.60 | 2.66 |
| 10. 16/12/22 | 22:00 | De Graafschap vs Willem II Tilburg | 2.47 | 3.51 | 2.52 |
| 11. 16/12/22 | 23:00 | Saint Brieuc vs Villefranche Sur Saone | 2.92 | 3.21 | 2.32 |
| 12. 16/12/22 | 23:00 | Dunkerque vs Bourg Peronnas | 2.41 | 3.17 | 2.82 |
| 13. 16/12/22 | 23:00 | Nancy vs FC Martigues | 2.30 | 3.15 | 3.01 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 14/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 10:00 | 3623 | Dalian Aerbing vs Wuhan Three Towns FC | 11.70 | 6.24 | 1.17 |
| 11:00 | 1335 | PS Tni vs Arema | 4.17 | 3.30 | 1.79 |
| 12:00 | 3845 | Wuhan Zall vs Tianjin Teda | 5.44 | 4.27 | 1.47 |
| 13:00 | 5911 | Kapaz vs Sabah | 7.01 | 4.09 | 1.40 |
| 14:00 | 3255 | Vietnam vs Philippines | 1.21 | 6.24 | 14.08 |
| 14:00 | 5621 | Persis Solo vs Barito Putera | 1.58 | 3.55 | 5.45 |
| 14:30 | 4626 | Guangzhou RF vs Shanghai Shenhua | 2.48 | 3.16 | 2.63 |
| 15:00 | 4409 | Apollon Paralimniou vs Nikolaos | 2.43 | 3.06 | 2.77 |
| 15:40 | 5975 | Sohar Club vs Al Suwaiq | 2.68 | 2.63 | 2.88 |
| 15:45 | 5082 | Ghazl EL Mahallah vs Talaea El Gaish | 2.73 | 2.78 | 2.87 |
| 16:00 | 1611 | Kalamata FC vs PAOK | 7.38 | 4.18 | 1.38 |
| 16:00 | 2183 | US Monastir vs Africain | 2.19 | 2.68 | 3.71 |
| 16:00 | 2238 | Hawassa Kenema SC vs Ethiopia Electricity | 2.15 | 3.15 | 3.50 |
| 16:00 | 2980 | Malaysia vs Maldives | 1.13 | 8.06 | 20.15 |
| 16:00 | 4467 | CS Sfaxien vs Stade Tunisien | 2.14 | 2.96 | 3.39 |
| 16:15 | 4106 | Dewa United vs Persib Bandung | 4.75 | 3.83 | 1.59 |
| 16:30 | 3877 | Sudeva Delhi FC vs Sreenidi Deccan FC | 4.18 | 3.45 | 1.75 |
| 17:00 | 3928 | Al Seeb vs Rustaq Club | 1.48 | 3.55 | 7.01 |
| 17:35 | 4991 | AL Tadamon vs Al Salmiyah | 4.00 | 3.70 | 1.82 |
| 18:00 | 1473 | FK Sumgayit vs Sabayil | 2.44 | 2.97 | 2.83 |
| 18:30 | 2070 | Sitra Club vs East Riffa | 2.31 | 3.26 | 2.77 |
| 18:30 | 3593 | Riffa Club vs Muharraq SC | 1.80 | 3.21 | 4.28 |
| 19:00 | 1366 | Lamia vs Kallithea FC | 1.80 | 3.21 | 4.28 |
| 19:00 | 2524 | Mqabba FC vs Zurrieq | 2.83 | 3.41 | 2.20 |
| 19:00 | 3340 | Homburg vs Hoffenheim II | 1.96 | 3.49 | 3.30 |
| 20:00 | 5257 | Rapid Bucuresti vs Petrolul Ploiesti | 1.79 | 3.43 | 4.37 |
| 22:00 | 1971 | France vs Morocco | 1.52 | 3.79 | 6.79 |
| 22:00 | 3824 | Tottenham W vs Everton W | 1.97 | 3.40 | 3.35 |
| 22:45 | 2393 | Havant and Waterlooville vs Dartford | 1.67 | 3.74 | 4.27 |
| 23:45 | 3576 | Covilha vs Nacional Madeira | 2.86 | 3.05 | 2.37 |
| 23:45 | 3696 | Portimonense vs Gil Vicente | 2.00 | 3.26 | 3.40 |

ALHAMISI - 15/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3772 | Turan Tovuz vs Neftchi Baku | 5.27 | 3.61 | 1.58 |
| 14:00 | 3998 | Shijiazhuang vs Henan Jianye | 2.52 | 3.35 | 2.47 |
| 14:30 | 1722 | Hangzhou NG vs Chengdu Qianbao | 2.00 | 3.31 | 3.36 |
| 14:30 | 3254 | Meizhou Kejia vs Shanghai SIPG | 4.28 | 3.60 | 1.70 |
| 17:30 | 3969 | Al Ahli Manama vs Al Shabbab | 1.85 | 3.31 | 3.89 |
| 18:00 | 1298 | El Ittihad Alexandria vs Farco FC | 2.18 | 2.69 | 4.08 |
| 18:00 | 2533 | El Daklyeh vs Smouha Club | 3.90 | 3.00 | 2.08 |
| 18:30 | 1772 | Panathinaikos vs Volos | 1.33 | 4.59 | 7.80 |
| 20:00 | 2161 | EN Paralimni vs AEL Limassol | 3.30 | 3.20 | 2.20 |
| 20:00 | 4463 | Apollon Limassol vs Doxa Katokopia | 1.40 | 4.51 | 7.41 |
| 20:00 | 4882 | Arab Contractors vs Enppi Club | 2.28 | 2.70 | 3.80 |
| 20:30 | 1259 | Al Shabab Riyadh vs Al Ittihad Jeddah | 2.05 | 3.54 | 3.34 |
| 20:30 | 1769 | Al Hidd Club vs Al Hala Muharraq | 2.65 | 2.90 | 2.85 |
| 20:30 | 4792 | Olympiakos vs Atromitos | 1.26 | 5.06 | 8.95 |
| 20:30 | 5104 | Bahrain Club vs AL Khalidiyah | 5.27 | 3.56 | 1.59 |
| 21:00 | 2916 | Steaua Bucuresti vs CFR Cluj | 2.52 | 3.06 | 2.81 |
| 22:00 | 4057 | Jong PSV vs Jong Ajax | 2.13 | 3.66 | 2.92 |
| 22:30 | 3830 | Kifisias vs AEK Athens | 8.94 | 5.25 | 1.25 |
| 23:00 | 5080 | Rangers vs Hibernian | 1.31 | 5.17 | 8.35 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WAGOMBEA 13 WAJITOKEZA KUWANIA KUIONGOZA SIMBA

**Na Saada Akida**

WAGOMBEA 13 wamejitokeza kuchukua na kurudisha fomu za kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Klabu ya Simba utakaofanyika Januari 29, mwakani.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Simba, Boniface Lihamwike, alisema kati ya wagombea hao wanne wanawania nafasi ya mwenyekiti na tisa nafasi ya ujumbe wa bodi ya wakurugenzi wa klabu hiyo.

Aliwataja miongoni mwa waliojitokeza kuchukua fomu ya kuwania nafasi ya uenyekiti ni aliyekuwa Mtunza Fedha wa klabu hiyo, Yussuph Nassoro Majid, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Viwango Zanzibar.

Wengine ni aliyewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa zamani wa klabu hiyo, Geoffrey Nyange 'Kaburu', Omary Yenga, Eng. Rashid Khomeini na Murtaza Mangungu anayetetea nafasi yake hiyo.

"Katika nafasi ya ujumbe wa bodi ya wakurugenzi hadi sasa waliochukua fomu ni wagombea tisa ambao ni Iddy Kajuna, Abubakari Zebo, Hawa Mwaifunga, Lauren Mganga, Elisony Edward Mweladzi, Lameck Lawrence na Abdallah Migomba," alisema.

Alisema mchakato wa kuchukua na kurudisha fomu ulianza rasmi Desemba 5, mwaka huu na unatarajiwa kuhitimishwa Jumatatu ijayo ya Desemba 19.

"Desemba 20, ukaguzi wa fomu zilizorudishwa ndani ya muda utafanyika, Desemba 22 hadi 24 itakuwa siku za usaili wa watia nia wakati Desemba 29, mwaka huu ikiwa maalum kwa ajili kupokea mapingamizi dhidi ya wagombea."

Alisema Januari Mosi hadi 4, mwakani itakuwa siku za kusikiliza na kutoa uamuzi wa mapingamizi wakati Januari 5 itakuwa ni kutangaza majina ya wagombea waliokidhi vigezo huku Januari 6 hadi 28 zitakuwa siku za kampeni kwa waliopita na baada ya hapo siku inayofuata Januari 29, ndipo uchaguzi wa kupata viongozi wapya wa Simba utafanyika.

Alisema kwa mujibu wa kanuni, mwenyekiti atakayechaguliwa atakuwa na nafasi ya kuchagua wajumbe wawili na kufanya idadi kufikia nane.




Msanii wa Hip Hop, George Mdemu 'G Nako' (kushoto), akipata maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha Gama, Wilfred Magotti, kuhusu namna ya kushiriki mchezo wa bahati nasibu unaoendeshwa na kampuni hiyo, wakati wa uzinduzi wa Bahati SMS, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Saido atimka, Simba yatajwa

INATOKA UK. 32

George Mpole na kuna wengine hatutakuwa nao, hivyo nitakiboresha kikosi na kama watabaki basi nitaendelea nao," alisema Minziro.

Aidha, Minziro alisema anahitaji kuwa na kikosi chenye ushindani zaidi katika mzunguko wa pili hata kama baadhi ya wachezaji wataondoka.

Saido ameisaidia Geita Gold kumaliza mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya tano baada ya kuhusika katika mabao 10, akifunga manne na kutoa pasi za mwisho ('assist') nne.

# SIMBA NA REKODI KWA MKAPA

INATOKA UK. 32

kwa hiyo hata hao Raja Casablanca wakae wakijua kuwa wakija huku wajue wamekuja machinjioni."

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kuwa baada ya kuipata droo juzi, tayari wameshaanza maandalizi ya michuano hiyo.

Alisema kundi walilopangwa si la kubeza kwani lina timu nzuri ambazo mpaka kufika hapo kuna kazi imefanyika, lakini watapambana kuhakikisha wanavuka.

"Sisi ukiangalia ni kama tumepelekwa nyumbani, tuna TP Mazembe kwenye kundi letu, ukiangalia tuna wachezaji wengi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambao wanatoka huko, halafu kuna Real Bamako ambako kipa wetu Djigui Diarra anatokea, pia tuna US Monastir ya Tunisia, huku ndiko kabisa kwenye mji ambao kocha wetu Nasreddine Nabi anatoka, kwa hiyo ni kama tumepelekwa nyumbani.

"Hatutokuwa na ugeni sana kwa sababu tuna watu ambao wanatoka kwenye nchi ambazo tumepangiwa nazo. Lakini mbali na yote tutafanya maandalizi makubwa ya kukabiliana na mechi hizo," alisema Kamwe.

Simba imepangwa na timu za Raja Casablanca ya Morocco, Horoya ya Guinea na Vipers ya Uganda zikiwa Kundi C Ligi ya Mabingwa na Yanga kwenye Kundi D, Kombe la Shirikisho Afrika iko na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Real Bamako ya Mali na US Monastir ya Tunisia.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi na CAF, Simba itaanzia ugenini nchini Guinea dhidi ya Horoya FC kati ya Februari 10-12, kabla ya kurejea nyumbani kuikaribisha Raja Casablanca Februari 17-19 na kisha Februari 24-26, mwakani kuifuata Vipers ya Uganda.

Kwa upande wa Yanga nayo itaanzia ugenini nchini Tunisia dhidi ya US Monastir Februari 12 na kisha kurejea nyumbani kuikaribisha TP Mazembe Februari 19 kabla ya kuhitimisha raundi ya kwanza kwa kuifuata Real Bamako ya Mali Februari, 26, mwakani.

# Michezo

Jumatano Desemba 14, 2022

Nipashe




UKURASA 29

**Ronaldo: Neymar atarudi Kombe la Dunia na nguvu**

# SIMBA NA REKODI KWA MKAPA CAF, YANGA SC...

## ●●●Kila moja yaeleza ugumu na ahueni, Wekundu wa Msimbazi waja na tisa kwa Mkapa, wenzao watambia kunufaika na...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba imetamka kuwa malengo yao kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa ni yale yale, kukusanya pointi zote tisa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kama ambavyo imekuwa ikifanywa mara zote na watani zao, Yanga wamesema droo ya Kombe la Shirikisho barani Afrika iliyotoka juzi na kupangwa Kundi D ni kama wamepelekwa nyumbani. Klabu hizo zinazoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, zimesema hayo baada ya droo iliyochezeshwa juzi jijini Cairo, Misri, Simba ikiangukia Kundi C Ligi ya Mabingwa na Yanga ikipangwa Kundi D, Kombe la Shirikisho Afrika.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema wamefurahi kupangwa kwenye kundi hilo haswa kuwekwa na timu ambazo hawajawahi kucheza nazo hata mara moja.

Alisema kuwa malengo ya Simba ni yale yale ambayo wamekuwa wakiyafanya huko nyuma, kupata pointi tatu kwenye kila mechi itakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tumefurahi kupangiwa na timu ambazo hatujawahi kucheza nazo, tutakwenda kucheza na timu bora kama Raja Casablanca nchini Morocco kwenye uwanja wao ambao unaingiza watazamaji 67,000, ni mkubwa zaidi ya Benjamin Mkapa, tunakwenda Guinea kucheza na Horoya, ni Afrika ya mbali sana huko, halafu tunakwenda Uganda hapa karibu.

"Tunakwenda tukiwa na malengo yale yale ya kupata pointi tisa nyumbani, halafu huko kwingine tutaangalia majaliwa ya Mungu na ubora wetu utaamua, kwa hiyo niwaambie wanachama na mashabiki wa Simba kampeni ni ile ile, tisa Benjamin Mkapa ni haki yetu na 'kwa Mkapa hatoki mtu'," alisema na kuongeza:

"Huku ndiko kwenye maeneo yetu ya kujidai, kipenga cha Ligi ya Mabingwa kikipulizwa wachezaji wa Simba wanakuwa ni tofauti na wale uliowazoea, kama wamelishwa sumu,

INAENDELEA UK. 31

**NI HIVI...**



Kylian Mbappe, akipata maelezo kutoka kwa Kocha Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps, wakati wa mazoezi jana nchini Qatar kujiandaa na mechi ya nusu fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Morocco leo. **PICHA: MTANDAO**

## Saido atimka, Simba yatajwa

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, amempa mkono wa kwaheri nyota wake wa Kimataifa, Saido Ntibazonkiza, anayetajwa kutakiwa na klabu kadhaa ikiwamo wawakilishi wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba.

Ntibazonkiza alitua Geita Gold katika usajili uliopita akitokea Yanga ambapo anatajwa kutakiwa na Simba huku timu lukuki zikiendelea kumtangazia ofa.

Akizungumza na Nipashe jana, Minziro alisema anajisikia fahari kuona mchezaji anayemfundisha akitakiwa na timu mbalimbali na kudai kuwa anaimani atapata mbadala wake kwenye usajili wa dirisha dogo linalotarajiwa kuwa wazi kesho.

"Ni fahari kwa kocha kuona unamfundisha mchezaji kisha anatakiwa na timu nyingine, pia ni juhudi zake mwenyewe amekuwa akizionyesha zimemsaidia, ametokea Yanga sasa Simba inamhitaji pia kuna timu nyingine kama mbili tatu hivi zote zinamtaka.

"Yeye mwenyewe ndio ataangalia ofa yake aone atakwenda wapi kwa kuwa mwenye maamuzi ni yeye kuangalia wapi patamfaa ili aweze kwenda kujiunga. Kwa sasa mchezaji huyo hayupo kikosini nadhani ameenda kwao simu yake haipatikani.

"Kwa upande wangu nitaangalia wachezaji wangu walipungua ili niweze kuongeza nguvu dirisha dogo, ukiachana na Saido pia tayari tumeshaachana na mchezaji wetu,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >